# MWINGILIANO WA FASIHI NA HISTORIA KATIKA *UTENZI WA NCHUU CWAVO YAPO TINI MWA IRARA* (MTU NI KWAO JAPO CHINI MWA IRARA)

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

ROSE MUTHEU MUNYAO

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamiii katika Chuo Kikuu Cha Nairobi**

**Novemba, 2017**

A1701784A
University of Nairobi Library Thesis
2016

# MWINGILIANO WA FASIHI NA HISTORIA KATIKA *UTENZI WA NCHUU CWAVO YAPO TINI MWA IRARA* (MTU NI KWAO JAPO CHINI MWA IRARA)

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

ROSE MUTHEU MUNYAO

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi**

**Novemba, 2017**

A1701784A
University of Nairobi Library Thesis
2016

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

____________________ Tarehe 17/11/2017.

Rose M. Munyao
(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

____________________ Tarehe 17/11/17

Prof. Kineene wa Mutiso
(Msimamizi)

____________________ Tarehe 17/11/2017

Bw. Samson Ongarora
(Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mamangu mzazi kwa kunisomesha nikapata msingi wa elimu. Pia, marehemu nyanyangu na babu yangu kwa kunilea na kunipa maadili. Mungu awabariki.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na neema ya kufanya kazi hii. Nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Kineene wa Mutiso na Bw. Samson Ongarora kwa mawaidha na subira zilizochangia kufanikiwa kwa kazi hii. Aidha, nawashukuru wahadhiri wengine katika Chuo Kikuu cha Nairobi ambao walinifunza au kunipa mawaidha ya kiusomi kipindi chote nilipokuwa masomoni. Nao ni: Mwenyekiti wa idara ya Kiswahili Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kineene Wa Mutiso, Prof Rayya Timammy, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Evans Mbuthia na Dkt Prisca Jerono miongoni mwa wengine. Shukrani za dhati ziwaendee wanafunzi wenzangu tulioshirikiana katika masomo ya shahada ya uzamili. Pia, namshukuru mume wangu mpendwa Bw. Abedi na wanangu Lance na Shammah kwa kunivumilia, kunitia moyo na kuniombea nilipokuwa naendelea na masomo yangu. Mwisho, singeweza kuwataja wote waliochangia kazi hii mmoja mmoja, lakini natoa shukrani za dhati kwa nyote mliochangia kwa njia moja au nyingine kufanikisha tasnifu hii.

# IKISIRI

Tasnifu hii inahusu mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* wa Abubaker M.B. Khuchi. Kazi hii ilikuwa na malengo mahususi matatu; kwanza, kuhakiki mchango wa historia katika kufumbata dhamira ya mwandishi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Pili, kuchanganua kwa kina maudhui kama kipengele cha fasihi katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* na mwisho kutathmini mchango wa mandhari katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Tuliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa katika kuchanganua kazi hii. Tumefanya uchanganuzi wa maudhui kama kipengele cha fasihi kwa kina. Aidha, tumechanganua mchango wa mandhari katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* na kubaini kuwa kazi hii imejengwa katika mandhari halisi inayofahamika na wanajamii. Vilevile, tumechunguza jinsi historia na fasihi zinavyoingiliana na kutegemeana kwa ujumla kabla ya kujibu swali letu la utafiti la mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa mtunzi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ameathiriwa na historia ya jamii yake kwa kiwango kikubwa.

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| G.S.U | - | General Service Unit |
| Mh | - | mwaka haujabainika |
| Nw | - | na wengine |
| TJRC | - | Truth, Justice, and Reconcilliation Commission |
| TY | - | Tafsiri Yetu |
| UNCHR | - | United Nations Commission on Human Rights |

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii

TABARUKU ........ iii

SHUKRANI ........ iv

IKISIRI ........ v

VIFUPISHO ........ vi

YALIYOMO ........ vii

**SURA YA KWANZA ........ 1**

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Tatizo la utafiti ........ 5

1.3 Maswali ya utafiti ........ 7

1.4 Malengo ya utafiti ........ 7

1.5 Sababu ya kuchagua mada ........ 7

1.6 Upeo na mipaka ........ 9

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 9

1.9 Msingi wa kinadharia ........ 16

1.9.1 Mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa ........ 18

1.9.2 Matumizi ya mihimili ya uhalisia wa kijamaa ........ 20

1.10 Njia za utafiti ........ 21

1.11 Hitimisho ........ 21

**SURA YA PILI: MWINGILIANO KATI YA FASIHI NA HISTORIA ........ 22**

2.1 Utangulizi ........ 22

2.2 Historia na fasihi ........ 22

2.3 Kutegemeana kwa fasihi na historia ........ 24

2.4 Kazi za kubuni za kihistoria ..... 26

2.5 Vipengele fafanuzi vya hadithi ya kubuni ya kihistoria. ..... 27

2.5.1 Uhusika ..... 27

2.5.2 Mandhari ..... 27

2.5.3 Mtiririko ..... 27

2.5.4 Maudhui ..... 28

2.5.5 Mbinu za lugha ..... 28

2.5.6 Hisia ..... 29

2.6 Ujumbe wa ujumla katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ..... 29

2.7 Historia ya Wabajuni ..... 30

2.7.1 Mtazamo wa Wabajuni ..... 33

2.8 Masuala ya kihistoria katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ..... 39

2.8.1 Mandhari ..... 39

2.8.2 Matukio ya kihistoria ..... 40

2.9 Hitimisho ..... 43

**SURA YA TATU: MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA NCHUU CWAVO YAPO TINI MWA IRARA*** ..... **44**

3.1 Utangulizi ..... 44

3.2 Dhana ya maudhui ..... 44

3.2.1 Dini ..... 45

3.2.2 Ukoloni mamboleo ..... 46

3.2.3 Dhuluma /Ukatili ..... 47

3.2.4 Ukiukaji wa haki za kibinadamu ..... 49

3.2.5 Vifo/ Tanzia ..... 50

3.2.6 Uchumi na mali ..... 51

3.2.7 Udugu/Ushirikiano ... 52

3.2.8 Woga ... 53

3.2.9 Utabaka ... 54

3.2.10 Ujenzi wa jamii mpya ... 55

3.2.11 Ukandamizaji ... 56

3.2.12 Utengano ... 57

3.2.13 Usaliti ... 58

3.2.14 Ukimbizi ... 59

3.2.15 Nafasi ya mwanamke ... 60

3.3 Hitimisho ... 60

**SURA YA NNE: MANDHARI NA DHAMIRA KATIKA UTENZI WA NCHUU *CWAVO YAPO TINI MWA IRARA* ... 62**

4.1 Utangulizi ... 62

4.2 Mandhari na dhamira ya mwandishi ... 62

4.3 Mandhari za Kijiografia ... 64

4.3.1 Mandhari ya Kiunga ... 64

4.3.2 Mandhari ya Witu ... 66

4.3.3 Mandhari ya Mtungui ... 66

4.3.4 Mandhari ya Mkunumbi na Mararani ... 67

4.3.5 Mandhari ya Mkwajuni ... 67

4.3.6 Mandhari ya Ngomeni ... 68

4.3.7 Mandhari ya Bura ... 68

4.4 Mandhari za Kihistoria ... 69

4.5 Dhamira katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ... 69

4.6 Hitimisho ... 72

**SURA YA TANO: MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .............. 73**

5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 73

5.2 Matokeo ya utafiti kuhusiana na maswali ya utafiti ........................................... 73

5.3 Matatizo yaliyojitokeza kutokana na utafiti ....................................................... 77

5.4 Hitimisho na mapendekezo ya utafiti zaidi ....................................................... 77

5.4.1 Hitimisho ................................................................................................ 77

5.4.2 Mapendekezo ya utafiti zaidi ................................................................. 78

**MAREJELEO ........................................................................................................ 79**

**VIAMBATISHO .................................................................................................... 81**

## SURA YA KWANZA

### 1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Kazi hii ina sura tano. Sura ya kwanza inaeleza kuhusu utangulizi kwa ujumla, maswali ya utafiti, lengo la utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia ya utafiti pamoja na mbinu zilizotumika kufanya utafiti. Sura ya pili inachunguza mwingiliano wa fasihi na historia. Sura ya tatu inafafanua maudhui katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Katika sura ya nne tumeeleza mandhari na umuhimu wake pamoja na dhamira katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Mwisho, katika sura ya tano tunatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo. Aidha, tunaangalia kama maswali ya utafiti yamejibiwa na malengo ya utafiti kutimizwa.

*Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ni miongoni mwa tenzi nyingi za jamii ya Waswahili hasa wanaozungumza na kuielewa lahaja ya Kibajuni. Utenzi huu una beti mia moja zilizo na mishororo miwili kwa kila ubeti. Umeandikwa kwa lahaja ya Kibajuni na kupewa fasiri ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kuwa utafiti wetu utachangia katika kuuelewa utenzi huu na kufaa kizazi cha sasa na kile kijacho cha wahakiki wa fasihi. Tuliuona utenzi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara,* kwa mara ya kwanza tukisoma kozi ya 'Swahili Poetry' na Prof. Kineene wa Mutiso katika darasa la uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Utenzi huu ulikuwa ni mojawapo ya tenzi nyingi tulizochambua pamoja na *Utenzi wa Vita vya Uhud*, *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Nguvumali* na tenzi zingine.

Ingawa haijabainika utenzi huu uliandikwa lini, mambo yanayozungumziwa yanaashiria kuwa uliandikwa katika kipindi cha baada ya nchi ya Kenya kujipatia

uhuru hadi miaka ya tisini baada ya mapinduzi ya kiongozi, Siad Bare katika nchi ya Somalia. Utenzi huu uliandikwa na Abubakar M.B Khuchi akieleza hali ya jamii ya Wabajuni na mambo waliyokuwa wamepitia. Mtunzi anaonyesha historia ya Wabajuni iliyojaa ubaguzi, unyanyasaji na mateso mengine mengi. Anaeleza hali ya Wabajuni kabla ya uhuru jinsi walivyokuwa wameendelea kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, baada ya uhuru, serikali haikuwatambua kama jamii. Kabla ya uhuru, Wabajuni walikuwa wameendelea katika usanii, uvuvi, uundaji wa dau na mengine.Wabajuni waligawanywa baada ya vita vya kiongozi Said Bare. Wengine walikaa Kiunga, Kizingitini na Chundwa. Sababu za mgawanyo huu zilikuwa za kukabila na kikoloni kwani wakoloni walikuwa wameweka mipaka ya kikoloni iliyogawanya jamii nyingi hasa za pwani ya Afrika Mashariki kuwa za nchi ya Kenya au nchi ya Somalia. Kwa sababu hii walikosa kitambulisho. Vita vya Wasomali vya kuanzia sitini na moja vilifanya Wasomali kuhamia katika visiwa vya Wabajuni hadi sehemu ya Jomvu mjini Mombasa.

Kulingana na Walsh (2010), akirejelea kazi ya Vinigi (1955), anasema kuwa, kazi hii inachukuliwa kuwa mojawapo ya kazi nzuri za utafiti kuhusu Waswahili wa mashambani wanaozungumza lugha ya Kiswahili. Kazi hii ni chanzo kikuu cha maelezo ya Kisayansi kuhusu Wabajuni (Wagunya au Watikuu ) ambao kidesturi himaya yao inajumuisha sehemu ndefu ya pwani iliyo na makazi pamoja na visiwa kati ya Kismayu (Somalia) upande wa kaskazini na Lamu (Kenya) upande wa kusini. Msukosuko wa kisiasa katika miongo ya hivi karibuni nchini Somalia uliifanya kazi hii kuwa maandishi ya kihistoria yenye thamani kwa kutoa rekodi ya jinsi maisha ya maelfu ya Wabajuni yalivyopondwapondwa kupitia mateso na migogoro iliyowapata kutokana na migogoro hii ya kisiasa.

Wabajuni walio wachache nchini Somalia hawakuwa na maisha mazuri sana wakati wa utawala wa Mohamed Siad Barre (1969 -1991) na walipitia ubaguzi na mambo yaliyowavunjia heshima. Mnamo mwaka 1974, wavuvi na vifaa vyao vya uvuvi vilichukuliwa na wakashinikizwa kujiunga na mashirika ya Ushirika ya Kiserikali na wengine wakalazimishwa kutoka visiwa vya Bajuni (Abby 2005). Lakini mambo yalizidi kuwa mabaya baada ya mkurupuko wa vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Somalia baada ya kung'atuliwa mamlakani kwa Siad Barre, Januari, 1991. Wabajuni walijiunga na watu wengi walioonewa na wakatoroka nchi ya Somalia huku wengi wao wakikimbilia kambi ya wakimbizi ya UNHCR ndani na viungani mwa mji wa Mombasa ambapo kambi ya 'Kwa Jomvi' ilikuwa makazi makuu mpaka mwaka wa 1998 ilipofungwa (TY) .

Wamitila (2008) anaeleza fasihi kama sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa au huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. King'ei na Amata (2011), wanasema fasihi ni sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe maalum unaomhusu binadamu kupitia tungo kama vile; mashairi, riwaya, tamthilia, tenzi, misemo, vitendawili, hadithi, ngano, methali na kadhalika. Hivyo basi, fasihi itachukuliwa kuwa sanaa inayotumia lugha kupitisha ujumbe unaomhusu binadamu kwa njia ya maandishi au mdomo na hulenga kugusa hisia za hadhira na huwasilishwa kwa tanzu mbalimbali. Fasihi hutumiwa kama chombo cha kutetea maslahi ya kikundi kimoja na kingine. Katika kazi ya uandishi, mwandishi huwa na madhumuni ya ya kupitisha ujumbe fulani kwa hadhira. Wanaosoma kazi hii wanaweza kuikubali au kuikataa. Baadhi ya mambo wanayoweza kuzingatia ni kama fani, mfumo wa siasa unaoongoza jamii hiyo au jinsi mwandishi anavyoainisha na kuwasilisha kazi yake.

King'ei na Amata (2011) wanasema kuwa sababu kuu ya kuandika kazi ya fasihi ni kuonyesha jinsi jamii ilivyo kama vile inavyofurahishwa au kuhuzunishwa na matukio yanayoikumba, matatizo wanayoyapitia, utetezi, sifa na kashfa wanazokumbana nazo pamoja na mwelekeo waliouchukua. Fasihi huzaliwa katika jamii katika wakati fulani wa historia ya jamii hiyo. Ni muhimu kueleza kuwa mambo anayozungumzia mwanafasihi, hutokana na mambo yanayomzingira na kipindi halisi cha kihistoria inachopitia jamii ya mwanafasihi. Mwanafasihi ni mwanajamii na kwa hivyo huwa ameathiriwa sana kisaikolojia na mambo yanayofanyika katika jamii anamoishi. Vilevile, mwanafasihi anapojenga kazi yake, hujihusisha na mambo anayoyaona kuwa muhimu kutokana na yale anayoyafahamu kuhusu jamii alikozaliwa na alikoishi.

Kapiyo na wenzake (2011) wanasema historia ina maana ya maelezo ya matukio yaliyotendeka wakati uliopita. Pia, historia ni tawi la elimu linaloshughulikia matukio ya wakati uliopita ya wanadamu na kuathirika kwao na mazingira yao kwa miaka kadhaa (TY). Kuwepo kwa fasihi kunaathiriwa na masuala ya kihistoria. Kila mara msomaji anaposoma kazi ya fasihi huhitaji kuelewa wakati wa kihistoria ambapo kazi hiyo ilitungwa ili kuithamini na kuielewa kazi hiyo. Tofauti kuu kati ya historia na fasihi ni kuwa mwanahistoria anarekodi mambo kama yanavyotokea ilhali mwanafasihi anatafsiri matukio ya kila siku kwa njia ya ubunifu. Kwa vyovyote vile, historia na fasihi hutegemeana. Katika hali halisi ya jamii, matukio halisi ya kihistoria yamekuwa yakipokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia za hadithi kama vile mighani ambapo jamii hujulishwa kuhusu asili yao pamoja na masuala mengine kuhusu jamii hiyo.

Hata hivyo, ni muhimu kutaja kuwa kazi ya fasihi wakati mwingine huongeza chuku ili kuvuta makini ya hadhira labda kwa lengo la kutumbuiza au kwa kuweka hali ya taharuki ili kuichochea hadhira zaidi. Wanahistoria hutafuta ushahidi kupitia mambo yaliyotokea katika maisha ya kila siku. Lengo la mwanafasihi aidha ni kufafanua matukio ya kihistoria na kuyafasiri na kuyawasilisha kwa hadhira. Ni muhimu kufahamu kuwa mwanahistoria anaweza kubadili ujumbe kutegemea hadhira yake naye mwanafasihi anaweza kutumia ubunifu na usanii wake kufafanua matukio kwa njia inayoweza kuondoa uhalisia. Kama tulivyotaja hapo awali, mara nyingi unaposoma kazi ya fasihi ni muhimu kuelewa wakati wa kihistoria ili kuielewa kazi hiyo. Hata hivyo, mwandishi anaweza kuamua kueleza suala la kihistoria jinsi lilivyo ili kuwaelimisha wanajamii. Mwanafasihi pia ana uhuru wa kuandika kazi kwa ubunifu tu bila kuzingatia suala lolote la kihistoria bali akiwa na lengo la kupitisha ujumbe wake ama akaamua kuifinyanga historia hiyo kiubunifu. Ni kwa sababu hii ambapo utafiti huu utatathmini mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

## 1.2 Tatizo la utafiti

Kumekuwa na mjadala kuhusu suala la uhusiano uliopo kati ya historia na fasihi. Mjadala huu umeibua masuala mengi kuhusu historia na fasihi. Kuna wale wanaodai kuwa kila kazi ya fasihi hutokana na tukio fulani la kihistoria. Wengine wanahisi kuwa fasihi ni kazi ya ubunifu na inaweza kuwepo pasipo kurejelea tukio la kihistoria. Pia, fasihi kama taaluma ni sanaa ambayo hutumia lugha kupitisha ujumbe unaomhusu binadamu. Ujumbe huu unasawiri mambo yote yanayomhusu binadamu kama vile mahusiano yake ya kijamii na kisiasa pamoja na shughuli zake za kila siku. Hata hivyo, mwanahistoria naye, huandika kazi zake akirejelea mambo yaliyotendeka katika jamii yake wakati uliopita.

Mwanahistoria anaweza kuzungumzia mambo mbalimbali yanayohusu jamii yake kama vile dini, siasa, utamaduni, uongozi na kadhalika. Mwanafasihi naye, hupata ujumbe wa kazi yake kutokana na masuala yanayomzunguka ya kijamii. Vilevile, ni muhimu kutaja kuwa, fasihi inaweza kubadilishwa kuwa historia baada ya muda mrefu. Pia, mambo anayoyapitia mtu huwekwa uhai kwa kuandikwa kwa njia ya ubunifu kama fasihi. Hii ina maana kuwa fasihi na historia ni taaluma zinazotegemeana kwa kiasi fulani. Mwanafasihi hujipata katika hali tata anapotaka kuandika kuhusu matukio ya kihistoria kwani wakati mwingine kazi kama hiyo inaweza kuchukuliwa kama ya kihistoria. Hata hivyo, ili kazi ikubalike kama ya fasihi lazima izingate vipengele vya kimsingi kama vile: kuwa na wahusika, dhamira, maudhui, mandhari pamoja na mbinu za sanaa.

Kumekuwa na kazi nyingi ambazo zimeandikwa kuhusu masuala ya historia ya jamii kama vile: *Utenzi wa Uhuru wa Kenya, Zinduko la Ujamaa, Utenzi wa Nguvumali* na tenzi zingine. Kazi zilizotajwa zinazungumzia matukio ya kihistoria ya jamii husika. Masuala ya kihistoria yamekuwa kichochezi cha uandishi wa kazi za fasihi tangu jadi. Ni muhimu kubainisha vipengele vya kimsingi vinavyotambulisha kazi za fasihi na za kihistoria. Utenzi ni sehemu ya vipera vya fasihi. *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* unazungumzia historia ya Wabajuni pamoja na mateso waliyoyapata Wabajuni baada ya Ukoloni. Hata hivyo, utafiti wetu wa tenzi pamoja na uhakiki uliofanywa kwa baadhi ya tenzi unaonyesha kuwa hakuna uhakiki uliowahi kufanywa kubainisha mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ambao unaohusu jamii ya Wabajuni. Utafiti huu ulibainisha masuala ya kihistoria yanayojitokeza katika utenzi huu ili kujibu swali letu la kutathmini mwingiliano wa fasihi na historia katika utenzi huu.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Swali kuu la utafiti huu ni: Kuna mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara ?*

Katika uchunguzi huu tulijibu maswali mahususi yafuatayo:

*i)* Historia imechangia vipi katika kujenga dhamira ya mwandishi katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara ?*

*ii)* Ni maudhui yapi yanayojitokeza katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara?*

*iii)* Mandhari yana umuhimu gani katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara ?*

## 1.4 Malengo ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

Uchunguzi huu ulitazamia kutimiza malengo mahususi yafuatayo:

i) Kuhakiki mchango wa historia katika kufumbata dhamira ya mwandishi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

ii) Kuchanganua kwa kina maudhui kama kipengele cha fasihi katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

iii) Kutathmini mchango wa mandhari katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

## 1.5 Sababu ya kuchagua mada

Utenzi huu ni mojawapo kati ya tenzi nyingi katika jamii ya Waswahili ambao umeandikwa kwa lahaja ya Kibajuni na kufasiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Mtunzi anazungumzia historia ya Wabajuni ambayo kuifahamu kwake kutasaidia katika

jitihada zao za kujitambulisha pamoja na jamii pana kufahamu jitihada hizo. Hii ni mojawapo ya sababu zilizotuchochea kuchagua mada hii. Vilevile, wahakiki wengi wa kifasihi hawajaushughulikia utenzi huu. Kwa hivyo, kwa kuuhakiki utenzi huu tumeziba pengo hilo la kiusomi.

Isitoshe, katika uchunguzi wa tafiti za awali zilizofanywa, hatujapata wahakiki wa utenzi huu ikilinganishwa na tenzi zingine za wakati huu kama vile *Utenzi wa Mwanakupona*, *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Nguvumali*, *Utenzi wa Al-Inkishafi* na tenzi zingine. Ni kwa sababu hii ambapo tulikuwa na shauku ya kuutafiti utenzi huu ili kujaribu kuziba pengo la ukosefu wa marejeleo. Uchunguzi wetu wa tenzi pamoja na uhakiki uliofanywa kwa baadhi ya tenzi unaonyesha wazi kuwa hakuna uhakiki wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* isipokuwa yale tulikuwa tumefundishwa darasani katika kozi ya *Swahili Poetry* ili kutimiza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Hata ingawa utenzi huu umefasiriwa kwa lahaja ya Kiswahili sanifu, umeandikwa kwa lahaja ya Kibajuni na hivyo utawafanya wanafasihi kuhamasishwa zaidi kuhusu lahaja ya Kibajuni kwa sababu ni sehemu ya fasihi na historia ya Kiswahili kwa jumla. Hata hivyo, suala la historia ya Wabajuni limeshughulikiwa katika miktadha ya kihistoria lakini sio katika mazingira ya kifasihi na hili lilituchochea kushughulikia masuala ya fasihi na historia katika utenzi huu.

Nurse (2010) anasema kuwa maandishi rasmi kuhusu utamaduni na lugha ya Wabajuni ni dhaifu na hupatikana tu katika akili za wazee wa Kibajuni lakini jinsi wanavyoendelea kufa ndivyo matumaini ya kunakili wanayoyafahamu yanavyoendelea kufifia. Madai haya ni kichochezi kwetu kwani utafiti huu umechangia katika kunakili na kuhifadhi baadhi ya masuala ya kiutamaduni na

historia kuhusu jamii ya Wabajuni. Ni matumaini yetu kuwa uhakiki huu umewafaa wasomi na wahakiki chipukizi wa somo la fasihi kwa jumla na kuwa utakuwa msingi wa kuwaongoza watafiti wengine kuhusu suala la historia na fasihi.

Jamii ya Wabajuni ni miongoni mwa jamii zilizo na idadi ndogo ya watu nchini. Hii ni jamii ambayo inatishiwa na kusahaulika na kupotea katika kumbukumbu ya jamii pana. Kama anavyosema mwandishi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini mwa Irara*, imekosa kitambulisho. Utafiti huu umechangia katika kukuza juhudi na harakati za Wabajuni kujitambulisha.

### 1.6 Upeo na mipaka

Kila kazi ya kiusomi huwa na mipaka na upeo. Utenzi huu unaweza kuhakikiwa kwa njia nyingi kama vile kifani, kimaudhui na hata kwa kutumia nadharia mbalimbali. Tulihakiki suala la mwingiliano wa fasihi na historia. Aidha, tuliangazia maudhui katika utenzi huu. Vilevile, tulichunguza dhamira ya mwandishi katika utenzi. Aidha, tuliangalia mandhari na umuhimu wake katika kazi hii. Tulitumia nadharia uhalisia wa kijamaa katika kuhakiki kazi yetu. Masuala ya lugha tumeyataja tu tukiendeleza utafiti wetu. Dhana ya historia na fasihi imetafitiwa kwa kina kwa lengo la kuielewa mihimili yake kabla ya kuihusisha na *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

### 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Udurusu wa yaliyoandikwa umetutia moyo kwani umeangazia mapengo ambayo utafiti wetu utaziba. Kama tulivyoeleza hapo awali, changamoto kubwa ya kutafiti kazi hii ni ukosefu wa marejeleo. Kazi nyingi ambazo zimetafitiwa kuhusu tenzi zinahusu mashairi ya zamani yaliyoandikwa kabla na mwanzo wa karne ya ishirini. Mashairi mengi ya wakati huu yalikuwa ya kidini. Hata hivyo, zipo tafiti ambazo zimefanywa kuhusu tenzi na hasa zikihusiana na historia ya jamii. Vilevile, kuna

makala ambayo yamezungumzia historia ya Wabajuni. Hizi ni baadhi ya kazi ambazo tulizipitia ili kufanikisha utafiti wetu.

Mohammed (1988) anadai kuwa *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* ni zao la historia ya Visiwa vya Unguja na Pemba. Anasema, historia hiyo, hasa tukio la mapinduzi ya Januari 1964, iliibua mhemko wa fasihi ya Kiswahili kutoka visiwani ambalo ilishtumu vitabu vilivyokosa kushughulikia mapinduzi hayo, kama vile vya kijasusi vya Muhammed Said Abdulla vya Mzimu wa Watu wa Kale ( 1960), *Kisima cha Giningi* ( 1960), *Duniani Kuna Watu* ( 1974) na *Siri ya Sifuri* (1975). Kazi hizi, zaidi ya kutoyasema mapinduzi hayo, zimetetea na hata kuuomba msamaha kwa sababu ya tamaa ya wakandamizaji. Kulingana naye, utenzi huu umeeleza sababu na kiini cha mapinduzi ya Zanzibar. Kutokana na maelezo aliyoyatoa mtunzi, mbinu za kimsingi zilizotumiwa na tawala hizo kandamizi kuwadhulumu watu wa Visiwani zilikuwa za umilikaji wa mali na biashara ya utumwa. Uhakiki wa kazi hii pamoja na utenzi huu ni wa manufaa kwa kazi yetu kwa kuwa umelinganisha matukio ya kihistoria na kazi ya fasihi ambayo ni msingi wa utafiti wetu.

Mwenda (2007) katika uhakiki wa "Upekee wa *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*: Utenzi wa Mpito, Mseto wa Imani za Jadi Na Usasa" anafafanua kwamba, *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* ni kazi ya kifasihi inayoelezea tukio lisilo la kawaida lililofanyika katika eneo la Kilwa. Kazi hii ya inaeleza jinsi kifo cha mwanamke mmoja kilivyosababishwa na kazi za kitamaduni kuhusu ushirikina na uchawi. Kifo hiki kilichangia kuitwa kwa mganga maarufu kwa jina Nguvumali. Utenzi huu umebeba utamaduni wa jamii ya bara ambayo ilikuwa inashikilia tamaduni na imani kuhusu uchawi na ushirikina pamoja na kushikilia dini ya Kiislamu. Kwa mujibu wa Ismaili (1968), kuna Mganga Nguvumali aliyewahi kuishi, mganga Mmatumbi

aliyekuwa amerithishwa uganga na Mngindo aliyeitwa Hamed Matoroka. Nguvumali wa kihistoria alipewa heshima kwa kuwa alionyesha umaarufu wa kiganga uliopunguza matumizi ya uchawi katika mji wa Kilwa. Hata hivyo, mtunzi anaonekana kuathiriwa na matukio ya Nguvumali wa kihistoria kama ilivyo katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ambapo anazungumzia kuhusu jamii ya Wabajuni.

Mwirabua (2009) katika kazi yake ya *Ukoloni Mamboleo na Utandawazi katika Tamthilia Teule* anasema kuwa ukuaji wa bara la Afrika umepitia awamu tofauti za kihistoria. Mwirabua alihakiki vitabu vya Afrika Mashariki. Anaeleza vipindi ambavyo bara hili limepitia kama vile: Kipindi cha utumwa cha karne ya 14, kipindi cha ukoloni mkongwe cha kame ya 19, kipindi cha ukoloni Mamboleo cha karne ya 20 na kipindi cha utandawazi cha karne ya 21. Anafafanua kwamba wale waliochukua hatamu za uongozi wa Afrika waliiga mitindo ya utawala wa kikoloni kama vile kuwepo kwa machifu, wakuu wa wilaya na mikoa. Vilevile, walichukua mitindo ya kielimu kutoka kwa wakoloni na kuiendeleza.

Kwa kuwa Waafrika hawa hawakuwa na uwezo wa kiuchumi walilazimika kuwafuata Wazungu kama vikaragosi wao. Isitoshe, Waafrika hawa waliwategemea Wazungu ili kupata misaada. Kupitia kuwatemegea Wazungu kwa kiasi kikubwa kulisababisha kukuzwa kwa ukoloni mamboleo pasipo kushughulikia maslahi ya nchi maskini za Kiafrika. Jambo hili lilisababisha nchi za kikoloni kuchukua rasilmali za nchi za Kiafrika. Mali ya Waafrika ambayo ilitwaliwa na wakoloni ilitumiwa kukuza uchumi wa nchi za kikoloni. Hata hivyo, Mwirabua anaeleza kuwa ukoloni mamboleo unaendelezwa katika jamii ya kisasa kupitia utandawazi ambao kwa kiwango kikubwa hutumika kudhulumu mataifa maskini.

Pia, Mwairabu anaeleza kuwa utandawazi huu unatumika kuwakandamiza na kuwanyanyasa watu wa mataifa maskini kiuchumi na kibiashara. Fauka ya haya, utandawazi huu ni mbinu mpya inayotumiwa na nchi za kimagharibi kuwakandamiza na kuwanyonya pamoja na kuwanyanyasa watu wa mataifa ya nchi zinazoendelea. Hata hivyo, utafiti wa Mwirabua uliongozwa na nadharia ya Baada ukoloni. Anaeleza kwamba kazi zinazoongozwa na nadharia ya baada ukoloni hukashifu kutumiwa kwa mataifa maskini ya ulimwengu wa tatu na mataifa matajiri kujiendeleza kiuchumi na kibiashara.

Kazi hii ni ya manufaa katika utafiti wetu kwa kuwa inazungumzia kuhusu ukoloni mamboleo ambao ni maudhui ya kimsingi katika kazi yetu. Vilevile, inachanganua masuala ya kihistoria kuhusu jamii za mataifa ya ulimwengu wa tatu. Hivyo basi itatusaidia katika kuhakiki suala la historia pamoja na maudhui ya ukoloni mambo leo katika kazi yetu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na kazi yetu kwa kuwa umechanganua ukoloni mamboleo na utandawazi katika tamthilia, nasi tutatathmini mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ambao unaohusu jamii ya Wabajuni.

Wataalamu mbalimbali wamezungumzia suala la historia ya jamii ya Wabajuni. Kulingana na Walsh (2010) kazi ya Vinigi (1955) inachukuliwa kuwa mojawapo ya kazi nzuri za utafiti kuhusu Waswahili wa mashambani wanaozungumza lugha ya Kiswahili. Kazi hii ni chanzo kikuu cha maelezo ya kisayansi kuhusu Wabajuni (Wagunya au Watikuu ) ambao kidesturi himaya yao inajumuisha sehemu ndefu ya pwani iliyo na makazi pamoja na visiwa kati ya Kismayu (Somalia) upande wa kaskazini na Lamu (Kenya) upande wa kusini. Msukosuko wa kisiasa katika miongo ya hivi karibuni nchini Somalia uliifanya kazi hii kuwa maandishi ya kihistoria yenye

thamani kwa kutoa rekodi ya jinsi maisha ya maelfu ya Wabajuni yalivyopondwapondwa na mateso na migogoro. Kazi hii itatusaidia kufahamu historia halisi ya Wabajuni. Baada ya kufahamu historia hii tutaweza kutathmini kama utenzi huu umeonyesha mambo halisi ya kihistoria yaliyowafika Wabajuni. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na utenzi huu kwa kuwa si ya kifasihi.

Nurse (2010) anasema kuwa maandishi rasmi kuhusu utamaduni na lugha ya Wabajuni ni dhaifu na hupatikana tu katika akili za wazee wa Kibajuni lakini jinsi wanavyoendelea kufa ndivyo matumaini ya kunakili wanayoyafahamu yanavyoendelea kufifia. Mwandishi huyu hata hivyo anasema ametoa madai yake kutokana na kazi zilizochapishwa na zingine ambazo hazijachapishwa za Alessandra Vianello, Brian na Tiffy Allen, Mohammed Bakari Mohammed (mzee kutoka kijiji cha Chula) Yusuf Omar Mwalim (mzee kutoka kijiji cha Chovae), Said Ahmed Abdurahman (Brava), *Bajuni.com*. Kuwepo kwa kazi kama hizi kutatusaidia kufanya utafiti wa kina kuhusu suala la historia ya Wabajuni ili kubainishia wasomaji masuala halisi ya kihistoria na kuyalinganisha na yanayozungumziwa katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Usawa kati ya Wabajuni, Wasomali na Waswahili ulibadilika katika mwaka 1991, wakati aliyekuwa Rais, Siad Barre, alipong'atuliwa mamlakani.

Migogoro na vita vya kikabila kati ya Wasomali na Wasomali, Wasomali na makabila yasiyo Wasomali viliongezeka. Mwanzoni, Wasomali walifurika kwenye visiwa na kama inavyotarajiwa kwenye makazi pia; hali hii ilisababisha fujo, vita, uharibifu na uchomaji wa mali, wizi, watu kupigwa, ubakaji na mauaji. Baadaye, Wasomali kutoka familia zilizovunjika ama Wasomali walio wachache walipewa makazi kwenye visiwa. Kikundi cha watu wanaozungumza lugha ya Kisomali kikaanzishwa

kwa mara ya kwanza katika historia na kiko hivyo hadi leo. Sio tu kabila la Wasomali lililohamia kwenye visiwa bali wengine kutoka bara waliohisi kutokuwa salama au ambao Shirika la Umoja wa Mataifa walihisi kutokuwa salama walihamishwa hadi kwenye visiwa pia (T.Y).

Wabajuni walibaguliwa wakati wa utawala wa Siad Barre nchini Somalia.Waliteswa na kudhulumiwa na makabila mengine nchini Somalia.Waliporwa mali yao na hata kulazimishwa kujiunga na mashirika ya ushirika ya kiserikali pamoja na kulazimishwa kuhama visiwa vya Bajuni. Kazi hii itatusaidia katika kulinganisha masuala yanayozungumziwa katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* kuhusu njia za kiuchumi na hali halisi ya kihistoria ya jamii ya Wabajuni.

Owallah (2013) katika Uhakiki wa Maudhui Teule katika *Utenzi wa Nabii Isa'* anaeleza kuhusu maudhui na mandhari katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Kwa kiwango fulani, *Utenzi wa Nabii Isa* ni wa kihistoria kwa kuwa mtunzi anazungumzia hali halisi kuhusu dini. Mhakiki huyu atatupatia mwelekeo kuhusu uhakiki wa maudhui na mandhari katika utenzi kwani maudhui ni kipengele teule cha uhakiki wetu wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Vilevile, utenzi huu ni tofauti na kazi yetu kwa kuwa unahakiki maudhui teule lakini sisi tutahakiki mwingiliano wa fasihi na historia.

Owallah kama hapo juu anasisitiza kuwa matukio yanayojitokeza katika kazi yoyote ya kifasihi pamoja na maudhui yanayohusishwa na matukio hayo yanatendeka mahali, wakati na katika mawanda fulani. Akimnukuu Wamitila (2008) anasema kwamba mandhari ni mazingira ya kimahali, kiwakati na ya kihistoria ambamo kazi fulani ya kifasihi inajikita. Basi ni dhahiri kuwa ili kuchunguza maudhui, mandhari ni msingi muhimu zaidi katika uchanganuzi huo. Uhakiki wake utakuwa wa manufaa

kwetu katika uelewa na uchambuzi wa maudhui ya *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Kazi hii ni msingi mkuu katika kutuongoza katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa na jinsi nadharia hii inavyoweza kutumika katika kuhakiki kazi ya fasihi. Hata hivyo, kazi hii imetumia nadharia hii katika tamthilia teule nasi tumetathmini mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*.

Onchwati (2016) inayohusu "Uhalisiajabu unavyojitokeza katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*" anaeleza kuwa fasihi huonyesha mambo yanayotendeka katika jamii. Tenzi ni sehemu ya fasihi, hivyo basi huonyesha masuala yanayotendeka katika jamii. Onchwati kama hapo juu anafafanua kwamba, jamii ya Waswahili hasa Waislamu hupata nafasi ya kujua historia ya jamii yao kutokana na kazi za fasihi kama tenzi . Jamii inapoangalia sifa za uhalisi ajabu hupata kuelewa mafanikio, mateso, mahangaiko na dhuluma nyingine ambazo wahusika wanaotajwa hukumbana nao. Changamoto za kijamii huwapata wahusika mbalimbali katika tenzi au kazi ya fasihii ambayo wanajitokeza. Jamii hupata historia yake kupitia sifa zinazojitokeza kupitia kwa wahusika hawa.

Onchwati pia anaeleza sifa za kiuhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*, zilinazopelekea kumulika baadhi ya miji walikozaliwa, walikokulia, walikolelewa, walikotembelea na hata walikopigania. Kwa mfano, katika *Ukawafi wa Miiraji* anaeleza vile Mtume Mohammed alivyotembea katika miji ya Medina, Bedar, Yathribu na Makkah na miji mingine. Umuhimu wa kuielewa miji hii ya Kiislamu husaidia katika kutambua na kufahamu chimbuko na kukua kwa dini ya Kiislamu pamoja na Kufahamu jamii yao. Kupitia kueleza historia ya miji hii ya Waislamu, wasomaji hupata nafasi ya kuelewa asili ya dini yao kwani

ufahamu huo ni nguzo muhimu ya kuielewa historia na jamii yao. Ufafanuzi wa sifa hizi za ajabu ndani ya *Ukawafi wa Miiraji* unatokeza majina ya kiukoo ya watu wa nasaba ya Mtume Mohammed. Miji aliyopitia Fumo Liyongo inatajwa katika utenzi huu ikiwemo Shaka, Ozi, Pate, na miji mingine. Ufahamu huu ni muhimu katika kueleza sifa za Fumo Liyongo.

Fumo Liyongo aliogelea katika mto Tana ambao unafahamika kihistoria. Hata hivyo, majina ya vifaa maridhawa alivyotumia Fumo Liyongo vinavyotajwa ni pamoja na miti, misitu, na maisha ya majirani kama vile Wadahalo na Wasanye. Hii inaonyesha kuwa mazingira yanayozungumziwa katika utenzi huu ni halisi na hivyo basi kukuza uelewa wa utenzi huu. Kazi hii itatusaidia katika kueleza vile fasihi inavyosaidia jamii katika kuielewa historia yake. Tenzi hizi zimetaja sehemu za kihistoria kama ilivyo katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na kazi yetu kinadharia kwa kuwa imehakikiwa kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu ilhali sisi tutahakiki kazi yetu kwa kutumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa.

### 1.9 Msingi wa kinadharia

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Nadharia hii ilianzishwa na Karl Marx mwaka 1818-1863 na Fredrich Engles (1820-1895). Uhalisia wa kijamaa ni nadharia inayotumika kuzihakiki kazi zote za kifasihi zinazolenga kuisawiri jamii katika uhalisia wake na kueleza hatua za mabadiliko za jamii husika. Katika kuifafanua nadharia hii, Karl Marx ambaye ni mmoja wa waasisi, amejikita katika historia na miundo ya kijamii. Mtazamo wa waasisi wa nadharia hii umekuwa nguzo muhimu wakati wanajamii wamekuwa waking'ang'ana ili kuifanya hali yao ya maisha iwe bora zaidi. Mapambano wanayozungumzia wanauhalisia wa kijamaa ni

kati ya tabaka tawala (matajiri) na tabaka tawaliwa (maskini). Tabaka tawaliwa inahusishwa katika uzalishaji mali lakini faida ya uzalishaji huu inawaendea matajiri (tabaka tawala). Kwa sababu hii kunatokea mvutano katika jamii ambao unaweza kumalizwa tu, ikiwa mfumo wa uzalishaji mali utamilikiwa na wafanyakazi walio wengi katika jamii.

Kwa mujibu wa Senkoro (1987), uhalisia wa kijamaa huchukuliwa kuwa kiwango cha juu cha uhakiki wa uhalisia. Uhalisia huu huwa na nguzo kuu ambayo ni harakati za kitabaka. Harakati hizi huwa hazina chochote kilichofichwa na kwa hivyo mambo huonekana kwa uhalisia wake. Kulingana na Njogu na Wafula (2007), nadharia hii ya uhakiki humchukulia binadamu kama uti wa mgongo wa kiuhakiki na kuwepo kwa ulimwengu na maana ya ulimwengu huo.

Waasisi wa nadharia hii wamejinasibisha na mwelekea wa Kimaksi kuhusu kuwepo kwa ulimwengu na historia. Kama anavyoeleza Maxim Gorki ambaye ni mmojawapo wa waundaji wa nadharia hii, anadai kuwa mambo yote yanayopendeza ulimwenguni yameumbwa au kufafanuliwa na binadamu. Anafafanua kuwa maisha ni matendo. Anaeleza kuwa dhamira ya kuishi ni kuzalisha na kusambaza vipawa vinavyomsaidia mtu kupigana na kushinda dhidi ya adui yake. Anasema kuwa binadamu anafaa awe na afya nzuri ili aweze kuishi maisha mazuri na afurahie maarifa yake ya kuudhibiti ulimwengu anaoishi.

Wamitila (2003), naye anasema kuwa uhalisia wa kijamaa ni mwelekeo unaojaribu kusisitiza umuhimu wa kuwasilisha uhalisia unaotilia mkazo mkuu kwa maendeleo ya kihistoria yanayokiuka ubepari na kufikia usoshalisti. Ili kazi ya fasihi iweze kuhakikiwa kwa kuongozwa na nadharia hii, kazi hiyo inapaswa kudhamiria kuwafikia wasomaji wa kawaida.

### 1.9.1 Mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa

Mihimili ya nadharia hii ni pamoja na kuonyesha uhalisia wake kwa uelekeo wa kijamaa. Uhalisia wa kijamaa hupinga kuwepo kwa matabaka ili njia za uzalishaji mali zimilikiwe kwa njia inayoleta usawa.

Nadharia ya uhalisi wa kijamaa huonyesha mfumo maalum wa kihistoria unaoonekana kuleta mvutano kati ya matabaka. Ili jamii iwe na mabadiliko au maendeleo lazima iwe na historia fulani ili itoke katika hatua moja kwenda nyingine. Mfano Karl Marx na Fredrick walisema "jamii zote ulimwenguni ilibidi zipitie katika hatua ya ukatili, umwinyi, ubwanyenye, ukabaila, ubepari na ujamaa ili ziweze kufikia usawa na hivyo kuleta maendeleo katika jamii."

Nadharia ya uhalisia wa kijamaa inasisitiza kuwa lengo la maisha kama matendo ni kuonyesha kukua kwa binadamu na kuonyesha anayeshinda katika mapambano ya nguvu za kiasili kwa njia ya ubunifu. Dhamira kuu ya nadharia ya uhalisi wa kijamaa ni kudokeza jinsi waandishi wanavyowasawiri wahusika tofauti katika jamii wanavyotakiwa kuwa watu walio na maarifa na wenye njia mbalimbali za kupambana na shida zinazowapata katika jamii, kama vile ukandamizaji, ufisadi, utabaka na umaskini ili waweze kuzishinda shida hizo. Asili ya mapambano hayo ni uzalishaji mali. Jambo hili hutokea wakati tabaka la chini linapojaribu kupambana na tabaka la juu ili kuweza kumiliki njia mbalimbali za kuzalisha mali kama vile mashamba na viwanda, hali ambayo hufanya tabaka la chini kufikia kiwango cha kupata usawa katika jamii.

Kazi za fasihi huonekana kama silaha ya kupinga ukatili, maonevu na ukandamizaji. Mara nyingi waandishi wengi wa kazi za fasihi hudhamiria kulikomboa na kulinasua tabaka la chini kutoka kwa maonevu, dhuluma na unyonyaji kwa nia ya kuleta usawa

katika tabaka hilo katika nyanja zote za kimaisha yaani: kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Nadharia ya uhalisi wa kiujamaa huwa na nia ya kujenga jamii mpya yenye ustawi na fanaka katika nyanja zote za maisha.

Uhalisia wa kijamaa hupigania jamii ili iachane na mambo yanayoirudisha jamii hiyo nyuma kwa kuwasawiri wahusika walijitolea kupigana ili walete mabadiliko katika sehemu zote za maisha ikiwemo kiuchumi, kifikira, kiutamaduni na kisiasa ili pawe na jamii yenye usawa na mafanikio.

Waanzilishi wa uhalisia wa kijamaa waliamini kuwa ikiwa wafanyakazi wa viwandani watachukua silaha na kutetea haki zao dhidi ya mwajiri wao, basi kutakuwa na mapinduzi ambayo yatazalisha jamii mpya isiyokuwa na matabaka.

Kazi nyingi za uhalisia wa kijamaa huamini kuwa suluhu dhidi ya ukandamizaji wa kitabaka ni tabaka la chini la wanyonge ambao ndio wenye nguvu ya kupigana na tabaka la juu kwa kutumia silaha ili kuzitetea haki zao. Baada ya kupigana na wanyonyaji, wanauhalisia wa kijamaa waliamini kwamba, kutatokea mapinduzi katika jamii inayohusika na hivyo kuzaliwa na kujengwa kwa jamii mpya isiyokuwa na ukandamizaji na matabaka na baadaye kuwa na jamii inayoishi kwa usawa.

Nadharia hii ya uhalisia wa kijamaa huonyesha kuwepo kwa matumaini kuhusu kizazi kipya cha binadamu. Hii inasawiri uwezekano wa kuwa na ushindi dhidi ya ukatili na dhuluma ya aina yeyote. Ni muhimu kutaja kuwa, lugha inayotumiwa katika uhalisia wa kijamaa inaendeleza malengo, matakwa na mapendekezo ya walio wengi katika jamii. Lugha hii huwa rahisi na inayoeleweka kwa urahisi na watu maskini.

Katika kipindi cha sasa kumeibuka Umarx mpya unaoshikilia kuwa kigezo cha utabaka na mabadiliko kisiwe ni cha kiuchumi pekee bali kuzingatiwe asasi nyingine *za jamii kama vile utamaduni* ambao unaweza kusababisha utabaka na baadaye kuleta

kuleta mapinduzi yatakayokuwa na athari kwa asasi za kiuchumi. (Williams 1981; Jameson 1991).

### 1.9.2 Matumizi ya mihimili ya uhalisia wa kijamaa

Kulingana na Wafula na Njogu (2007) wahusika wa kimaendeleo; ni wahusika wanaonuia kuipindua na kuibadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika wenye nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao. Kulingana na waandishi hawa uhalisia wa kijamaa unahusishwa na misimamo ifuatayo:

Hata ingawa nadharia hii huonyesha matukio kihistoria, wahusika hutenda matendo yao wakiwakilisha tabaka lao. Mhimili huu ni wa manufaa kwa utafiti wetu kwa kuwa utasaidia katika kufafanua masuala ya kihistoria yanayojitokeza katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Vilevile, utasaidia katika kumueleza msimulizi kama mhusika ambaye anawakilisha tabaka lake la wanyonge la jamii ya Wabajuni. Nadharia ya uhalisia wa kijamaa hushughulikia mahitaji ya maskini. Mhimili huu utasaidia katika kuangazia juhudi za jamii ya Wabajuni katika kujiokoa kutoka kwa ukandamizaji wa tabaka tawala.

Binadamu huonyeshwa kiuyakinifu wahusika ambao hutumiwa kama vipasa sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao. Nadharia hii husawiri matumaini ya kizazi kipya cha binadamu. Mhimili huu utasaidia katika kubaini matumaini ya kizazi kipya cha jamii ya Wabajuni na uwezekano wa juhudi za jamii hiyo kushinda dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wanaofanyiwa na tabaka tawala.

Nadharia hii inasisitiza matumizi ya lugha rahisi inayoendeleza na kupendekeza malengo ya walio wengi ambao ni wa tabaka la chini. Mhimili huu ni muhimu katika

kuchanganua matumizi ya lugha ya Kibajuni kama mojawapo ya lugha zilizotumiwa kuandika utenzi huu

## 1.10 Njia za utafiti

Kwa kiwango kikubwa utafiti wetu umefanyiwa maktabani na kwenye mtandao. Kwa ujumla tulikusanya data yetu kwa kuvisoma vitabu vinavyohusiana na *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Tulitafuta ushauri kutoka kwa wahadhiri wetu kuhusiana na suala hili. Tulisoma makala kuhusu *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* huu na kuuelewa kikamilifu kikamilifu. Tuliusoma utenzi huu kwa ujumla ili kuelewa ujumbe wa mwandishi. Tulisoma vitabu mbali mbali kuhusu fasihi ili kuelewa vipengele vya kimsingi vya fasihi. Vile vile, tulisoma vitabu vya historia ili kuelewa dhana ya historia kikamilifu. Baadaye, tulisoma utenzi huu kwa kina ili kubaini maudhui, dhamira na mandhari.

Tulisoma majarida na pia kutoka kwa mtandao mambo yote yaliyoandikwa kuhusu historia ya Wabajuni. Vilevile, tulisoma tasnifu mbalimbali ili kupata mwongozo wa kuhakiki na kuweka wazi suala la utafiti. Tuliteua data kuhusu maswali yetu ya utafiti . Tulichanganua data tuliyoipata kwa mujibu wa sura ya pili, tatu na nne ili kubainisha kama maswali ya utafiti yamejibiwa au la. Baadaye tulitathimini msingi wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu. Data tuliyoipata ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kimaandishi.

## 1.11 Hitimisho

Katika sura hii, tulishughulikia masuala ya kimsingi yanayohusiana na kazi yetu. Tulishughulikia utangulizi wa kijumla, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, nadharia ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na njia ambazo zilitumiwa kufanya utafiti wetu.

# SURA YA PILI

# MWINGILIANO KATI YA FASIHI NA HISTORIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tutachunguza vipengele vya historia na fasihi. Tutaangalia tofauti kati ya dhana hizi mbili. Vile vile tutaangalia mwingiliano wa dhana hizi mbili. Baadaye tutaangalia jinsi historia na fasihi zilivyoingiliana katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

## 2.2 Historia na fasihi

Tangu zama za kale kumekuwa na utamaduni wa kurekodi matukio na wakati kama yalivyotendeka. Hii ilianza kwa kuwepo kwa matumizi ya lugha kama chombo cha kuhifadhi lakini ikanawiri zaidi baada ya kufumbuliwa kwa mitambo ya uchapishaji. Hata hivyo, utamaduni wa kurekodi matukio umekuwepo hata kabla ya kubuniwa kwa mitambo ya uchapishaji kwani kumekuwa na maandishi machache yaliyokuwa yanaandikwa kwa karatasi na kwa ngozi za wanyama yaliyoonyesha ustawi wa watu wa zama wakinuia kuhifadhi ujumbe kwa vizazi vijavyo. Historia ni taaluma inayohusika na mambo yaliyorekodiwa na watu kutoka zamani walioaminika na watawala ili kurekodi ufanisi wa milki zao. Kwa kuwa maandishi hayo yalinuia kusifu uongozi, wakati mwingine yalikosa uhalisia kwa kuwa yaliegemea upande mmoja. Hata hivyo, hata yakichukua mwelekeo fulani, yaliaminika kuwa ya kweli na kama ujumbe ulioaminika kuhusu yaliyopita kuhusu jamii husika.

Kazi ya fasihi hueleza yaliyotendeka zamani na yanayotendeka katika jamii wakati wa kuandika kazi hiyo. Fasihi hutoa ufafanuzi wa mambo yote yaliyoandikwa kuhusu yaliyopita. Fasihi hutumia tanzu zake kama vile michezo ya kuigiza, ushairi, riwaya na nyingine kwa ubunifu wa mwandishi pasipo kuzingatia ukweli halisi. Kazi za

fasihi zisizokuwa za kubuni, wasifu na tawasifu zinachukuliwa kuwa za kifasihi hata ingawa huwa zimesheheni habari za ukweli halisi.

Fasihi na historia ni muhimu katika kueleza kuhusu ulimwengu unaotuzunguka na hasa kuhusu mambo yaliyopita. Hata ingawa historia inahusu kurekodi matukio kama yalivyotendeka, kazi ya fasihi inaweza kuwa na mambo yasiyokuwa ya kweli kutegemea ubunifu wa mwandishi. Fasihi pia hujumuisha tendi za nyakati za kabla ya historia katika nyakati tafauti za ustaarabu ilhali vita, kukua na kuanguka kwa ustaarabu, vipindi vya viongozi, mapinduzi na mengine, zote huchukuliwa kama historia.

Hata hivyo, fasihi na historia huingiliana kwa kiasi kikubwa. Historia, kwa upande mmoja inahusu maelezo ya matukio yaliyopita yanayoaminika kutokuwa na ubunifu. Kwa upande mwingine, fasihi inashughulikia chochote kilichoandikwa kwa ubunifu ili kipitishe ujumbe kwa binadamu. Fasihi pia hujumuisha kazi za kibunifu au kazi zilizoandikwa kuhusu matukio halisi au kazi za historia ya matukio yaliyopita.

Taaluma hizi zinaingiliana kwa kuwa maandishi yote ya kibinafsi/tawasifu au simulizi za kihistoria huchukuliwa kama fasihi na kazi nyingi za kibunifu na zisizo za ubunifu ni za kihistoria. Lengo kuu ya dhana hizi mbili ni kutoa mwelekeo wa mambo yajayo kutegemea matukio yaliyopita na matukio ya hali ya sasa. Kwa vyovyote vile taaluma hizi mbili huhusiana katika hali tofauti.

Ubunifu ni nguzo kuu ya kazi ya fasihi. Kuandika kazi ya fasihi, kutafakari mambo ya kihistoria kunahitaji ubunifu kwa kuwa inaaminika kuwa ubunifu husaidia kuwasilisha kwa urahisi mambo halisi na yasiyo halisi, mwandishi wa kazi ya historia anahitaji kuwa mbunifu kiasi cha kuwasilisha mambo kwa uwazi na kwa njia ya kuridhisha hadhira yake.

Mamilioni ya kazi nyingi za kihistoria zimeandikwa kwa njia isiyovutia, ya kidrama au ya kishairi. Hivyo basi, mwanahistoria mzuri anahitaji kuwa mbunifu katika uwasilishaji wake wa masuala ya kihistoria na usuli wa mambo ya kihistoria ili kunasa na kuburudisha hadhira yake pasipo kupoteza ujumbe wake.

## 2.3 Kutegemeana kwa fasihi na historia

Kwa mwalimu, Fasihi husaidia katika kumsaidia wanafunzi kufahamu yanayoendelea katika jamii kwa ujumla au sehemu fulani ya jamii wakati wa kuandikwa kwa kazi ya fasihi. Historia pia ni somo linalofunzwa kupitia hadithi. Kwa hivyo, kuweka wazi mambo ya kihistoria kwa kutumia hadithi iliyo na wahusika hai wanaohusiana na kutangamana huwa ni chombo muhimu cha kufunzia na kusoma katika mfumo wa elimu. Kwa ujumla, mwanafasihi huathirika na mambo ya kihistoria hata ingawa sio kwa njia ya moja kwa moja. Unaposoma kazi ya fasihi, utapata fununu ya jinsi mwandishi au jamii ya mwandishi ilivyoathiriwa na matukio ya kihistoria.

Unaposoma kazi ya fasihi iliyoandikwa katika mahali na kipindi fulani, itakuwa ni rahisi kufahamu jambo fulani kuhusu mambo yanayowasumbua watu watu wa jamii hiyo na mambo wanayoyathamini katika kipindi hicho cha kihistoria. Mwanafasihi huendelea kuonyesha historia naye Mwanahistoria huangalia mambo yanayomulikwa na Mwanafasihi.

Mfano mzuri ni kazi ya Shakespeare's *A Midsummer Night's Dream*. Katika mchezo huu wa kuigiza uliandikwa katika kipindi cha enzi za kati unaonyesha mahangaiko waliyokuwa nayo wasomi wakati huo. Inaonyesha vile watoto wa kike na wanawake walivyochukuliwa na jamii ya jumuiya ya Ulaya katika enzi ya kati. Shakespeare aliamini kuwa kulikuwa na haja ya kuweka wazi ukosefu wa usawa katika jumuiya ya Ulaya na hasa nchi ya Italia. Mfano mwingine ni katika kazi ya Wole Soyinka ya *A*

*play of Giant* (1984) inayomulika maangamizi ya kukatisha tamaa chini ya uongozi wa Mobutu Seseseko nchini ya Uganda.

Historia husaidia fasihi kwa kupeana nafasi ya kupanua mawanda ya fikira kuhusu kazi za fasihi yanayowekwa wazi kwa wanafunzi wa fasihi. Kwa mfano, utakuwa na uelewa wa kina wa kazi ya Shakespeare ya King Henry VIII ikiwa utasoma historia ya utafutaji wa ulimwengu mpya wa Watakatifu ama ukisoma kazi ya Christopher Marslow ya *The Passionate Shepherd To His Love* basi utakuwa na uelewa wazi wa changamoto za kijamii na utamaduni waliopitia watu wa enzi za kati. Vilevile, kazi za fasihi ya kihistoria husaidia wanafunzi wa historia kukuza ujuzi wa kufikiria na kutafakari masuala muhimu yanayoathiri jamii.

Kuna kazi za fasihi zinajulikana kama kazi za kihistoria. Hizi ni kazi ambazo zinashughulikia maudhui yanayoaminika kuwa ya kihistoria. Msomi halisi wa kazi za kihistoria anapevuka zaidi akisoma kazi za kihistoria za fasihi kwani huhitaji kufanya uchanganuzi wa kina akirejelea sababu, yaliyomo, muundo na uteuzi wa miundo ya sentensi na kiwango cha uteuzi wa maneno cha mwandishi. Uchanganuzi huu hueleza sana kuhusu anayezungumziwa na wakati wa kutolewa kuliko wakati uliokuwa umewekwa. Hii ni muhimu kwa kuwa itasaidia wanafunzi kuelewa mwono ulimwengu wa watu katika kipindi maalumu cha historia ambayo inaweza kuwa ni tofauti na yetu. Kwa hakika, fasihi huleta ufafanuzi wa mambo yaliyopita.

Aristotle wakati mmoja alisema kuwa historia hutueleza yaliyotendeka nayo fasihi hutueleza yaliyofaa kufanyika. Tofauti na maoni ya wengi, kulingana naye, ujumbe wa kifasihi ulitegemeka kuliko wa kihistoria labda kwa kuwa inaaminika kuwa historia ya 'kweli' na iliyo sahihi kabisa haipo. Kama kuna kitu kilichoongezwa, basi lazima kingine kiondolewe. Hivyo ndivyo ilivyo katika fasihi kwani tunajifunza

kuhusu jamii kupitia kazi za zinazoibuliwa na fasihi lakini maarifa tunayosoma mara nyingi hayaoani na hayajakamilika. Kama alivyosema Durant (2010) "yaliyopo ni yaliyopita yaliyogeuzwa kwa matumizi, na yaliyopita ni yaliyopo yaliyofunuliwa ili yaeleweke" yaliyopita ambayo ni yaliyopo yaliyofunuliwa ili yaeleweke ni historia, ilhali yaliyopo yakitajwa kuwa yaliyopita yaliyogeuzwa kwa matumizi itatajwa kuwa fasihi.(TY)

## 2.4 Kazi za kubuni za kihistoria

Kazi za kubuni za kihistoria ni aina ya hadithi au kazi ya fasihi inayoelezwa kwa njia tofauti tofauti. Hizi ni hadithi zilizo na misingi ya hali halisi ya maisha kutokana na matukio ya kihistoria na zilizojengwa katika mahali na wakati fulani wa kihistoria. Hata hivyo, wahusika wengine wanaweza kuwa hawajawahi kuishi pamoja na matendo yao yasiyokuwa na umuhimu wa kihistoria lakini yanaweza kujumuishwa ili yasimuliwe hadithi nzuri zaidi. Kwa mfano, kunaweza kukosa kuwa na matukio maalum yaliyorekodiwa, chakula kilicholiwa, mavazi yaliyovaliwa, njia walizopitia lakini mwandishi anaweza kuchopeka mambo yanayofikiriwa kuwa sahihi kihistoria kwa wakati huo.

Kazi nzuri ya kubuni ya kihistoria inaeleza hadithi inayolinganisha ujumbe sahihi na wa kweli pamoja na ubunifu ambayo inafaa kuwa na sifa zilizotajwa hapa chini. Pia, inaweza kupewa sifa kwa kurejelea muundo wa hadithi kwa kuangalia vipengele vifuatavyo: Wahusika, mandhari, maudhui, lugha, kiimbo na mwonoulimengu. Kazi za kubuni za kihistoria huwa na sifa zifuatazo: Kuna mchanganyiko wa matukio halisi na ya kubuni. Matukio muhimu ya kihistoria huwa sahihi kihistoria lakini matukio machache au wahusika wanaweza kuongezwa au kubadilishwa kidogo. Pili, wahusika wanahusika na migogoro au shida halisi au zinazoiga maisha kwa kipindi

hicho. Tatu, inatumia uandishi fafanuzi unaowachunguza wahusika na kuwafanya wavutie na rahisi kujinasibisha nao. Pia, mtiririko wa kazi kubuni za kihistoria huwa unazua hali ya taharuki kwa wasomaji na unaoeleweka na ulio na suluhu. Hata hivyo, kazi hizi huwa na mandhari halisi ya kihistoria inayoongoza mwelekeo wa hadithi. Muhimu zaidi ni kuwa inapatikana katika mahali halisi na wakati maalum wa kihistoria ambao msomaji angetaka kufahamu zaidi.

## 2.5 Vipengele fafanuzi vya hadithi ya kubuni ya kihistoria

### 2.5.1 Uhusika

Wahusika katika kazi hizi huwa ni watu wa kawaida waiowahi kuishi au wanadhaniwa kuwa waliishi katika kipindi cha kihistoria. Pia, wahusika kwa kawaida wanaathiriwa na kuumbwa na mazingira. Wahusika hawa pia, kwa kawaida hubadilika kwa sababu ya shida na ni lazima waweze kupata suluhu ya shida hizo. Msimulizi ni mhusika katika utenzi huu kwa kuwa anazungumza kama mmoja wa watu anaozungumzia. Kwa hivyo, ni mtu anayeaminika kuwa aliwahi kuishi miongoni mwa jamii ya Wabajuni.

### 2.5.2 Mandhari

Mandhari hujumuisha mahali maalum kihistoria na kijiografia na pia kipindi maalum cha kihistoria. Mandhari katika kazi za kubuni za kihistoria ni muhimu kwa kuwa huonyesha mahali halisi ambapo kazi hizi zimejengwa. Kazi hii, kama tulivyoeleza katika sura ya nn imerejelea mandhari nyingi halisi kama vile kutaja miji ya Kiunga, Mararani na mingine inayojulikana katika Pwani ya Afrika Mashariki.

### 2.5.3 Mtiririko

Mtiririko wa kazi hizi huwa ni wa kuvutia na unaoaminika. Hii ni kwa sababu kazi hizi zinashughulikia masuala yanayoaminika yalitendeka na wanajamii. Vilevile,

mtirirko huu unafaa uvutie ili wasomaji waweze kuendelea kusoma kazi hizi. Kazi hizi pia huwa na zinaeleza shida fulani inayotokana na wakati au mahali fulani kuhistoria ili wahusika watatutie. Pia, ni lazima msomaji ahisi kuwa hadithi ilitendeka au inakisiwa ilitendeka. Mtunzi ameeleza kisa chake kwa njia inayoeleweka vizuri akianzia na matukio anayoamini yalitokea kwanza kiwakati kama vile nchi kupata uhuru.

### 2.5.4 Maudhui

Maudhui hujikita katika muktadha wa kihistoria au miktadha inayokinzana katikati ya mielekeo tofauti ya kihistoria. Maudhui yana uhusiano na maisha, watu, miundo ya kijamii na kisiasa pamoja na matukio mazuri dhidi ya mabaya na maudhui ya kijumla yasiyofungamanishwa na wakati. Kama vile tumefafanua katika sura ya tatu, mambo mengi aliyozungumzia yana uhusiano na mambo ya kihistoria ya jamii inayoelezwa.

### 2.5.5 Mbinu za lugha

Mwandishi anatumia utabiri au mbinu rejeshi ili kuiweka hadhira yake katika hali ya taharuki. Pia, Matukio mengine yakiwemo matukio ya kihistoria, mazungumzo, mawazo ya kipindi fulani, usahihi wa kihistoria lakini sio habari zote zinaweza kuaminika na kuthibitika. Wahusika na mazungumzo yakibuniwa lazima yaingizwe katika mwelekeo wa kihistoria. Mazungumzo, kazi za kubuni, hisia zinatoka kwa ulimwengu halisi na zinafafanuliwa kwa usahihi kwa kipindi hicho na vipengele vingine vya hadithi. Hadithi inafaa itolewe kwa kuzingatia umuhimu wa kumuweka msomaji au msikilizaji katika mazingira ya kihistoria. Hata ingawa utafiti wetu haukushughulikia suala la mbinu za lugha, msomaji anapoanza kusoma utenzi huu anawekwa katika hali ya taharuki.

### 2.5.6 Hisia

Kazi za aina hii zinafaa kumfanya msomaji ahisi kwamba jambo hilo lilifanyika. Uhalisia wa jambo hilo unafaa kuonekana kwa kuwa watoto watauliza kama jambo hilo lilitendeka na watavunjika moyo wakipata halikutendeka. Vilevile, msomaji anafaa ahisi kuwa kuwa alipitia katika hali na mazingira hayo ya kihistoria ili aikubali kazi hiyo kama ya ukweli. Mwandishi anafaa awazie hisia za wanajamii na yaliyothaminiwa katika utamaduni wa wakati huo. Pia, anafaa ashirikishe ujumbe bila kubadilisha matukio yanayojulikana, mitazamo inayojumuisha na mionoulimwengu katika kipindi hicho cha kihistoria. Kwa kurejelea maoni ya Wilson (1984), Wabajuni wamekuwa na mtazamo kuwa wanaonewa na kuwa Serikali haiwatambui na hivyo kila Mbajuni ana huo mwelekeo na ndio maana mtunzi anaeleza kuhusu jamii yake kama mmoja wao ili kujinasibisha na jamii yake na atoe hisia zake kuhusu hali ya Wabajuni.

Katika *utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* kuna mambo mengi yanayoonyesha mwingiliano wa fasihi na historia, kwa kurejalea maswali yetu ya utafiti, tutaangalia baadhi ya masuala yanayoonyesha kuwa pana uhusiano wa karibu wa masuala ya kihistoria na utenzi huu. Vilevile, tutaangalia mambo ambayo yanaonyesha tofauti kati ya fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

## 2.6 Ujumbe wa ujumla katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*

*Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* unaelezea kuhusu vile jamii ya msimulizi ambaye ni Mbajuni ilivyovamiwa na watu wa kabila la Wasomali baada ya uhuru. Kichwa cha utenzi huu kinaashiria kuwa watu wa jamii hii wangetamani kurudi kwao nyumbani walipovurushwa na wavamizi. Mwandishi anaelezea vile

walivyohamia sehemu tafauti za upwa wa Afrika mashariki. Anafafanua masaibu wanayopitia watu wa jamii yake yakiwemo mashambulizi, vifo, kunyang'anywa mashamba yao, nyumba zao kuchomwa na mengine. Anaonyesha vile walipotaka kurudi katika sehemu walizoamini ni makazi yao wanakatazwa na hata kufungwa jela. Kwa sababu hii anajaribu kuelezea vile walivyokuwa wakiishi kabla ya uvamizi. Inabidi ataje majinayawahusika ili kuthibitisha anachosema. Isitoshe, anaeleza kuhusu ramani ya mji wa Kiunga ya zamani kama alivyoifahamu. Anasisitiza kuwa ni muhimu watu waangalie upya ramani hiyo ili kuwapa watu wa jamii yake haki yao kwa kuwarudishia ardhi yao.

**2.7 Historia ya Wabajuni**

Katika kuangalia historia ya Wabajuni, ni muhimu kutaja kuwa, Wabajuni walikuwa wanaishi kama jamii moja kabla ya kuja kwa wageni katika Pwani ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, baada ya kuja kwa wakoloni maisha yao yaliathirika pakubwa kwa sababu ya sera za kikoloni za nchi za kiutawala zilizoingia nchini Somalia na Kenya. Wakati nchi za Kenya na Somalia zilipopata uhuru, Wabajuni waliathirika zaidi kwa kuwa waliathiriwa na mipaka ya nchi huru iliyowagawanywa na kuwafanya kutoendesha shughuli zao za kijamii. Isitoshe, utawala wa Uingereza nchini Kenya ulikuja na mabadiliko mengi kuhusu maingiliano ya kijamii ikiwemo mifumo ya elimu, dini, kudunishwa kwa lugha za Kiafrika, mifumo tofauti ya kibiashara, teknolojia mpya miongoni mwa mengine.

Hata hivyo, Wabajuni waliendelea kujihisi kama jamii moja na wamekuwa katika harakati za kutetea maslahi yao pasipo kuzingatia kama ni Wabajuni wa kutoka nchi ya Somalia au katika nchi ya Kenya. Kisadfa, matatizo yanayowakabili Wabajuni nchini Kenya yana historia inayokaribiana na ya Wabajuni wa Somalia. Katika

kuieleza historia ya Wabajuni, utafiti wetu utakuwa ukirejelea masuala ya Wabajuni kwa kurejelea nchi hizi mbili.

Nurse (2010) anaeleza kuwa kwa zaidi ya karne tano Wabajuni waliishi kwa amaniwakifanya uvuvi, biashara na ukulima katika makazi yao ya Pwani ya Afrika masharìki kutoka Kismayu kaskazini mwa nchi ya Somalia hadi Kaskazini mwa kisiwa cha Pate nchini Kenya kwa sehemu ya upana urefu wa kilomita mia mbili hamsini. Walikuwa wachache na walikuwa na majirani wa Bara wa kabila la Wasomali waitwao Oromo ambao walikuwa wamejihami na walipenda vita. Makaazi yao yalikuwa visiwani huku wakiwa na mashamba ya kulima katika sehemu za bara zilizokuwa mkabala na visiwa hivyo. Wakati hali ilikuwa inazorota , Wabajuni waliokuwa wanaishi bara walikuwa wanaelekea katika sehemu za visiwani. Majirani zao hawakupenda kwenda visiwani kwani walikuwa wafugaji wa kuhamahama na hivyo hawakujihusisha na shughuli za uvuvi za visiwani.

Hata hivyo, katika nchi ya Somalia mambo yalibadilika mwaka wa 1991 baada ya kugatuliwa mamlakani kwa kiongozi Siad Barre, aliyekuwa kiongozi wa Somalia. Kilichofuata baada ya mwaka wa 1992 ilikuwa ni kipindi cha misukosuko. Mambo yalibadilika .Wasomali (Kabila la Hawiye, Darod / Maehan) walitoka sehemu za bara na kufurika visiwani huku wakiwahamisha Wabajuni kutoka makazi yao ambayo walikuwa wameishi kwa zaidi ya karne nne.

Wakimbizi wanaeleza visa vya kutisha ambapo walipokonywa mali yao, wakauawa, wanawake wakanajisiwa, vijana wakachapwa huku wengine wakiingizwa kwa kazi za sulubu katika kambi zilizokuwa mjini Kismayu. Nurse anasema kuwa katika hali hiyo kulikuwa na uwezekano kuwa Wabajuni wachache walirudi nchini Somalia na kuwa alikisia kuwa jamii na utamaduni wa Wabajuni ungeweza kusahaulika kwa kipindi

kilichofuata nchini Somalia. Hesabu rasmi ya kipekee kuhusu Wabajuni Wasomali ilifanywa na utawala wa kiitaiano mwaka wa 1926 na ulihusisha sehemu kuu za Wabajuni zikiwemo: Chovai (watu 434), Kismayu (334), Chula (301) na Koyama (172) kama ilivyoripotiwa na Grottanelli (1955). Kulingana naye, Wabajuni nchini Somalia hawakuzidi 2000.

Katika karne ya ishirini, familia zingine za Wabajuni ziliteremka nchini Kenya hata kabla ya misukosuko ya kisiasa ya miaka ya tisini nchini Somalia. Hata hivyo, baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Somalia, Wabajuni wengi walihamia katika kambi za Wakimbizi nchini Kenya walipokaa hadi mwaka wa 1997 waliporudishawa nchini Somalia.

Nurse anasema kuwa ilikuwa rahisi kuyaona na kuyataja makazi ya Wabajuni kama vile Kismayu: mamia ya nyumba, Fuma na visiwa vilivyo karibu, takriban kumi na mbili, Koyani: Vijiji vitatu na kiasi cha nyumba mia moja hamsini, Chovai: vijiji viwili na kiasi cha nyumba mia moja. Istambuli: majengo hamsini, Chula: vijiji vitatu miongoni mwa mengine.

Pia, kumetaja majengo yaliyoaminika kuwa misikiti yaliyopatikana katika vijiji tofauti tofauti. Nurse anadai kuwa kulingana na utafiti wake Wabajuni walikisiwa kuwa takriban elfu tatu kwa kila miji mikubwa ya Pwani ya Kaskazini Afrika Mashariki lakini anakubali kuwa sio rahisi kubainisha idadi kamili ya Wabajuni kabla ya misukosuko nchini Somalia kwa kuwa pia kulikuwa na miingiliano ya jamii baina ya makabila mengine nchini Somalia na Wabajuni.

Wilson (1992) katika utafiti wake kuhusu makazi ya Wabajuni anaeleza kuwa makazi makubwa yanayoaminika kukaliwa na Wabajuni ni kama vile: Ghedeni, Ngumi, Chula, Buri kavo, Kiamboni, Ishakani, Kiunga, Omwe, Shehe Jafari, Fadha na

Chundwa. Anasema kuwa kuna maeneo makubwa na madogo yaliyokaliwa na Wabajuni nchini Kenya kama ilivyokuwa nchini Somalia. Nurse (2010), historia ya Wabajuni inaweza kuelezwa kupitia kazi za fasihi za Kibajuni. Wabajuni wana kazi nzuri za kifasihi. Mojawapo ni *vave*. *Vave* ni aina ya ushairi au wimbo unaoimbwa wakati wa kuchoma misitu ili kujitayarisha kwa msimu wa kupanda na ziliimbwaa katika kipindi maalum cha mwaka. *Vave* ni mashairi marefu na moja inaweza ikaimbwa hata kwa zaidi ya saa kumi na mawili.

Ujumbe mkuu katika *vave* uhusu masuala ya kijamii na kisiasa na hupitishwa kwa usanii mkubwa maudhui yake yanaeleweka na yana umuhimu mkuu kwa Wabajuni pekee. Marejeleo ya kihistoria ya aina hii ya fasihi huwa yamewekwa katika lahaja na mara nyingi ujumbe sio wa moja kwa moja na kwa kawaida hakuna tarehe ya wakati yalipoandikwa. Visiwa vya Bajuni vinavyorejelewa katika kazi hii vimeonyeshwa katika ramani ya 1 ukurasa wa 81.

### 2.7.1 Mtazamo wa Wabajuni

Kwa sababu ya historia ya Wabajuni na mambo ambayo wamepitia, wamekuwa na mitazamo tofauti kuhusu hali yao na hasa uhusiano wao na jamii pana. Wabajuni wanaamini kuwa "hatuna serikali, tutasukumwa kila upande na serikali kuu na zingine, sisi ni wavuvi, lakini hii ni ardhi yetu." Kwa hakika, Wilson (1984) anasema wana ukweli fulani kwani wameishi katika upwa wa kusini miaka mingi kuliko Wasomali wa Kaskazini ambao wamevuka mipaka na kuingilia makazi yao.

Mieleko hii labda ilikita mizizi baada ya utawala wa Kibajuni kufifia katika karne za hivi karibuni hasa kwa sababu ya ukuaji wa kiutawala wa jamii ya watu wa sehemu za Bara ya Pwani kwanza, na baadaye uvamizi wa kabila la Wasomali kutoka kaskazini. Grottanelli (1955) anadokeza kuwa Wabajuni hawahisi kuwa sehemu ya Taifa la

Somali na hata hawana neno mwafaka kurejelea nchi ya Somalia. Neno *iti ina* maana ya nchi ya Kibajuni lakini sio maana pana kama inavyojulikana katika lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa walianza kutumia neno hili kabla ya kuwepo kwa mifumo rasmi ya Kiserikali hii inaashiria mielekeo hasi kuhusu serikali kuu za nchi ya Kenya na nchi ya Somalia. Wabajuni wanahisi kuwa watu waliotengwa. Mwelekeo huu unaashiriwa hata katika matumizi ya lugha pale ambapo kwa karne nyingi, Wasomali waliishi Pwani na na hawakuingia visiwani ambapo wengi wa Wabajuni walizaliwa, kukua na kufa kwenye visiwa. Uko barani kulikuwa na makazi ya watu waliozungumza lugha ya Kisomali na kwenye visiwa kulizungumzwa Kibajuni pekee.

Ni watu wazima wachache waliozungumza lugha ya Kiswahili na kisomali kutokana na mwingiliano mna makabila haya katika shughuli za kiuchumi kama vile uvuvi na biashara. Watu wengi kutoka visiwani walikuwa wanafahamu lugha moja tu ya Kibajuni na zaidi ya hayo hawakujali kuzungumza lugha ya Kisomali na hawakujali kuwa hawakuifahamu na hata waliwakataza watoto wao kuzungumza lugha nyingine isipokuwa Kibajuni. Uhusiano kati ya Wabajuni na Wasomali ulikuwa mbaya kwa sababu ya matukio ya kihistoria. Nurse (1994) Baadaye kulipotokea misukosuko nchini Somalia, uhusiano na mwelekeo wa maonevu kwa Wabajuni ulizidi.

Katika makala ya '*Wabajuni hatujijui tutokako wala twendako*' Masuo (2011) anadai kuwa Wabajuni hawajijui. Anasema kuwa kuna hali tofauti kati vile Wabajuni walivyokuwa kabla ya nchi ya Kenya kupata uhuru, baada ya kupata uhuru na jinsi walivyo kwa wakati huu. Kulingana naye wilaya ambazo Wabajuni wanajulikana waliishi katika nchi ya Kenya ni Lamu, Malindi na Mombasa.

Kwake, asili ya Wabajuni ni wilaya ya Lamu. Anasema kuwa wilaya ya Lamu ni wilaya iliyokuwa imesitawi katika maendeleo kabla ya nchi ya Kenya kuopata uhuru.

Hii ni kwa sababu Wabajuni ni watu walio na juhudi nyingi sana katika kilimo, sanaa, usafiriri na uvuvi. Anashangaa ni kwa nini wakati huu wilaya ya Lamu ina umaskini mwingi. Anasema, watu wanafaa kujua historia yao. Kulingana naye, ufahamu wa historia ya Wabajuni unatokana na yale wanayoambiwa na wazee wao lakini inafaa kufanywe utafiti ili waweze kufahamu zaidi kuhusu historia yao. Wengi wa waandishi kuhusu jamii ya Wabajuni wamesisitiza haja ya kufanya utafiti zaidi kuhusu jamii hii. Kutofahamu historia kuna maana kuwa hakutakuwa na ufahamu wa kule wanakoelekea Wabajuni. Wanataka wafahamu utamaduni wao na majina yao kama vile makabila mengine wanavyofahamu. Masuo anasema kuwa kutoka zamani Wabajuni hawakuwa taifa moja lakini sehemu mbalimbali za Wabajuni zilikuwa na watawala tofauti waliokuwa wakishirikiana, kutambuana na kuheshimiana. Wabajuni walipatikana katika miji ya Pwani kuanzia mji wa Kismayu hadi visiwa vya Ngazija huko Komoro.

Wabajuni walipatikana katika miji hiyo hadi wa leo lakini wengine hawajifahamu. Anasema sababu kubwa ni kwa kuwa muungano wa Waislamu ulimalizwa na muungano wa Wamagharibi kupitia kwa Njia ya 'Tenga utawale'. Vilevile, wakaanzisha utawala wa kikoloni na kuzigawanya nchi na kuweka mipaka kwa kutumia kanuni walizotunga na wakaondoa sharia ya Mungu. Kabla ya uhuru wa nchi ya Kenya, Wabajuni waliishi kama taifa moja wakiongozwa kwa misingi ya dini ya Kiislamu. Kabla ya kuja kwa wakoloni, Wabajuni walipigana na watawala wa Unguja waliotaka kuwatawala. Anaeleza kisa ambapo walipokuwa katika mapambano viongozi wao walialikwa kwa karamu ya kusitisha vita na chakula chao kikatiwa sumu na hivyo kushindwa na maadui zao ambao baadaye waliwauza kwa wakoloni. Wakoloni nao wakawauza kwa vibaraka wao baada ya uhuru na hivyo wao hawako huru hata sasa.

Vilevile, anasema kwamba Wabajuni ni watu walio na utamaduni wa kuvutia na walistawi katika kilimo, ufugaji, uvuvi, ukataji makoko, uundaji wa mashua na mengine. Walikuwa na vijiji vingi vilivyoingiliana katika masuala ya kijamii kama vile ndoa na mengine. Lakini anashangaa kuwa watu wengi hata wana uhusiano wa damu lakini hata hawajijui. Anadai kuwa Wabajuni wana utamaduni wa kuvutia lakini katika jamii ya sasa wanachukuliwa kuwa watu duni. Katika wakati wa sasa Wabajuni wanajitambulisha kama wa nchi ya Kenya au wa nchi ya Somalia. Kitambo hali haikuwa vile lakini serikali za wakoloni walifanya vile. Baadaye serikali huru ya nchi ya Kenya ikawagawanya kama Wabajuni wa Bara na wa visiwani.

Hata hivyo, Wabajuni walijigawa kwa misingi ya miji ambapo wengine watajitambulisha kama wakutoka Kiunga au kutoka mji wa Chundwa au hata kutoka Kingitini. Mwandishi anasema kuwa mgawanyiko huu umesababisha Wabajuni kutojijua wala kujitambua. Kulingana na Gona (2012) wakati wa 2010 na 2011 kundi la wanaharakati la '*Mombasa Republican Council*' lilisisimua na kuchukua nafasi katika siasa za Pwani ya Kenya, waliweka wazi masuala kadhaa waliyoamini yalihitaji kuangaliwa wakidai uhuru wa Mwambao wa Pwani.

Masuala makuu yalikuwa misukosuko kuhusu umiliki wa ardhi katika mwambao wa Pwani, dhana kuwa umiliki wa mali na nafasi za kazi zilikuwa zimemilikiwa na watu kutoka Bara, imani kuwa eneo la Pwani halikuwa na miundo msingi ya kielimu iliyokamilika pamoja na dhana kuwa mapato kutoka katika Sekta ya Utalii yalitumika katika sehemu zingine ni baadhi ya mambo waliyodai wakereketwa wa '*The Mombasa Republican Council*. Walioendeleza harakati hizi walirejelea historia na walirejelea kipindi cha kati ya miaka ya 1950 hadi 1964.

Walirejelea masuala mawili: Kwanza hali ya maili kumi kutoka Pwani iliyojulikana kama '*Ten-Mile Strip*' huu ulikuwa ni mpaka wa mwambao na ambao haukuwa umewekwa kwenye ramani ipasavyo na ulitawaliwa na Sultan wa Zanzibari. Baadaye suala hili lilisuluhishwa na kukazuka lingine. Hili lilihusu Mkoa wa Pwani kwa jumla na ambao ulikuwa umetoka kwenye eneo la maili kumi na kuingia ndani kidogo Barani.

Kutoka mwaka wa 1962 hadi 1964 kulikuwa na mijadala ya kisiasa kuhusu iwapo mikoa ya nchi ya Kenya inafaa kuwa ya kimajimbo au itawaliwe na serikali kuu. Baadaye walikubaliana kuwa nchi huru ya Kenya itawaliwe na serikali kuu hata ingawa sehemu ya maili kumi kutoka Pwani haikuwa huru wakati huo lakini kufikia 1964, nchi ya Kenya ilikuwa na utawala wa serikali kuu katika sehemu zote nchini. Baada ya uhuru , kumekuwa na mikataba mingi kuhusu hali umiliki wa ardhi katika Pwani ya Kenya.

Kutokana na ripoti ya TJRC ya 2013 inasemekana kuwa serikali ya aliyekuwa Rais wa Kenya Mzee Jomo Kenyatta ilikubali sheria kuhusu umiliki wa ardhi zilizowafanya wakaazi wa sehemu mbalimbali za nchi ya Kenya kuwa maskwota. Sehemu ya Lamu kwa mfano, ilichukuliwa kuwa eneo ambapo ardhi ilikuwa imilikiwe na serikali na wenyeji wawe maskwota ilhali wao ndio walikuwa wamiliki halisi. Istoshe, wenyeji hawakuwa na hati miliki za mashamba jambo lililowafanya wavurushwe kwa nguvu kila wakati na vikosi vya usalama vikidai kuwa vinadumisha usalama. Ripoti hii inaeleza vile wakati fulani wasomali walivamia mji wa Kiunga na kumuua askari wa polisi. Kikosi cha polisi wa G.S.U pia kiliwadhulumu sana Wabajuni na kuharibu vijiji vyao vikiwemo Rasini na Mtanga na kuwafanya

watoroke. Baadaye waliporudi walipata kuwa ardhi yao ilikuwa imesajiliwa kwa watu wa Bara ambao hadi leo wanadai kumiliki ardhi hiyo.

Kwa wenyeji wa Kipini, Swahili, Giriama walidai kuwa waligundua kuwa watu wa Bara wakiwemo Wakamba na Wakikuyu na askari waliokuwa wamevamia makazi yao kwa sababu zisizoelezeka walikuwa wamegawa mashamba yao na wamechukua hati za kuyamiliki.

Ripoti ya TJRC ilisema kuwa kumekuwa na misukosuko kati ya jamii ya sehemu hiyo na labda jamii jirani, maafisa wa usalama wa serikali na kikundi cha uhalifu kutoka Somalia kiitwacho 'Shifta' kinapovuka mipaka kutoka Somalia kuiba au kufanya uhalifu wa aina wa aina yeyote. Ripoti hii ya TJRC ilieleza kuwa kila mara askari wa kulinda usalama walipotumwa katika eneo hilo kukabiliana kikundi cha 'Shifta', walikuwa wanawageukia wakaazi wa eneo hilo na kuwadhulumu, kuharibu mimea yao, kuharibu nyumba zao na kuwavurusha kutoka kwa makazi yao.

Kwa sababu hiyo wakaazi wamefurushwa kutoka vijiji kumi na mbili vikiwemo vya Shendeni, shakani na Vundeni. Makamishina wa tume hiyo walisema kuwa wengine walifukuzwa ili kupeana nafasi kwa watu kutoka Bara. Makamishena hao waliorodhesha sehemu za Kishakani, Kiunga, Funambai, Materoni, Ashwei, Materoni na Vibondeni kama sehemu zilizokuwa zimemilikiwa na Wabajuni kufikia Kenya kupata uhuru na ambavyo baadaye viliharibiwa na kuchukuliwa na watu kutoka Bara.

Kuhusu mradi wa kutengeneza bandari ya Lamu, ripoti hii ilisema kuwa watu wa Pwani walidai kuwa serikali ilifahamu kuhusu mradi huu kutoka mwaka wa 1965 na wanaamini ndio maana walileta watu wengi kutoka Bara ili wafaidi fidia kutoka kwa mradi huu. Ijapokuwa ripoti hii ililetwa bungeni, hakujawai kuwa na mjadala kuihusu. Baada ya uhuru, vijiji vya Kiunga, Kishakani, Funambai, Vibondeni, Ashwei na

Materoni vilivyokuwa makazi halisi ya Wabajuni, viliharibiwa . Wabajuni wenyeji wamefurushwa au idadi yao kuonekana kuwa chache kuliko makabila mengine yaliyohamia kwao na hivyo kuwafanya kuwa walio wachache katika makao yao halisi.

### 2.8 Masuala ya kihistoria katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*

Baada ya kuangalia historia ya Wabajuni kwa kina, kuna mambo kadhaa yanayoonyesha kuwa utenzi huu una masuala ya kihistoria:

#### 2.8.1 Mandhari

Katika baadhi ya beti, mwandishi anazungumzia kuhusu miji inayojulikana kihistoria kama vile mji wa Kiunga,Witu, Mararani, Mkunumbi na Bura miongoni mwa mengine. Hii inadhihirika katika ubeti wa 5, 6, 36, 39, 40, 41, 45 na 46:

> 5. Kisha taeleza kwetu walipata tabu watu
> Wajitie kwenye mwitu KIUNGA kuikimbia
>
> 6. Watu walihama mji Wengine wakenda kui
> Kwa Pwani ya mtungui Kisiwani kulekea
>
> 46. Mwanzo tawapa ramani ya Kiunga ya zamani
> Kwa rasini na kwa Pwani nanyi mpate elewa

Kiunga ni mji unaopatikana katika Pwani ya nchi ya Kenya karibu na mpaka wa nchi ya Kenya na nchi ya Somalia. Vilevile, mji wa Mararani unapatikana katika mpaka wa nchi ya Kenya na Somalia. Mji huu umetajwa katika ubeti wa 47:

> 47. Tutaanza kwa rasini ukiingia mjini
> Utokapo Mararani madirasa tatapia

Baadaye mtunzi anataja barabara iendayo Bura. Bura ni mji unaopatika katika kaunti ya Tana River na uko ukingoni mwa Mto Tana nchini Kenya. Mji huu umetajwa katika ubeti wa 48:

48. Kisha kuna barabara iendayo hadi Bura
Kabla watu kugura wakenda kujilimia

Isitoshe, mtunzi anaelezea kuhusu mji wa Mararani na mji wa Witu. Miji hii ni sehemu zinazojulikana kihistoria katika eneo la Pwani hasa karibu na mpaka wa nchi za Kenya na Somalia. Sehemu hizi zimetajwa katika beti za 37 na 38:

37. Witu nayo ilipigwa na watu wengi kushikwa
Na nyumba zao kusakwa na wengine kukimbia

38. Mkunumbi ilingiwa na mji wakaachiwa
Lakini hazikutiwa moto nyumba hata moja

Ramani ya sehemu ya pwani ya Afrika mashariki inayoonyesha mji wa Mararani na Mji wa Kiunga imeambatanishwa mwishoni mwa kazi hii katika ukurasa wa 83 na 84 mtawalia.

### 2.8.2 Matukio ya kihistoria

Mtunzi pia anarejelea tukio la kihistoria la mwaka wa 1963 ambapo nchi ya Kenya na Somalia zilipata uhuru. Pia, anataja watu waliowavamia ambao ni kabila la Wasomali na ambalo linajulikana katika eneo la Afrika mashariki. Hata hivyo, anataja miji iliyovamiwa kama tulivyoeleza katika sehemu tulizozipitia. Miji hiyo ni kama vile Kiunga, Mararani, Mkunumbi, Witu, Bura na miji mingineyo. Baadhi ya miji kama vile mji wa Kiunga imetajwa kihistoria ikivamiwa katika vipindi tofauti kama vile katika ilivyokuwa ikivamiwa na kikundi cha kihalifu cha '*Shifta*'. Vilevile, miji hii iliathiriwa na misukosuko iliyotokea nchini Somalia ambapo waakimbizi kutoka nchi ya Somalia waliingia katika miji mingi ya Pwani ya Afrika Mashariki baada ya kung'atuka mamlakani kwa aliyekuwa rais wa nchi ya Somalia Siad Barre. Misukosuko hii ni tukio la kihistoria ambalo linajulikana na jamii ya ulimwengu. Hii inaonyesha kuwa, anarejelea matukio halisi yanalojulikana na jamii nzima kwa ujumla. Haya yanadokezwa katika beti za 2 na 3:

2. Nataka kufahamisha Maneneo kuyafupisha
Nyaka nyingi zilokwisha Mambo yaliyotokea

3. Mwaka sitini na tatu Kupata uhuru wetu
Ilipigwa miji yetu Na wasomale horia

Hata ingawa mtunzi hajataja jamii ya Wabajuni katika sehemu yoyote ya *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara,* katika utangulizi amejitambulisha kama mbajuni halisi na ambaye anataka kueleza kuhusu mambo yaliyotukia. Kurejelea jamii ya Wabajuni ni suala la kihistoria kwa kuwa Wabajuni ni watu wanojulikana kama wakaazi wa eneo la Pwani ya nchi ya Kenya na Somalia.

Hata hivyo, mwandishi katika ujumbe wake anarejelea mambo ambayo yalitokea kwa jamii zinazoishi Pwani ya Kenya baada ya kupata uhuru. Kama tulivyoeleza katika kazi hii, kulikuwa na uvamizi kwa wenyeji wa mkoa wa Pwani na watu wa Bara, vikosi vya usalama na kikundi cha kiuhalifu kiitwacho '*Shifta*' kutoka nchi ya Somali.

Kisadfa pia, baada ya kiongozi wa nchi ya Somalia, Siad Barre kung'atuliwa mamlakani, kulitokea misukosuko ya kisiasa nchini Somalia. Watu kutoka Somalia Bara walikimbilia usalama wao katika visiwa viitwavyo ' Bajuni Islands' ambavyo vilikuwa ni makazi ya Wabajuni. Ilibidi Wabajuni kuhamishwa kwa lazima kutoka makazi yao na kukimbilia usalama katika miji mingine iliyokuwa karibu nao. Kufikia sasa, kuna matatizo mengi yanayokabili umiliki wa ardhi katika eneo la Pwani mwa nchi ya Kenya. Kuna makundi mengi ambayo yamezungumzia suala hilo likiwemo kundi lililopigwa marufuku la *Mombasa Republican Council.*

Katika kazi ya Nurse (2010), akimrejelea Wilson anaeleza kuhusu mtazamo wa Wabajuni na jinsi wanavyojichukulia wao wenyewe na uhusiano wao na jamii zinazowazunguka. Wanaamini kuwa wanaonewa na serikali haziwatambui. Jambo hili limedhihirika katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* kwa kuwa mtunzi

anaeleza vile jamii hii imedhulumiwa bila kutaja jamii zingine za pwani ambazo zimepitia katika hali kama yao. Kulingana na mtunzi, Wabajuni hawajatambuliwa kama jamii. Kwa kurejelea ripoti ya TJRC, ni dhahiri kuwa makabila mengine yanayoishi mkoani Pwani yalipitia katika hali sawa na Wabajuni lakini mtunzi katika utenzi anaeleza kuhusu jamii yake pekee. Hili, kwa maoni yetu ni athari ya mtazamo wa Wabajuni kuwa wamekuwa wakionewa. Hili, linaonekana katika

17. Pakitokea matata pakawa pana na vita
    Watu shida wakipata Sirikali Hutetea

20. Na hakuna alionena na waliweko Mabwana
    Ni ajabu kubwa sana haki kutotaradhia

Katika ripoti ya TJRC, kumetolewa maelezo ya vile watu wa jamii ya mkoa wa Pwani walivyovamiwa na askari kutoka serikali huru ya nchi ya Kenya. Pia, askari waliokuwa wakienda kudumisha amani baada ya mashambulizi ya kundi la '*Shifta*',walikuwa wanawavamia wenyeji na kuwahamisha kwa lazima wakidai kuwa hawakuwa na vyeti vya kumiliki ardhi. Baadaye, wakuu wa serikali walikuwa wanagawiwa ardhi hiyo na kupewa vyeti vya kumiliki ardhi hiyo. Katika, *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara,* mtunzi ameeleza vile askari walikuja kudumisha usalama na baadaye wakachoma nyumba zao. Pia, anataja Mabwana ambao hawakuwatetea hata wakati walikuwa wakidhulumiwa. Hili linaonyesha mwingiliano wa fasihi na historia.

10. Wakaletwa asikari sasa hali ya hatari
    Tukakatazwa safari kwa sababu tunalindwa

20. Na hakuna alionena na waliweko Mabwana
    Ni ajabu kubwa sana haki kutotaradhia.

Hata hivyo, sio kila sehemu ya utenzi huu ni imeonyesha masuala ya kihistoria. Lakini mtunzi anataja majina ya watu alioamini kwamba anafahamu makazi yao. Hata ingawa, majina haya hayajaoana na watu wanaojulikana katika jamii hii, lakini

yanafuata mtindo wa kazi ya utafiti ya Nurse (2010) aliyeeleza kuhusu uchache wa Wabajuni na kutaja majina ya wazee waliompa maelezo kuhusu jamii ya Wabajuni. Mtindo huu wa kutaja majina unatumiwa na mtunzi kuonyesha uhalisia wa kile anachozungumzia kama anavyoonyesha katika beti za 69 na 70 ambapo anataja majina wakazi wa mji wa Kiunga.

69. Nyumba ya Asha Nyekombo Mamiri na Banyekombo
Wazee Madi Nyakombo Na Umari na Swafia

70. Nyalali na Bavuwae na Mwanase ni mwanae
Na Muhamadi ndugue Ngomeni waloguria

**2.9 Hitimisho**

Katika sura hii, tumechanganua dhana za fasihi na historia. Tumebaini kuwa vipengele hivi viwili vinahusiana na kutegemeana. Tumegundua kuwa mwanafasihi hufaidi na kuathiriwana matukio ya kihistoria anapoandika kazi yake. Pia, fasihi baada ya kukaa kwa muda mrefu hubadilika na kuwa historia. Vilevile, tumeangalia sifa za kazi za kiubunifu za fasihi ambazo husimulia hadithi kutoka kwa maisha halisi. Istoshe, tumebainisha ujumbe wa kijumla wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ili kuweka wazi masuala yanayozungumziwa ya kihistoria yaliyo katika utenzi huu. Baadaye tumeeleza historia ya Wabajuni na mitazamo yao ili kubaini kama kuna vipengele vya historia hii katika utenzi. Mwisho tumehakiki kama kuna masuala ya kihistoria katika *Utenzi wa Nchuu Cwapo Yapo Tini Mwa Irara.*

# SURA YA TATU

# MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA NCHUU CWAVO YAPO TINI MWA IRARA*

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii ya tatu, tutashughulikia maudhui kama yanavyojitokeza katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Mtunzi wa utenzi huu ameandika kama mmoja wa jamii anayoizungumzia. Hivyo basi, amejaribu kuyaeleza masuala yanayoathiri jamii yake kwa kina. Kwa kuwa ujumbe wa mwandishi mara nyingi hubainika kupitia kwa maudhui, tutayatalii mambo yote aliyoyaeleza mtunzi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Mengi ya mambo anayoyazungumzia yanatokana na uvamizi wa jamii yake na kabila la Wasomali horia katika kipindi kisichobainika baada ya uhuru. Hivyo basi, maudhui mengi yatakayojitokeza yana uhusiano wa moja kwa moja na athari za uvamizi huo. Hata hivyo, kabla ya kuyaeleza maudhui hayo, tutafafanua dhana ya maudhui.

## 3.2 Dhana ya maudhui

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza maudhui kama ujumbe wa kazi ya fasihi unaohusu kitu, wahusika, hali ya maisha na matukio ya kila siku ya maisha. Kwa kawaida maudhui ni sehemu ya ujumbe wa mwandishi. Vilevile, maudhui yanaelezwa kama fikra za mtunzi kwa kutegemea muktadha fulani. Wamitila (2008) naye, anasema kuwa maudhui ni dhana pana inayofaa kufafanuliwa kwa njia mbili. Kwanza, kuwa ni jumla ya mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Mambo haya yanatokana na vile mtunzi anavyoilea mada ambayo ni nguzo ya kazi yake. Hata hivyo, Wamitila anatumia maudhui kueleza kiwango cha maana cha kazi ya fasihi. Mbatiah (2010) anaeleza maudhui kama masuala ya kijumla yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi.

Maudhui kulingana na Mdee (2011), ni masuala yanayoonekana kwenye riwaya, hotuba, hadithi, tamthilia na masimulizi yoyote yale. Kwa maoni yetu, tukirejelea fafanuzi za wasomi tuliowanukuu, maudhui basi ni jumla ya mawazo, ujumbe mkuu na masuala yote yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Maudhui ni jumla ya mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Maudhui humsaidia mwandishi wa kazi ya fasihi kujenga dhamira yake. Maudhui hujumuisha uelewa wa vipengele vya dhamira, falsafa, msimamo na itikadi ya mwandishi wa kazi ya fasihi.

Maudhui hupatikana kutokana na matendo ya wahusika. Hata hivyo, ili kufanikisha ujumbe wake, mwandishi hutumia mbinu za sanaa ili kufanya kazi yake ivutie hadhira huku akipitisha ujumbe wake kwa ufasaha. Katika sura hii tutajadili maudhui kama yanavyojitokeza katika *Utenzi waNchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* . Kuna maudhui mengi yanayojitokeza katika *Utenzi waNchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara,* lakini katika kazi hii tutashughulikia maudhui mengi iwezekanavyo tukiamini yatafanikisha lengo mojawapo la tasnifu hii. Baadhi ya maudhui tutakayoshughulikia ni pamoja na: dini, ukoloni mamboleo, utabaka , ukandamizwaji, unyanyasaji, ukiukaji wa haki za kibinadamu, utengano, ukombozi na udugu miongoni mwa mengine.

### 3.2.1 Dini

Dini katika jamii yoyote ni imani walionao wanajamii kuhusu uwezo wa nguvu/ viumbe waliokiuka uwezo wa kawaida wa binadamu. Mtunzi amerejelea dini katika ubeti wa 1:

1. Naanza kwa jina lako Bwana Mungu peke yako
   Unipe uwezo wako Lengo langu kutimia

Mtunzi anaanza kwa kumtukuza Mungu kwa kusema ndiye pekee aliye na uwezo wa kumsaidia kutimiza lengo lake. Vilevile, katika ubeti wa 21, Mtunzi anataja misikiti iliyoachwa wakati wa uvamizi. Misikiti ni nyumba za kuswali kwa waumini wa dini ya Kiislamu. Kuachwa kwa misikiti kunaashiria heshima wanayozipa sehemu za ibada wavamizi wa jamii ya Wabajuni. Istoshe, katika ubeti 56, mshairi anasema kuwa Mungu ndiye muumbaji na hivyo aliwaumbia Boi na Khadija Joji Banyekombo na Maboji. Hii inaonyesha kuwa mtunzi anaamini kuwa Mungu peke yake ndiye aliye na uwezo wa kuumba. Pia, katika ubeti wa 78:

> 78. Kuna nyumba ya Rashidi nduguye Madi Abedi
> Ndugu hawa sina budi kwa mola kuwaombea

Katika ubeti huu mtunzi anasema ana wajibu wa kuwaombea Mola Rashidi na nduguye Madi Abedi kwa sababu anaamini katika uwezo alionao mola kuwalinda ndugu hao. Wanapoamua kurudi makwao mtunzi anasema wanafaa waanze msikitini na wamalizie Mkwajuni. Kwanza kutaja msikitini ina maana kuwa wao ni waumini wa dini ya Kiislamu. Pili, kuanza kwa msikiti ina maana kuwa wanaheshimu msikiti kama sehemu ya ibada.

> 83. Turudieni mjini tuanze msikitini
> Upande wa Mkwajuni tupate kumalizia

### 3.2.2 Ukoloni mamboleo

Ukoloni mamboleo ni njia ya kutawala iliyo na mitazamo pana. Mojawapo ya njia hii ni vile viongozi wa nchi tawala wanavyoendelea kuingilia masuala ya nchi huru hata baada ya nchi hizo kuwa huru. Mtazamo mwingine ni pale ambapo viongozi wa nchi huru wanaendelea kutumia mitindo ya utawala ya wakoloni kuwanyanyasa watu wa mataifa yao. Ukoloni mamboleo unajitokeza katika utenzi huu kupitia ubeti wa 1:

> 3. Mwaka sitini na tatu Kupata uhuru wetu
> Ilipigwa miji yetu Na wasomale horia

Ubeti huu unaeleza jinsi miji ya msimulizi ambaye ni mtunzi wa utenzi huu ilivyovamiwa na Wasomali horia. Uvamizi huu unatokea baada ya nchi kupata uhuru kuonyesha ni ukoloni mamboleo. Katika ubeti wa 8 na 9, mtunzi anaeleza vile walivyoteswa usiku na mchana hadi wakawa katika shida nyingi. Anaeleza vile walivyopigwa mara nyingi na watu waliovamia miji yao. Wakoloni ndio walioleta mfumo wa kuwapiga waafrika na kuwahamisha kutoka makazi yao. Huu ni ukoloni mamboleo kwa kuwa kupigwa huku kunatokea baada ya nchi yao kupata uhuru. Vilevile, katika ubeti wa 10:

> 10. Wakaletwa asikari sasa hali ya hatari
> Tukakatazwa safari kwa sababu tunalindwa

Askari wanaletwa ili kuwalinda raia lakini badala yake askari wanawazuia kutembea. Matumizi ya askari kuwadhulumu raia ni ukoloni mamboleo. Katika hali ya kawaida, askari wanafaa kuwalinda raia. Kuwazuia raia kutembea wanavyotaka katika nchi yao ni ukoloni mamboleo. Katika ubeti wa 16, mtunzi anashangaa ni kwa nini walinda usalama wanavunja nyumba zao. Katika hali ya kawaida katika nchi huru, askari wanafaa kulinda raia pamoja na mali ya raia, kwa hivyo askari kutumika katika kuharibu nyumba za raia ni ukoloni mamboleo. Serikali ya nchi huru, inawatumia askari katika kuendeleza utawala dhalimu kama walivyokuwa wakifanya wakoloni.

### 3.2.3 Dhuluma /Ukatili

Dhuluma au ukatili ni hali ya kuweka watu katika hali inayokatisha tamaa. Hali hii inaweza kuwa kupitia kwa uharibifu wa mali au kusababisha madhara katika maisha au afya ya waathiriwa kwa jumla. Ukatili umebainika katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Unaonekana wazi katika ubeti wa nne:

> 4. Walianza Ishakani waingie majumbani
> Na wengini madukani jamaa wakakimbia

Mtunzi anaeleza vile wavamizi walivyoingia nyumbani pamoja na sehemu zao za biashara hadi wakasababisha watu kukimbilia usalama wao. Kuharibia watu makazi yao na kuwaacha bila biashara za kujikimu ni unyanyasaji wa kiwango kikubwa. Katika ubeti wa 9:

9. Kisha tukapigwa tena tena na tena
Usiku mara mchana dhikini tukaingia

Mtunzi anaeleza vile walivyopigwa tena na tena usiku na mchana. Anasema waliingia katika shida nyingi. Hii inaleta hali ya kukatisha tamaa. Kuwapiga raia usiku na mchana ni ukatili wa hali ya juu. Pia, katika ubeti wa 14, Msimulizi anafafanua vile mji wao ulitiwa moto ili watu wasiweze kujificha kutokana na mashambulizi. Hii inaonyesha kuwa lengo la wavamizi lilikuwa ni kuhakikisha kuwa wamewashambulia bila msaada. Hii inaonyesha kuwa walikuwa na lengo la kuwaangamiza. Vitendo hivi vyote ni vya kikatili. Katika ubeti wa 57 na 58,Mhusika Madi Lali anapokuja anaambiwa kwao ni Ngomeni. Kitendo cha kikatili kuwakataza watu kukaa katika makao yao na kuwalazimisha kuwa wakimbizi. Baadaye wanamfunga jela . Kufunga watu jela wakirudi makwao ni ukatili wa hali ya juu. Vilevile, katika ubeti wa 86:

86. Nai ikimsikia nae katumikia
Ng'ombe hukatwa mikia huwa akiangalia

Wavamizi wanaonyesha ukatili kwa kuwakata ng'ombe mikia.wanasimamiwa kutekeleza kitendo hicho cha ukatili. Hata hivyo, ng'ombe ni sehemu ya mali wanayomiliki watu . Kuwakata ng'ombe wao mikia ni kuwadhoofisha kiuchumi ili wasiweze kuendelea na wasipate uwezo wa kiuchumi ambao unawawezesha kuweza kupinga udhalimu. Hili linaonyesha ukatili mwingi. Katika ubeti wa 59 - 61:

60. Wakawa waende zao huku Kiunga si kwao
Na vitambulisho vyao Kiunga viandikishwe

61. Twendeni kwenye ramani ya Ngomeni
Kamwe wao si wageni wala hawana hatia

Mtunzi anaeleza jinsi wahusika Abudi wa Saidi na Walali Muhamadi walikuja katika mji wa Kiunga wakiwa na nia ya kujiandikisha wawe wapiga kura. Baadaye wanaambiwa warudi kwao kwani kwao sio Kiunga. Upigaji kura ni haki ya raia na huwa inawasaidia kutafuta viongozi wanaoweza kuwanasua kutoka dhiki zinazowakabiii kama vile umaskini. Aidha, wanatakiwa kuandikisha vitambulisho vyao Kiunga ili wasirudi tena. Hii inaonyesha dhuluma kubwa kwani wananyimwa ardhi yao.

### 3.2.4 Ukiukaji wa haki za kibinadamu

Kila mwanadamu duniani ana haki ya kuishi, kuwa salama, kumiliki mali, kuabudu, kutembea na hata kusikilizwa. Katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* kuna mifano mingi inayodhihirisha ukiukaji wa haki za binadamu. Kwa mfano katika ubeti wa 3:

> 3. Mwaka sitini na tatu Kupata uhuru wetu
> Ilipigwa miji yetu Na wasomale horia

Mwandishi wa utenzi huu anaeleza jinsi miji yao ilivyovamiwa na Wasomali horia. Huu ni ukiukaji wa haki ya kumiliki mali, haki ya usalama na haki ya kuishi. Uvamizi huu pia unawanyima haki ya kufurahia uhuru waliopata kutoka kwa wakoloni. Pia, katika ubeti wa 11

> 11. Alotaka kusafiri sharti atoke kwa siri
> Kwa miguu si kwa gari msituni kujitia

Wananchi wamenyimwa haki ya kusafiri vile wanavyotaka. Ilibidi kila walivyotaka kusafiri watoke kwa siri ili wasikamatwe. Vilevile, hawakuruhusiwa kutumia vyombo vya usafiri bali ilibidi watembee kwa miguu. Huu ni ukiukaji wa haki ya kuwa huru kutembelea sehemu yoyote ya nchi. Kwa kurejelea ubeti wa 14, msimulizi anaeleza vile miji yao ilitiwa moto na wavamizi bila kujali kwamba walikuwa wamiliki wa

miji hiyo. Aidha, kuchomwa kwa mali yao kulikiuka haki ya kumiliki mali. Kuzuiwa wasijifiche kunakiuka haki ya usalama. Kwa kurejelea ubeti wa 20,

> 20. Na hakuna alionena na waliweko Mabwana
> Ni ajabu kubwa sana haki kutotaradhia

Mtunzi anashangaa ni kwa nini Mabwana hawakuongea chochote kuwatetea raia. Anadai kuwa ni jambo la kushangaza kuwa hao hawakuwatetea watu jinsi walivyopaswa kufanya na hivyo hawakuwatendea haki raia. Kwa kuangazia ubeti wa 24 - 26, msimulizi anasema kuwa kuna wahusika waliojaribu kuzuia nyumba zao zisiteketezwe. Anasema baadaye ilibidi nyumba hizo ziachwe. Kwa maoni yake huu ulikuwa ni ukiukaji wa haki na anawarai wasomaji waulizie ili kuthibitisha kama aliyokuwa akisema ni ya ukweli. Kuna ubaguzi wa jinsi nyumba zinavyochomwa. Mwandishi analalamika kuwa walikuwa wanaacha nyumba zingine walipokuwa wanachoma makazi yao. Anaona kuwa kuacha nyumba zingine ni ukiukaji wa haki.Mtunzi anaeleza vile ukiukaji wa haki umekita mizizi katika jamii. Hii inatokea pale ambapo wahusika Abudi wa Saidi na Walali Muhamadiwanapokuja kuchukua kura kwao. Hata hivyo,wanaambiwa kuwa Kiunga sio kwao. Hii inadhihirisha ukiukaji wa haki ya kumiliki mali.

### 3.2.5 Vifo/ Tanzia

Kuna mauaji mengi yanayotokea wakati jamii ya msimulizi inaposhambuliwa na wavamizi. Maudhui ya tanzia hutokea pale ambapo kumekuwa na hali nyingi za kukatisha tamaa na masikitiko na ambayo mara nyingi husababisha maafa au kifo. Pia, tanzia huwa habari kuhusu kifo. Kwenye ubeti wa 54:

> 54. Na kwa Bahero wa sizi Famau Mbwara Mahazi
> Bwaheri na Inyasizi na wote wamejifia

Msimulizi aneleza wahusika anowafahamu ambao tayari wamekufa. Vile anavyoeleza hali yao kuwa 'wamejifia' inaonyesha hali ya masikitiko iliyosababisha kifo cha

Bahero wa sizi Famau Mbwara Mahazi Bwaheri na Inyasizi. Hata hivyo, katika ubeti wa 75, mtunzi anamtaja mhusika Alii ambaye anaeleza kuwa nyumba yake ilikuwa mbali. Anaeleza vile alikufa katika nyumba yake. Hali ambapo watu wanafia katika nyumba zao inaonyesha hali ya masikitiko mengi inayosababisha kifo. Vilevile, katika ubeti wa 84:

> 84. Tima Kupi na Ridhai ni watu waliohai
> Mahamudhu hako hai marehemu mejifia

Msimulizi anaeleza kuhusu wahusika Tima Kupi na Ridhai ambao bado wako hai lakini anamtaja mhusika mmoja ambaye ni marehemu. Hii inaleta hali ya tanzia.

### 3.2.6 Uchumi na mali

Maudhui ya uchumi na mali yanashughulikia mambo ambayo msimulizi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* anayoyaonyesha kama njia za kuzalisha mali za jamii anayozungumzia. Mambo haya yanaweza kuwa ukulima, ufugaji, biashara, kufanya kazi ya malipo na mengineyo. Kwa kuangazia ubeti wa 48:

> 48. Kisha kuna barabara iendayo hadi Bura
> Kabla watu kugura wakenda kujilimia

Msimulizi anaeleza kuhusu mazingira ya Bura ambapo anasema watu walikuwa wakienda kulima kabla ya kugura. Katika ubeti huu,ukulima ni jambo ambalo watu wa jamii hii wanajivunia. Na ni njia ambayo huwasadia watu katika jamii hii kuwapatia pato la kujikimu. Hata hivyo, kwenye ubeti wa 55:

> 55. Mama Titi Mwanaezi niweleze waziwazi
> Kwake kwaliko na mbuzi maziwa tukinunua

Mtunzi anaeleza kuhusu mhusika Titi Mwanaezi alikuwa anamiliki mifugo kama mbuzi. Mbuzi hawa walimpa maziwa ambayo anawauzia wanajamii. Hii ni njia mojawapo ambayo jamii hii ilijipa riziki ya kila siku na kujiendeleza kimaisha. Hata hivyo, katika ubeti wa 72, msimulizi anamzungumzia mhusika Famau Wembe

ambaye anasema ana matunda ya maembe ambayo ni matamu. Kuwepo kwa matunda ya maembe kunaashiria ukulima wa mimea ya matunda. Hii ina maana kuwa jamii hii inajihusisha na kilimo cha matunda kama njia kujipatia pato. Vilevile, katika ubeti 94:

> 94. Tima Sizi nyumba yake Mzina rafiki yake
> Na Shomari duka lake zishikemene pamoja

Katika ubeti huu, mtunzi awataja wahusika Tima Sizi , Mzina na anataja Shomari ambaye ana duka.Duka ni nyumba ya kufanyia biashara.hii inaashiria kuwa wanajamii hawa wanfanya biashara ili ktimiza mahitaji ya kila siku. Hata hivyo, katika ubeti wa 82, mtunzi anazungumzia vile Mhusika Bwana Mahazi alikuwa akiokota nazi. Nazi hutoka kwa mti wa mnazi ambao ni mmea unaopandwa na kutunzwa. Hii inaonyesha kuwa kuna kilimocha minazi.Aidha,katikaubeti huo huo kuna ujenzi wa nyumba ya shekhe. Hii inabainisha njia nyingine ya kujipatia pato ambayo ni kazi ya ujenzi.

### 3.2.7 Udugu/Ushirikiano

Kila jamii huwa mahusiano ya kijamii. Jamii inayozungumziwa na msimulizi inaishi kwa ushirikiano na udugu. Walipovamiwa walijiona kama jamii iliyovamiwa sio mtu binafsi. Hata hivyo, katika juhudi zao za kujikomboa kutoka kwa wavamizi wao, msimulizi anonyesha jinsi walivyosaidiana kama ndugu kwa hali na mali. Vile vile, katika kazi yake, mwandishi anatuonyesha uhusiano wa kinasaba katika baadhi ya beti. Ushirikiano huu unadhihika katika ubeti wa 53:

> 53. Hamadi mtu mzima na Bahero na Fatima
> Mwana mimi na Fatuma hawa ni laini moja

Mtunzi anatueleza kuhusu mhusika Hamadi, Bahero, Fatima Mwana na Fatuma. Anaeleza kuwa wote hawa wanatoka katika ukoo mmoja.Uhusiano wa kiukoo ni jambo ambalo mtunzi amelitilia mkazo ili kusawiri muundo wa kijamii wa jamii

anayozungumzia. Katika ubeti wa 51, Msimulizi anawataja Fatima Fumo, nduguye Madi Fumo na Khadija na kueleza kuwa wao ni watu wa jamii moja. Jambo linaloonekana wazi ni kuwa wanawahusisha ndugu wa kike na kiume katika jamii kwa usawa. Jambo hili linaonyesha kwamba watu katika jamii hii waliishi kwa ushirikiano bila ubaguzi wa kijinsia na walifanya kazi pamoja kama ndugu. Baadaye katika ubeti wa 63:

> 63. Ya Mwenyekombo KhalidiBanti nduye Abudi
> Na Nyashee Muhamadi zao laini moja

Mtunzi anaeleza ukoo wa MwenyeKombo ambaye ni ndugu ya Abudi pamoja na Nyashee Muhamadi. Undugu huu ni jambo linaloenziwa na jamii anayozungumzia mtunzi kwa kuwa mara nyingi kila anapomtaja mhusika anataja ndugu zake. Vilevile, katika ubeti wa 98,

> 98. Mwanaheri Mbwaravae na Bakari ni kakae
> Bakari Fumo ni nduwe maneno kifunulia

Mtunzi anataja kuhusu wahusika Mwanaheri Mbwaravae na Bakari ambao anaonyesha uhusiano wao wa kindugu unaowafanya kujadiliana kuhusu mambo yanayoendelea katika jamii yao. Wahusika hawa wanazungumza kuhusu mambo yaliyokuwa yametendeka katika jamii yao na kuonyesha hali ilivyokuwa mbaya. Hii inaonyesha misingi thabiti ya kifamilia inayowafanya wanajamii kushirikiana kwa kila jambo.

### 3.2.8 Woga

Woga ni hali ya kuwa na wasiwasi kuhusu jambo fulani. Kuwa na woga humfanya mtu kuwa katika hali ya kukatisha tamaa. Baada ya uvamizi unaotokea katika makazi ya jamii unavyoelezwa na msimulizi, unawatia wanajamii woga wa hali ya juu, labda kwa kutokuwa na uwezo wa kupambana na wavamizi ambao wanaonekana kuwazidi nguvu. Hata hivyo, woga unaowapata wanajamii ni mkubwa kiasi cha kuwafanya

waangalie hata wakati mali yao inateketezwa na wasifanye chochote. Wanaangalia mali yao ikiteketezwa bila kupinga kwa kuwa wanaamini kuwa wanaweza kushambuliwa na hata kuuliwa. Hali hii inajitokeza katika ubeti wa 22:

> 22. Na watu walioweko wakawa kama hawako
> Wakashikwa na viteko moto wakiangalia

Msimulizi anasema kuwa wanajamii waliangalia kwa mshangao moto ukiteketeza mali yao. Vilevile, kwa sababu ya kuogopa, hawakufanya chochote ili kuzuia uteketezaji wa mali yao. Woga huu unawafanya kuwaacha wavamizi wateketeze mali yao pasipo hata kunusuru chochote. Vilevile, katika ubeti wa 34, anaeleza kuwa watu wameshikwa na woga kiasi cha kutoweza kutetea haki zao. Katika hali ya kawaida, watu hawa walihitaji kupinga dhuluma waliokuwa wakifanyiwa lakini badala yake walinyamaza na kuangalia mali yao ikiteketezwa. Hata ingawa wanazifahamu haki zao wameshindwa kuchukua hatua kwa kuwa wanaogopa dhuluma zaidi dhidi yao.

### 3.2.9 Utabaka

Utabaka ni hali ambapo jamii hugawika katika makundi mawili yanayotokana na umiliki wa mali. Utabaka husababishwa na misingi ya kisiasa inayosawiri mifumo ya uongozi uliopo. Utabaka ni hali inayojengeka katika jamii baada ya kipindi fulani cha ukuaji wa jamii hiyo. Mara nyingi tabaka la juu ambalo linamiliki mali huwa ni tabaka tawala na tabaka la chini huwa ni tabaka tawaliwa. Mtunzi ameiweka jamii katika makundi mawili. Ameonyesha tabaka tawala jinsi linavyowanyanyasa tabaka tawaliwa kama inavyodhihirika katika ubeti wa 10:

> 10. Wakaletwa asikari sasa hali ya hatari
> Tukakatazwa safari kwa sababu tunalindwa

Askari wanasimamia tabaka tawala na wanawazuia watu wa jamii ya msimulizi kutembea. Watu hawa wamefanywa maskini na uvamizi uliofanyiwa jamii yao na kuwafanya wakimbizi.

Pia, katika beti za 20 na 91:

> 20. Na hakuna alionena na waliweko Mabwana
> Ni ajabu kubwa sana haki kutotaradhia
>
> 91. Ufalme jambo bora si jambo la masikhara
> Wakicheza kwa bakora miguu chini yalia

Mtunzi ametaja kuwa mabwana walikuja katika eneo la wakazi lakini hawakufanya lolote kutetea haki za wanajamii. Kuwepo kwa mabwana na ufalme unaowakandamiza watu wake katika jamii yoyote kunadhihirisha hali ya utabaka.

### 3.2.10 Ujenzi wa jamii mpya

Baada ya uvamizi uliotokea katika jamii ya msimulizi, jamii inaanza harakati za kujikomboa. Utenzi mzima unadhamiria kuweka wazi masuala ya jamii hii ili kuweza kujikomboa. Hata hivyo, katika ubeti wa 40 na ubeti wa 90 harakati za kujenga jamii upya zinadhihirika.

> 40. Kupatikana amani waloweko kisiwani
> Wakashukia mjini kubuni Kiunga mpya
>
> 90. Wana Tiani Sulubu tushindane na aibu
> Wala msione tabu vyama kuvisimamia

Msimulizi anaeleza jinsi jamii ya Wabajuni walivyorudi mjini Kiunga ili kuanza kuijenga upya. Hata ingawa juhudi hizo hazifanikiwi kikamilifu, hili linaashiria matumaini ya kuijenga jamii upya. Katika ubeti wa 90, mtunzi anahimiza umuhimu wa kuunda vyama ili washindane na aibu waliyokuwa wamepitia. Hii ni njia mojawapo ya kuanza ujenzi wa jamii mpya iliyo na ufanisi na inayowatambuliwa na jamii pana.

### 3.2.11 Ukandamizaji

Ukandamizaji ni hali ambapo watu wanawekwa katika hali ya kuhisi kwamba hali wanayopitia haina suluhu na kwa hivyo hakuna haja ya kujaribu kuitatua. Hali hii huwafanya wanaoendeleza dhuluma au ukuikaji wa haki nafasi ya kuendelea kufanya hivyo. Ukandamizaji husababisha hali ya kukosa matumaini kwa anayekandamizwa na mara nyingi kuwa katika hali ya kukubali hali yao mbaya. Katika ubeti wa 3:

> 3. Mwaka sitini na tatu Kupata uhuru wetu
> Ilipigwa miji yetu Na wasomale horia

Msimulizi anaeleza vile miji ya jamii anayozungumzia ilivyovamiwa na kabila la Wasomali. Labda kwa kiwango fulani kufanya uvamizi bila kichocheo chochote ni ukandamizaji. Pili, wanafanya uvamizi huu kwa kuwa wanafahamu kwamba jamii wanayoivamia haina nguvu ya kujilinda. Hali hii inasababisha ukandamizaji wa kiwango cha juu. Katika ubeti wa 34, Mtunzi anaeleza vile watu wanaogopa kujitetea kutokana na uvamizi huo. Mwandishi anaposema wanaona ni sawa wakati nyumba zao zinateketezwa inaonyesha kuwa wametiwa woga mpaka wakakubali hali yao ya kugandamizwa. Katika ubeti wa 33:

> 33. Basi watu wa Kiunga sitosema ni wajinga
> Walichelea kupinga amri ilotolewa

Mtunzi ansema kuwa watu wa mji wa Kiunga wanaonekana kuwa wajinga kwa kuwa wanakosa kupinga amri iliyotolewa. Hata hivyo, sababu ya kutopinga amri inatokana na woga waliotiwa na wavamizi walioharibu na kuchoma mali yao.Vilevile, fikra ya matokeo ya kupinga amri iliwafanya kutodhubutu kufanya hivyo. Jamii hii kutokubali kutetea miji yao inapovamiwa kunaonyesha wamekata tamaa na hii imesababishwa na ukandamizaji.

### 3.2.12 Utengano

Utengano ni hali ya kuwa au kuwekwa mbali kwa sababu maalumu. Utengano unaweza kuwa wa kifamilia, wa kisiasa, wa kitabaka na kadhalika. Utengano unasababishwa na hali tofauti tofauti kama vile vita, mizozo ya kijamii, hali ya kiuchumi, vifo na sababu nyinginezo. Katika utenzi huu kuna utengano wa kijamii unaosababishwa na uvamizi unaofanyiwa jamii ya msimulizi. Kwa sababu ya hali ya kivangaito inayotokea wakati jamii hii inapovamiwa, familia nyingi zinatengana kupitia vifo, kufungwa jela au hata kuhamishwa kwa lazima. Katika utenzi huu, katika ubeti wa 7:

7. Wakatupa mama ZAO Halima Lali na Jao
Kufuata wana wao Mwambore kuelekea

Mwandishi anaeleza kuhusu utengano wa kifamilia unaosababishwa na mtoto wa familia hii kupotea wakati wa kivangaito cha uvamizi. Hali hii inawafanya kutengana na mama yao Halima Lali ili kuelekea sehemu za Mwabore kuwasaka wana wao. Aidha, baada ya uvamizi uliotokea katika jamii ya mtunzi, kunatokea utengano wa kifamilia ambapo jamii nyingi zinatengana katika hali hiyo. Vilevile, kuna utengano unaosababishwa na vifo vya baadhi ya wanajamii kama inavyoelezwa katika ubeti 54, 75, na 85, mtunzi anataja majina ya waliokufa kama vile: Bahero wa sizi, Famau Mbwara Mahazi, Bwaheri na Inyasizi, Mjahidi wa Alii baba Moyo wa Alii na Mahamudhu.Vifo hivi vinasababisha utengano wa kifamilia, wa majirani na hata kutengana kwa wanajamii husika kwa jumla.Utengano wa hali yoyote ile husababisha jamii kurudi nyuma kiuchumi kwani utengano huu huharibu misingi ya uzalishaji mali pamoja na asasi za kijamii kama vile ndoa na hivyo kuifanya jamii iwe dhaifu.

### 3.2.13 Usaliti

Usaliti ni hali ambapo adui hupata siri za mtu kwa nia ya kuharibia mtu maisha hasa unapomwamini. Usaliti ni kuungana na adui ili kuweka maisha ya unayemwamini katika hatari. Usaliti ni hali ambapo matarajio ya watu katika jamii yanakosa kutimizwa kwa njia ya kinafiki. Maudhui ya usaliti yamejitokeza katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Katika ubeti wa 3:

> 3 Mwaka sitini na tatu Kupata uhuru wetu
> Ilipigwa miji yetu Na wasomale horia

Mwandishi anaeleza kuwa baada ya kupata uhuru, watu wa jamii ya msimulizi walivamiwa na Wasomali ambao walichukua mali yao. Watu katika hali ya kawaida wanatarajia kufurahia matunda ya uhuru. Walidhani kwa kuwa mkioloni alikuwa ameondoka sasa wangefanya shughuli zao bila matatizo. Lakini badala yake wanavamiwa na jambo hilo linawanyimwa nafasi ya kufurahia uhuru wao. Huu ni usaliti mkubwa kwa juhudi na matarajio yao kuhusu kupata uhuru. Katika ubeti wa 10,

> 10. Wakaletwa asikari sasa hali ya hatari
> Tukakatazwa safari kwa sababu tunalindwa
>
> 11. Alotaka kusafiri sharti atoke kwa siri
> Kwa miguu si kwa gari msituni kujitia

Mtunzi anaeleza vile askari waliletwa ili kulinda jamii ya msimulizi. Askari walitakiwa kuwalinda raia lakini badala yake wanaanza kuwawekea wanajamii masharti kama vile kuwakataza kusafiri wanavyotaka. Huu ni usaliti mkubwa kwa jamii ya msimulizi inayotarajiwa kulindwa na askari.Askari kama kikosi cha usalama cha nchi huru walitakiwa kuwaahakikishia wananchi usalama wao. Lakini kama anavyofafanua mtunzi katika ubeti wa 16, badala yake walivunja nyumba za wakazi. Mtunzi anaeleza kuwa walikuja walinda usalama ili kuhakikisha usalama lakini badala yake waliwavunjia nyumba zao. Kitendo cha walinda usalama kuwavunjia

wanajamii nyumba zao badala ya kuwalinda ni kuwasaliti. Vilevile, katika nchi huru, watu wakifanyiwa dhuluma za aina yoyote wanafaa kulipwa fidia na waliotekeleza hiyo dhuluma hiyo kushtakiwa mili haki itendeke. Katika ubeti wa 19 na 20,

19. Ni watu walionewa zao nyumba kuvunjiwa
Yafaa kushitakiwa ama kulipwa fidia

20. Na hakuna alionena na waliweko Mabwana
Ni ajabu kubwa sana haki kutotaradhia

Msimulizi anaeleza vile watu walitarajia kulipwa fidia kwa uharibifu waliofanyiwa . Vile vile walitarajia kutendewa haki baada ya wakubwa wao kuja. Msimulizi anashangaa vile wakubwa wao hawakuingilia suala hilo ili haki itendeke. Mabwana kutowatetea ni usaliti mkubwa kwani ni kama wanaungana na maadui wao kuwadhulumu.

### 3.2.14 Ukimbizi

Ukimbizi ni hali ambapo watu wanatoka katika makazi yao ili kukimbilia usalama wao. Uvamizi wa jamii yamsimulizi ulisababisha watu wa jamii hii kuwa wakimbizi katika sehemu za Pwani ya Afrika mashariki. Hali ya ukimbizi huwa ni hali iliyojaa matatizo kama vile: vifo, ukosefu wa chakula, magonjwa na hata wakati mwingine kukabiliana na majanga ya kimaumbile kama vile mafuriko na matatizo mengine. Msimulizi anasema kuwa watu walikimbilia usalama wao mistuni. Hii inaashiria kuwa walikumbana na matatizo mengi ikiwemo uwezekano wa kuvamiwa na wanyama wa porini. Ukimbizi unaonekana katika katika ubeti wa 5 na 6:

5. Kisha taeleza kwetu walipata tabu watu
Wajitie kwenye mwitu KIUNGA kuikimbia

6. Watu walihama mji Wengine wakenda kui
Kwa Pwani ya mtungui Kisiwani kulekea

Msimulizi anaeleza vile jamii ya msimulizi walivyopata matatizo baada ya kuvamiwa na majirani zao. Msimulizi anaeleza kuwa watu walitoka Kiunga kukimbilia usalama

wao kwenye msitu. Vilevile, walihama kutoka kwao wakaenda kuishi visiwani kama vile kisiwa cha Mtungui.

### 3.2.15 Nafasi ya mwanamke

Mtunzi ametumia majina mengi ya wanawake wa Pwani. Hii inaonyesha kuwa ameipa jinsia ya kike nafasi muhimu katika utenzi huu. Anaisawiri jamii kama isiyo na ubaguzi wa jinsia ya kike kwani anapowataja watu waliothirika na uvamizi anawahusisha wanawake kama ilivyo katika beti 51 hadi 53:

> 53. Hamadi mtu mzima na Bahero na Fatima
> Mwana mimi na Fatuma hawa ni laini moja
>
> 55. Mama Titi Mwanaezi niweleze waziwazi
> Kwake kwaliko na mbuzi maziwa tukinunua

Mtunzi anawataja wanawake kama vile Fatima, Fatuma Mwanaezi, Mama Titi na wengine. Hii inaonyesha jamii ya mtunzi inawathamini na kuwaheshimu wanawake na ndio maana inawataja katika shughuli zao za kawaida.Mtunzi anawasawiri wanawake kama wenye bidii na wanaofanya biashara kama anavyofanya Mama Titi Mwanaezi ambaye anafuga mbuzi wa maziwa na kuwauzia wanajamii mbuzi wa maziwa. Jambo hili linaonekana katika beti 55-56:

> 55. Mama Titi Mwanaezi niweleze waziwazi
> Kwake kwaliko na mbuzi maziwa tukinunua
>
> 56. Boi na Khadija Joji Banyekombo na Maboji
> Bwana Mungu Muumbaji na hawa katuumbia

### 3.3 Hitimisho

Sura hii imeeleza maana ya maudhui kwa ujumla. Vilevile, maudhui yanayojitokeza katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* yamefafanuliwa kwa kina.Tumebainisha kuwa maudhui mengi yanyojitokeza katika utenzi huu, yamemsaidia mtunzi katika kuendeleza dhamira yake. Baadhi ya maudhui kama vile: ukoloni mamboleo, ukiukaji wa haki, ukimbizi na mengine yametusaidia katika

kubaini iwapo maudhui kama kipengele cha kifasihi yanataja mambo yaliyotokea kihistoria katika jamii ya mtunzi.. Tumebaini kuwa mengi ya masuala yanayozungumziwa na mwandishi yana uhusiano wa moja kwa moja na historia ya jamii inayozungumziwa.

# SURA YA NNE

# MANDHARI NA DHAMIRA KATIKA UTENZI WA NCHUU *CWAVO YAPO TINI MWA IRARA*

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tuaangalia mandhari kama kipengee cha kimsingi katika kujenga ujumbe wa mwandishi. Mandhari ni muhimu katika kuelewa kazi ya fasihi kwa kuwa mazingira ya kijiografia na kihistoria yanayoonyeshwa na mwandishi huathiri matendo ya wahusika na kwa hivyo kuathiri ujumbe unaopitishwa. Kila jambo linalotendeka katika jamii hutendeka mahali fulani. Mara nyingi mwanafasihi huathiriwa na mambo yanayotendeka katika jamii yake. Hivyo basi, katika hali ya ubunifu atakuwa anasawiri matukio katika wakati na mahali fulani. Mandhari pia huonyesha miundo halisi ya mahusiano ya jamii inayozungumziwa na mwandishi. Vilevile, tutachunguza dhamira ya mwandishi wa kazi hii kwa kina. Hii ni kwa sababu dhana ya dhamira ni kiungo muhimu katika kujibu maswali yetu ya utafiti. Tutaeleza dhana ya dhamira na ya mandhari na baadaye kueleza vile zinavyoonekana katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

## 4.2 Mandhari na dhamira ya mwandishi

Kanyua (2011) Mandhari ni mazingira ya kufanyia kazi ya fasihi. Mandhari huashiria wakati na mahali tendo la fasihi hufanyika. Mandhari ni muhimu kwa mwanafasihi kwa kuwa humwelekezaa kufahamu mahali mahsusi na wakati maalum ambapo matendo ya fasihi hufanyika. Kwa hivyo, mandhari humsaidia mwanafasihi kumwonyesha msomaji mahali na wakati matukio yanayowasilishwa katika kazi ya fasihi yalitendeka.

Wamitila (2008) anasema kuwa mandhari yanajumuisha mazingira, mwanda na wakati wa kutendeka kwa tendo la fasihi. Kwa wataalamu hawa, mandhari hairejelei tu, sehemu ya kijiografia inayotajwa lakini hata wakati wa kutendeka kwa tukio hilo kama inavyoonyeshwa na wahusika. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza mandhari kama mahali maalum ambamo mtunzi amejenga ili wahusika wakae na waingiliane ili wazue matukio ya utendaji. Mbatiah (2001) naye anasema kuwa mandhari ni kipengele kinachorejelea sana utanzu wa drama. Kulingana naye, mandhari huzungumzia sura itokanayo na mapambo na vifaa kama vinavyopangwa kwenye jukwaa. Mazingira hayo yanaweza kuwa ya nyumbani, shambani, njiani au katika uwanja wa vita. Kwa maoni yetu, mandhari haipatikani tu katika utanzu wa drama, bali katika kazi yoyote ile ya fasihi.

Kwa kurejelea maoni ya Mbatiah, Wamitila (2004) anasema kuwa mandhari yanaweza kurejelea mazingira ya jukwaani ya kazi ya fasihi au pia wakati wa tukio lenyewe. Anafafanua kuwa kuna vipengele muhimu vya kuzingatia wakati wa kuchambua tamthilia kama vile: sifa za jukwaa, sehemu ya uigizaji na jinsi jukwaa lilivyoangaziwa. Kwa kurejelea maoni ya wataalamu hawa, mandhari ni sehemu ya utendaji anayoumba mtunzi wa kazi ya fasihi ambapo wahusika huingiliana na hutumia mapambo na vifaa vya utendaji ili kufanikisha utendaji wao. Ni muhimu kutaja kuwa mara nyingi matendo ya wahusika huambatanishwa na wakati maalum wa kutendeka kwa tukio hilo. Wamitila (2010), anasema kuna aina tofauti za mandhari: mandhari ya kijiografia, kihistoria, kidhanifu, kiishara, kidokezi na kiajinabi. Ili kufanikisha kazi yetu, tutaangalia mandhari ya kijiografia na ya kihistoria kwa kina na baadaye tutachunguza kuwepo kwa zile aina zingine za mandhari katika kazi yetu. Katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Kuna mandhari za kijiografia ambazo ni za sehemu halisi kama zinavyojulikana

katika Pwani ya Afrika Mashariki na pia mandhari za kibunifu. Katika uchambuzi wetu, tutaanza na mandhari za kijiografia na baadaye tuangalie mandhari za kihistoria.

### 4.3 Mandhari za Kijiografia

#### 4.3.1 Mandhari ya Kiunga

Mtunzi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara,* ameonyesha mambo mengi yanayotendeka ndani na nje ya Kiunga. Mji wa Kiunga ndio kitovu cha matukio mengi anayoyaeleza mtunzi. Katika ubeti wa 5 na 6:

> 5. Kisha taeleza kwetu walipata tabu watu
> Wajitie kwenye mwitu KIUNGA kuikimbia
>
> 6. Watu walihama mji Wengine wakenda kui
> Kwa Pwani ya Mtungui Kisiwani kulekea

Mwandishi anasema kwamba baada ya uvamizi, watu walikimbia kutoka Kiunga hadi msituni. Katika ubeti wa 6, mtunzi anaelezea kuwa watu wengine walikimbilia Pwani ya Mtungui. Umuhimu wa mandhari haya ni kumpa msomaji picha kamili ya mahangaiko waliyopitia wanajamii baada ya mji wa Kiunga kuvamiwa. Pia, katika beti za 35 na 36

> 35. Miji mingi ilipigwa na raia wakateswa
> Walobaki wakatekwa vikumoni wakatiwa
>
> 36. Kisha wakarudi kwao waingie nyumba zao
> Lakini Kiunga sivyo mambo walivyotokea

Mwandishi anasema kuwa kuna miji mingine ambayo ilivamiwa na watu wakapigwa na wakatoroka. Hata hivyo, katika baadhi ya miji, watu walirudi makwao na wakaingia katika nyumba zao. Lakini katika mji wa Kiunga watu hawakurudi . Hii ni kwa sababu nyumba zao zilikuwa zimeteketezwa na wavamizi. Hii inaonyesha dhuluma waliyofanyiwa wavamizi. Baada ya kueleza yaliyotokea katika miji tofauti tofauti ya Pwani ya Afrika mashariki, mtunzi anaturudisha tena Kiunga. Katika beti za 39, 40 na 41:

39. Turudi tena Kiunga nilosema si wajinga
Nyumba zao kuziwanga ambazo walivunjiwa

40. Kupatikana amani waloweko kisiwani
Wakashukia mjini kubuni Kiunga mpya

41. Sasa watake kujenga ya pili hiyo Kiunga
Hakuna mji ni minga ndio ilioenea

Mtunzi anawarudisha wasomaji katika mazingira ya mji wa Kiunga kwa vile ujumbe wake mkuu unajitokeza katika mji wa Kiunga. Katika ubeti wa 40, anasema baadaye kulipatikana amani mjini Kiunga. Wenyeji waliamua kurudi kutoka sehemu walizokuwa wamekimbilia. Wakaenda Kiunga ili waujenge mji huo upya. Mazingira haya yanamsaidia mwandishi kuleta matumaini ya ujenzi wa jamii mpya baada ya misukosuko ya kijamii. Pia, kuanzia ubeti wa 45 hadi 48:

45.Nataka niwaeleze maneno ni ya eneze
Miji yote ni tangaze kila mtu kusikia

46.Mwanzo tawapa ramani ya Kiunga ya zamani
Kwa rasini na kwaPwani nanyi mpate elewa

47.Tutaanza kwa rasini ukiingia mjini
Utokapo Mararani madirasa tatapia

48.Kisha kuna barabara iendayo hadi Bura
Kabla watu kugura wakenda kujilimia

Mtunzi anasema anataka kuwaelezea wasomaji kuhusu mazingira anamojengea kazi yake. Anasema kuwa atawaeleza kuhusu ramani ya Kiunga ya zamani. Anaeleza kuwa ili wasomaji waweze kumuelewa vizuri inabidi awaeleze vile Kiunga ilivyokuwa. Maelezo haya ni muhimu kwa wasomaji kwani wanatambua madhara ya uvamizi uliofanyiwa jamii ya msimulizi na vile ulivyoleta misukosuko ya kijamii na kuwatawanya wanajamii katika sehemu tofauti tofauti za Pwani ya Afrika Mashariki. Katika ubeti wa 56 hadi 60:

56. Boi na Khadija Joji Banyekombo na Maboji
Bwana Mungu Muumbaji na hawa katuumbia

57.Kablia njia kuu karibu na Memkuu
Madi Lali wa Mkuu Kiunga aliekuja

58.Alambiwa ni mgeni ati kwao ni Ngomeni
Nendeni kamfungeni huko jela atatiwa

59.Na Abudi wa Saidi na Walali Muhamadi
Walikuja maksudi kura kwao kuchukuwa

60.Wakawa waende zaohuku Kiunga si kwao
Na vitambulisho vyao Kiunga viandikishwe

Mwandishi anaeleza kuhusu wahusika waliokuja mjini Kiunga ili kujiandikisha kura. Mwandishi aneleza vile walivyoshikwa na kufungwa jela na wakaandikisha vitambulisho vyao ili wasirudi tena Kiunga. Kuweka wahusika hawa katika mji wa Kiunga ni njia ya mtunzi ya kuonyesha mateso waliyokuwa wakipitia wanajamii wakitaka kurudi katika makazi yao mjini Kiunga. Vilevile, kutaja matukio mengi katika mji huu wa Kiunga kunadhamiria kusisitiza kuwa mji huu ni makazi halisi ya Wabajuni.

### 4.3.2 Mandhari ya Witu

Mwandishi anatuonyesha mandhari ya mji wa Witu. Katika ubęti wa 37:

37. Witu nayo ilipigwa na watu wengi kushikwa
Na nyumba zao kusakwa na wengine kukimbia

Msimulizi anaeleza vile mji wa Witu ulivyopigwa na wavamizi na watu wakakamatwa huku nyumba zao zikisakwa na hivyo ikawabidi kukimbilia usalama wao. Kutaja mji huu kunaashiria kuwa sio mji wa Kiunga pekee uliovamiwa bali miji mingine miji ya pwani ya Afrika Mashariki.

### 4.3.3 Mandhari ya Mtungui

Msimulizi pia anaweka tukio la usimulizi wake katika mandhari ya Mtungui. Katika ubeti wa 6:

6. Watu walihama mji Wengine wakenda kui
Kwa Pwani ya mtungui Kisiwani kulekea

Mwandishi anaeleza kuwa, watu walihama kutoka mji wao baada ya uvamizi wakaenda Pwani ya Mtungui kisiwani. Anajaribu kueleza kuwa, watu walikuwa wakikimbilia usalama wao katika sehemu mbalimbali za ujirani wa mji wa Kiunga.

### 4.3.4 Mandhari ya Mkunumbi na Mararani

Katika ubeti wa 37 na 38, msimulizi anatuweka katika taswira ya ujumla kuhusu misukosuko inayotokea katika shemu wanamoishi watu wa jamii yake. Kwenye ubeti wa 37 na 38:

> 37. Witu nayo ilipigwa na watu wengi kushikwa
> Na nyumba zao kusakwa na wengine kukimbia
>
> 38. Mkunumbi ilingiwa na mji wakaachiwa
> Lakini hazikutiwa moto nyumba hata moja

Anaeleza kuwa miji mingine pia ilivamiwa kama vile mji wa Witu. Anasema watu walishikwa na nyumba zao zikasakwa. Hata hivyo, watu wengine walikimbilia usalama wao. Ili kuonyesha ubaguzi uliofanyika, anasema kuwa mji wa Mkunumbi pia ulivamiwa lakini nyumba zao haikuchomwa.

### 4.3.5 Mandhari ya Mkwajuni

Mwandishi ametaja sehemu iitwayo Mkwajuni katika kazi yake. Katika ubeti wa 76 na 83

> 76. Khadija Obo kwa chini na Nyabudi ubavuni
> Ukipita Mkwajuni huwa hukuangalia
>
> 83. Turudieni mjini tuanze msikitini
> Upande wa Mkwajuni tupate kumalizia

Msimulizi anaeleza kuhusu mazingira ya jamii anayozungumzia. Anataja majina ya watu ambao wanaishi katika katika sehemu ya Mkwajuni kama vile akina Khadija Obo na Nyabudi. Lengo lake ni kuonyesha kuwa aliwafahamu kama wakaazi halisi

wa sehemu ya Mkwajuni.Vile vile, anapoeleza kuhusu watu wa jamii yake, anasema kuwa atamalizia na sehemu iitwayo Mkwajuni.

### 4.3.6 Mandhari ya Ngomeni

Sehemu ya Ngomeni imetajwa na msimulizi anapoelezea masaibu ya watu wa jamii yake walipotaka kurudi kwao mjini Kiunga. Anasema kuwa walipotaka kujiandikisha kupiga kura waliambiwa warudi kwao Ngomeni kama inavyodhihirika katika ubeti wa 58:

> 58. Alambiwa ni mgeni ati kwao ni Ngomeni
> Nendeni kamfungeni huko jela atatiwa

Katika ubeti wa 70,

> 70. Nyalali na Bavuwae na Mwanase ni mwanae
> Na Muhamadi ndugue Ngomeni waloguria

Msimulizi anazungumzia mji wa Ngomeni kama mji ambao wanajamii kama akina Nyalali Buvuwae na mwanase waliguria. Hili linaashiria kuwa mji huu ulikuwa makazi ya jamii ya Wabajuni walipokimbilia usalama wao hasa baada ya uvamizi uliotokea katika maeneo yao kama mji wa Kiunga. Maelezo haya yanasaidia kusawiri matatizo waliyokuwa wanapitia watu wa jamii ya msimulizi baada ya misukosuko ya kikabila kutulia. Ramani ya mji wa Mararani imeambatanishwa mwishoni wa kazi hii katika ukurasa 66.

### 4.3.7 Mandhari ya Bura

Mtunzi ameeleza kuhusu ramani ya Bura ambao ni mji unaopatikana katika kaunti ya Tana River. Mandhari hii inarejelewa katika ubeti wa: 48

> 48. Kisha kuna barabara iendayo Bura
> Kabla watu kugura wakenda kujilimia

Ramani ya mji wa Bura kama unavyoonekana katika Pwani ya Afrika mashariki imeambatanishwa katika kazi hii katika ukurasa 82.

### 4.4 Mandhari za Kihistoria

Mandhari ya kihistoria kama vile tulivyotaja hapo awali ni kusawiri mazingira , mahali na wakati kwa kufungamanisha na kipindi maalum cha kihistoria. Mwandishi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* ametaja vipindi maalumu vya kihistoria kama vinavyojulikana katika hali halisi. Katika ubeti wa 2, 3 na 80:

2. Nataka kufahamisha Maneneo kuyafupisha
   Nyaka nyingi zilokwisha Mambo yaliyotokea

3. Mwaka sitini na tatu Kupata uhuru wetu
   Ilipigwa miji yetu Na wasomale horia

80. Kale nae alijenga kwa miti akaifunga
    Huko mjini Kiunga Somale waliingia

Msimulizi anasema anataka kuwaeleza wasomaji mambo yaliyotokeakwa kifupi. Anasema kuwa anayowaambiwa yalifanyika miaka mingi iliyopita. Kisha anasema kuwa nchi yao ilipata uhuru mwaka wa sitini na tatu. Baadaye anasema baada ya kupata uhuru ndio miji walimoishi watu wa jamii yake ilipovamiwa na watu wa kabila la Wasomali. Nchi kupata uhuru ni wakati unaojulikana wa kihistoria wa nchi hiyo. Katika ulimwengu halisi, watu wa jamii ya Wabajuni walivamiwa katika miaka ya tisini na kabila la Wasomali. Hivyo basi, mwandishi ameweka kazi yake katika mandhari ya kihistoria.

### 4.5 Dhamira katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*

Kila mwandishi huandika kazi yake ili kufikisha ujumbe fulani. Dhamira katika kazi ya fasihi ni wazo kuu linalomwongoza mwandishi kuandika kazi yake. Dhamira ni lengo la mwandishi ambalo anataka liwafikie wasomaji wa kazi yake. *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* umeandikwa kwa lugha ya Kibajuni na kufasiriwa kwa lugha ya Kiswahili sanifu. Hata ingawa kipengele cha lugha si mojawawapo ya malengo ya kazi hii, uteuzi wa lugha unalenga kuwafikia wasomaji wa lugha ya Kibajuni, kwanza labda akiwa na lengo la waweze kutathmini kama

mambo aliyosema yana umuhimu au uhalisia wowote kuhusiana na jamii ya Wabajuni na pia ili awafikie hadhira wengi iwezekanavyo.

Pili, kufasiri utenzi huu kwa lugha ya Kiswahili kunalenga kuifikia jamii pana ili kuwaeleza kuhusu historia ya jamii yake na labda kuwajulisha harakati za kujitambulisha na kujiokoa kutoka kwa dhuluma za kihistoria zilizofanyiwa jamii ya Wabajuni.

Mwandishi anaeleza historia ya jamii yake hasa baada ya uvamizi kutoka kwa makundi ya jamii ya Wasomali. Anaeleza vile miji mingi inayopatikana kwenye upande wa Pwani ya kaskazini mwa Afrika mashariki ilivyovamiwa. Anaitaja miji hiyo kama vile Kiunga, Witu, Mkwajuni na mingine. Isitoshe, anaeleza miji walikokimbilia kutafuta usalama ikiwemo miji ya Ngomeni, visiwani Mkunumbi na kadhalika. Lengo la kutaja miji hii ni kujaribu kuuelezea ulimwengu kuwa anayoyazungumzia yaliwahi kufanyika katika sehemu zinazojulikana na wasomaji.

Anwani ya kazi ya fasihi mara nyingi huwa imebeba ujumbe wa kijumla wa kazi hiyo. Anwani, *Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*, inamsaidia mwandishi kupitisha ujumbe wake. Marara ni aina ya mti unaopatikana katika Pwani ya Afrika Mashariki. Mwandishi anajaribu kueleza kuwa nyumbani ni nyumbani hata kama ni chini ya mti. Hii inaonyesha kuwa watu wa jamii ya msimulizi wangetamani kurudi kwao kwani kuwa nyumbani ni muhimu sana kwa mwanajamii yeyote. Hii inaonyesha kuwa mwandishi anataka watu wa jamii yake wapewe nafasi ya kurudi kwao nyumbani walikotolewa na Wasomali hata kama kunaonekana kubaya kwani watakuwa radhi kuwa kwao hata kama mazingira sio mazuri kuliko kuwa wakimbizi.

Hatimaye, mwandishi anataja majina ya watu anaoamini waliwahi kuishi katika jamii zao pamoja na kutaja uhusiano wao wa kifamilia na hata ujirani wao. Hili linaonyesha

kuwa mwandishi aliwafahamu watu anaowataja na analenga kutilia mkazo ujumbe wake kuhusu jamii ya Wabajuni na kuwashawishi wasomaji wamuunge mkono katika harakati za kuipigania jamii yake. Kwa kuwa mwandishi anahisi jamii yake ilipokonywa mali na vipande vyao vya ardhi, anawaeleza kuhusu ramani ya eneo la Kiunga. Kuwajulisha wasomaji kuhusu mji wa Kiunga kunaashiria kwamba analenga kuonyesha maeneo waliyokalia watu wa jamii yake kabla ya kuvamiwa na Wasomali.

Kwa ujumla, mwandishi analenga kuwajulisha wasomaji kuhusu historia ya jamii yake inayoonekana kufifia kwa sababu ya maonevu ya kihistoria akilenga kuishinikiza jamii ya ulimwengu iwatambue Wabajuni kama kabila na kutafuta haki kwa watu wa jamii yake. Mwandishi wa utenzi huu pia analenga kuwahimiza wanaofanya maamuzi kuhusu sera za umiliki wa ardhi kurejelea tena ramani ya mji wa Kiunga ili wachunguze mipaka ya Wabajuni kabla ya uvamizi waliofanyiwa.

Hata ingawa mwandishi anaitetea jamii ya Wabajuni, ni muhimu kueleza kuwa matatizo waliyopitia Wabajuni sio yao pekee bali yanawakilisha ukiukaji wa haki za kibinadamu katika eneo la Pwani na hivyo, utenzi huu ni kiwakilishi cha maonevu ya kihistoria ya wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki kwa ujumla. Kwa hivyo, mtunzi anatoa sauti kwa niaba ya makabila mengine yanayoishi Pwani ili serikali au makundi ya kutetea haki za jamii waweze kuwasaidia.

Jamii ya Wabajuni imekosa kutambulika kama jamii ya kipekee na badala yake wanajumuishwa katika kundi pana la jamii ya waswahili au wanachukuliwa kuwa wageni.Watoto waliozaliwa baada ya kuvunjwa kwa miundo ya kijamii ya Wabajuni na hasa baada ya miaka ya tisini hawana ufahamu maalum kuhusu utamaduni wa Wabajuni na wengine hawajajifunza lugha ya kibajuni na hivyo pana uwezekano wa kufifia kwa lugha hii katika siku za usoni. Mtunzi analenga kuchochea hamu ya

kufahamu utamaduni wa jamii yake na pia kuzuia lugha ya Kibajuni isiache kuzungumzwa baadaye kufa.

Kwa kumrejelea Nurse (2010), ikiwa hakutakuwa na maandishi kuhusu jamii hii, kuna uwezekano wa kusahaulika kwa utamaduni wa jamii hii kwani wazee wanaofahamu mambo mengi kuhusu jamii hii wanaendelea kufa. Hivyo, mtunzi analenga kuweka kumbukumbu ya kimaandishi kuhusu jamii yake ili isije ikasahaulika katika siku za usoni na hivyo kukosa kutendeweka haki kutokana na dhuluma za kihistoria.

### 4.6 Hitimisho

Katika sura hii, tulifafanua dhana ya dhamira na mandhari. Baadaye, tulijadili dhamira namandhari katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Tumebainisha kuwa mandhari katika utenzi huu ni halisi na ya kihistoria na hivyo, mandhari imechangia katika kujenga dhamira ya mwandishi. Hii ni kwa sababu, kuweka kazi hii katika mandhari halisi kunalenga kuupa ujumbe wake uzito ili ukubalike na wasomi. Pia, tumebainisha kuwa masuala ya kihistoria yamechangia katika kujenga dhamira ya mtunzi.

# SURA YA TANO

# MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tutaeleza kwa ujumla muhtasari wa utafiti wetu. Utafiti wetu ulinuia kuchunguza mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*Tulilenga kuangalia maudhui katika utenzi huu, mandhari katika utenzi huu na jinsi historia inavyofumbata dhamira yamwandishi. Utafiti wetu ulikuwa wa maktabani na tuliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Baada ya kuchunguza maudhui, mandhari na dhamira katika *Utenzi* wa *Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara,* tumebaini mambo mbali mbali yanayochangia kujibu swali letu la utafiti. Tumeonyesha muhtasari na maoni yetu na pia tumejibu maswali yetu ya utafiti kwa kina. Baadaye tumetoa mapendekezo yetu kuhusu tafiti zitakazofanywa na wasomi siku zijazo.

## 5.2 Matokeo ya utafiti kuhusiana na maswali ya utafiti

Katika kazi hii, tumeangalia mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Mrara.* Kazi hii iliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Ili kufikia lengo letu, tuliusoma utenzi huu kwa kina pamoja na kuangalia vipengele vya kimsingi vinavyoonekana katika kazi ya fasihi. Tumechungiza maudhui, mandhari na dhamira katika utenzi huu. Vilevile, tumeangalia maana ya historia na vipengele vinavyobainisha kazi ya kihistoria. Tumechunguza tofauti kati ya kazi za kihistoria na za fasihi na kuangazia uhusiano uliopo kati ya fasihi na historia kwa ujumla. Baadaye tumechunguza kwa kina masuala ya kihistoria yanayojitokeza katika utenzi huu pamoja na kuangalia sehemu zisizoonyesha sifa za kazi ya kihistoria.

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza inaonyesha masuala ya utangulizi wa tasnifu kama vile: utangulizi, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na nadharia inayoongoza kazi hii na njia za utafiti. Sura ya pili imeangazia mwingiliano wa fasihi na historia kwa ujumla na baadaye tumeonyesha jinsi mambo ya kihistoria kuhusu jamii yaWabajuni yalivyojitokeza katika *Utunzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Tumebaini kuwa, kihistoria jamii ya Wabajuni pamoja na jamii nyingine za Mkoa wa Pwani zimekuwa zikivamiwa na makundi kutoka nchi jirani ya Somalia na pia vikosi vya serikali kutoka nchi ya Kenya. Tumebaini kuwa mwandishi ameathiriwa kwa kiwango kikubwa na masuala waliyopitia watu wa jamii yake anapoandika utenzi huu. Hata hivyo, tumedokeza kuwa kuna masuala machache ya kazi yake tusiyoweza kuyaeleza kihistoria.

Katika sura ya tatu tumejadili maudhui kwa kina katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Tumeeleza dhana ya maudhui kewa kina na tukabaini kwamba maudhui mengi yaliyojitokeza yanaonyesha maonevu iliyofanyiwa jamii ya Wabajuni. Katika sura ya nne, tumejadili mchango wa mandhari katika utenzi huu. Tumebaini kuwa mwandishi ametumia mandhari za kihistoria na mandhari za kijiografia. Baadhi ya sehemu alizotaja katika utenzi huu ni sehemu halisi zinazopatikana katika Pwani ya Afrika Mashariki. Tumeeleza umuhimu wa mandhari haya katika kujenga dhamira ya mwandishi. Vilevile, tumeeleza dhamira ya mwandishi wa utenzi huu. Tumefafanua masuala tunayoyaona kama kichocheo cha mwandishi kuandika kazi hii. Katika sura ya tano tumeeleza muhtasari wa kazi yetu.Tumeonyesha matokeo ya utafiti kulingana na swali letu la utafiti na baadaye tumetoa hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

Kwa kurejelea maswali yetu ya utafiti, tulidhamiria kuhakiki mchango wa historia katika kufumbata dhamira ya mwandishi wa *UtenziNchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Katika utafiti wetu, imebainika wazi kuwa historia imeongoza dhamira ya mtunzi kwa kiwango kikubwa. Hata ingawa hii ni kazi ya kifasihi, kuna masuala mengi yaliyoelezwa katika utenzi huu ambayo ni ya kihistoria. Kama tulivyofafanua hapo juu, mtunzi amezungumzia suala la uvamizi wa watu wa jamii yake ya Wabajuni na Wasomali. Katika historia, uvamizi huu ulitokea mara nyingi katika sehemu ya Pwani kukiweko maeneo yanayokaliwa na Wabajuni katika Pwani ya Afrika Mashariki. Vilevile, ametaja kipindi ambacho uvamizi huu ulipotokea ambao ni mwaka wa 1963 baada ya nchi ya Kenya kujipatia uhuru. Katika hali halisi, nchi ya Kenya ilipata uhuru mwaka wa 1963 kwa hivyo hili ni suala la kihistoria.

Kwa upande mwingine, miji iliyotajwa katika utenzi huu inajulikana na iliwahi kupata uvamizi na wakaazi wa miji hiyo kutorokea sehemu zingine za Pwani ya Kenya. Miji hiyo ni kama vile: Witu, Mararani, Kiunga na miji mingine. Kutaja kwa miji hiyo kunarejelea sehemu zinazojulikana katika pwani ya Afrika Mashariki na hivyo mwandishi kuathiriwa na maeneo ya kihistoria nchini Kenya. Vilevile, ameeleza maingiliano ya kijamii na njia za kiuchumi za watu wa jamii yake ambazo zinarejelewa katika historia ya Wabajuni kama ilivyoelezwa awali. Njia za kiuchumi ni kama vile: ufugaji, biashara, uvuvi na nyingine.

Hata ingawa mwandishi ametaja sehemu za kihistoria kuna baadhi ya mambo ambayo ni ya ubunifu kama majina ya wahusika aliotaja katika kazi yake. Hata hivyo, majina haya yanaashiria jamii ya Uislamu ambayo ni dini inayotambulika hata katika jamii ya sasa. Kwa kutamatisha ni kuwa, historia imefumbata dhamira ya mwandishi kwa kiwango kikubwa.

Kwa kurejelea lengo letu la pili, tulilenga kuchanganua kwa kina maudhui kama kipengele cha fasihi katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Lengo hili lilikusudia kujibu swali la: Ni maudhui yepi yanayojitokeza katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara?* Kwa kurejelea suala la maudhui, tulieleza hapo awali kuwa maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Maudhui humwongoza msomaji kuelewa ujumbe wa mwandishi. Katika utenzi huu, tumeangazia maudhui mengi kama vile: ukoloni mamboleo ambapo tumeeleza kuwa baada nchi ya msimulizi kupata uhuru, viongozi wanaochukua mamlaka wanaanza kuwadhulumu watu wa jamii yao kwa kuwanyang'anya mashamba, kuwapiga na kuwaua. Katika hali hii kunatokea unyanyasaji, dhuluma, vifo, ukiukaji wa haki za kibinadamu na mengine. Utafiti wetu umechambua maudhui yanayopatikana katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* kwa ufanisi mkubwa. Maudhui haya yametusaidia katika kuelewa dhamira ya mwandishi wa utenzi huu ikiwemo jitihada za kuonyesha maovu iliyofanyiwa jamii ya Wabajuni kwa lengo la kutafuta haki

Lengo la tatu la utafiti lilikuwa ni kutathmini mchango wa mandhari katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Lengo hili lilidhamiria kujibu swali la: Mandhari yana umuhimu gani katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara ?* Katika utafiti wetu tulieleza dhana ya mandhari, tukabainisha aina za mandhari: za kijiografia na za kihistoria. Baada ya kuchunguza suala la mandhari, tulibaini kuwa mandhari yana umuhimu wa kujenga dhamira ya mwandishi. Hii ni kwa sababu, baada ya kuangalia mandhari ya kihistoria tulibaini kuwa ujumbe wa utenzi huu umeingilia katika kipindi maalumu cha historia ambacho ni baada ya nchi ya Kenya na Somalia kujipatia uhuru. Pia, kwa kurejelea mandhari za kijiografia, tumebaini kuwa, mwandishi amejihusisha na sehemu halisi kama vile miji ya Kiunga, Witu,

Mararani na mingine akiwa na lengo la kuonyesha jinsi anavyoelewa suala la uvamizi wa jamii yake.

### 5.3 Matatizo yaliyojitokeza kutokana na utafiti

Katika kazi yoyote ya utafiti, huwa kuna matatizo yanayomkabili mtafiti. Mojawapo ya changamoto tulizokumbana nazo ni ukosefu wa vitabu vya marejeleo hasa kuhusiana na historia ya jamii ya Wabajuni. Tuligundua kuwa nyingi ya kazi kuhusu jamii hii zimeandikwa na watafiti wachache. Vilevile, suala la kutathmini Wabajuni wa nchi ya Kenya na wa nchi ya Somalia lilikuwa changamoto kwetu. Hii ni kwa sababu kabla ya uhuru kama jamii nyingine za Kiafrika, hakukuwa na mipaka iliyoletwa na wakoloni. Ili kukabiliana na changamoto hizi tulisoma kwa kina kazi za watafiti walizoandika katika miaka tofauti kuhusu historia ya Wabajuni.Vilevile, tulisoma kuhusu historia ya Wabajuni nchini Kenya na nchini Somalia na kubainisha wazi masuala yaliyotufaa kwa utafiti wetu.

Aidha, tulipata changamoto katika kuuweka utenzi huu katika muktadha maalum wa kihistoria kwa kuwa mwaka wa uchapishaji wa utenzi huu haujabainishwa. Hata hivyo, changamoto hizi hazikuzuia kufanikiwa kwa utafiti wetu.

### 5.4 Hitimisho na mapendekezo ya utafiti zaidi

#### 5.4.1 Hitimisho

Katika kazi hii tulidhamiria kuangalia mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.* Katika utafiti wetu, tumebainisha kuwa kuna mwingiliano wa kiwango cha juu cha fasihi na historia. Hii ni kwa sababu masuala yaliyozungumziwa katika utenzi huu yana uhusiano wa moja kwa moja na mambo yaliyotokea katika jamii ya Pwani ya Afrika Mashariki kama tulivyoeleza hapo awali. Matokeo haya yametusaidia kujaza pengo la utafiti wetu kwa kuwa tumebaini kuwa

hata ingawa hii ni kazi ya fasihi, pana mwingiliano kati ya vipengele vya fasihi na masuala historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara.*

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Nadharia hii husawiri migogoro ya matabaka na juhudi za tabaka la wanyonge katika kujikomboa kutoka kwa tabaka tawala. Msimulizi amejitokeza kama kiwakilishi cha tabaka tawaliwa lililo katika jitihada za kujinasua kutoka kwa tabaka tawala lililowanyang'anya ardhi yao. Anatumia lugha ya Kibajuni ili iweze kueleweka kikamiklifu na wasomaji wake labda akiwa na nia ya kuwajumuisha katika harakati za utetezi wa jamii yake.

### 5.4.2 Mapendekezo ya utafiti zaidi

Baada ya kufanya kazi ya utafiti huu, tunapendekeza utafiti ufanywe katika utenzi huu kuhusu: Sifa za kifani zilizotumiwa na mshairi, uchanganuzi wa Ubaada Ukoloni katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. Mwingiliano wa kimaudhui wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara* na tenzi zingine za Kiswahili. Tafiti hizi zikifanywa zitasaidia katika kuelewa utenzi huu kwa kina.

## MAREJELEO


Abby, A. (2005). "Field Research Project on Minorities in Somalia". Unpublished report, Oxford House, London, October 2005

Abdulla, M. (1960). *Kisima cha Giningi.* London:Evans Bros

__________ (1960). *Mzimu wa Watu wa Kale.* Nairobi: East African Literature Bureau

__________ (1974). *Duniani Kuna Watu.* Nairobi: East African Publishing House

__________ (1975). *Siri ya Sifuri* Nairobi: East African Publishing House

Abubaker, M. (mh) *Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara (MTU NI KWAO Japo Chini Mwa Irara)*

Durant, W.(2010) *The Lessons of History.* Ariel, Simon & Schuster. Limited.

Gona, G.(2012) *Memory,Documents and Secessionist Politics in Coastal Kenya.* African Affairs, Volume 112, Issue 446. Oxford University Press

Ismaili, H. (1968). *The Medicine Man: Swifa ya Nguvumali.* Peter Lienhardt (Wahar.) Oxford. Kanyua, G. (2011). "Mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Natala*" Chuo Kikuu cha Nairobi. ( haijachapishwa).

Kapiyo, n.w (2011). *The Evolving World:A History and Government Course Book.* Oxford University Press East Africa

King'ei, K. na Amata, J. K. (2011). *Taaluma ya Ushairi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau

Masuo, M. (2011) Wabajuni hatujui tutokako wala twendako. Online http:// Bajuni .com

Mbatiah (2010): *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine: Mambo muhimu katika uhakiki wa Hadithi fupi.* Jomo Kenyatta Foundation.

Mdee n w (2011): *Kamusi ya karne ya 21*, Longhorn Publishers.

Mohammed, S. (1988) *Ushairi - Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam University Press Ltd.

Mukuthuria, M. (2007): "Upekee wa Swifa ya Nguvumali": Nordic Journal of African Studies 16(3):298-319

Mwirabua, A. K. (2009) "Ukoloni Mamboleo na Utandawazi katika Tamthilia Teule" Chuo Kikuu cha Kenyatta. ( Haijachapishwa)

Njogu na Chimera (1999): *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Nurse, D. (2010). *Bajuni Database*. Onlinehttp://www.ucs.mun.ca/~dnurse/bajuni_db.html

Onchwati, S. (2016) "Uhalisiajabu Kama Unavyojitokeza Katika Ukawafi wa Miiraji wa Utenzi wa Fumo Liyongo" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. ( Haijachapishwa).

Owallah, K. (2013) "Uhakiki wa Maudhui Teule Katika Utenzi wa Nabii Isa" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. ( Haijachapishwa)

Senkoro, F.E.M.K. (1987) *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre. Soyinka, W. (1984) *A Play of Giant.* London. Methuen ; First Edition

Walsh M. (2010). *Deep memoriesor symbolic statements? The Diba, Debuli and related traditions of the East African coast.* Paris: Karthala. 453- 476.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi Ya Fasihi:Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

___________(2010). *Kichocheo cha fasihi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Williams, R. (1981) *Marxism, Structuralism and Literary Analysis*. London


Wilson, T.H. (1984). *Sites and Settlement Patterns of Coastal Jubaland, Southern Somalia*, in T. Labahn (ed.). Proceedings of the 2nd International Congress of Somali Studies, Vol. II:

_________.( 1992). *Settlement patterns of the coast of southern Somalia and Kenya.* In Adam & Geshekter (eds). Proceedings of the First International Congress of Somali Studies

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

VIAMBATISHO

Ramani ya 1: Visiwa vya Bajuni





Imenukuliwa kutoka *google maps*

**Ramani ya 2: Mji wa Bura**




Imenukuliwa kutoka *google maps*

**Ramani ya 4: Mji wa Kiunga**




Imenukuliwa kutoka *google maps*

bado yuko katika hali ile ya kwanza na kuendelea kuchangia katika riwaya. Katika wakati wa kistari, binadamu anazaliwa, anakua kijana, anaoa au kuolewa, anazeeka halafu anakufa. Katika uhalisiajabu, mhusika anaweza kufa na kufufuka baadaye kama huyu Eks ama babu Mzuka katika *Babu Alipofufuka*. Pengine ndio maana mwandishi Danow (1995:94) anapendekeza kwamba, hatupaswi kufikiria wakati kama kitu kinachofululiza moja kwa moja.

Katika mandhari haya ya kiuhalisiajabu, tunaona mhusika kwa jina MKUU akimweleza Eks umuhimu wa matunda ambayo Mungu aliyaumba pale mwanzoni kabla ya kumuumba Eks kwa maana ya binadamu. (uk. 30-34). Mtunzi kwa kutumia mandhari ya kiuhalisiajabu amefanikiwa kumuelimisha hata msomaji kuhusu umuhimu wa kula matunda kama ilivyokuwa mapenzi ya Mungu alipoumba miti na matunda kabla ya kumuumba binadamu. Eks na mkewe Takosani wamezoea mapishi mazitomazito na kuyaita '*Real Typical English Breakfast*' ambayo ni mchanganyiko wa nyama, na mkate uliopakwa siagi kila upande na chupa ya mvinyo mkali chapa *martel.* Wanachukia kwa nyoyo zao maboga na matunda na kuyaona kama chakula cha sungura. Ukweli ni kuwa magonjwa mengi yanatokana na kutokula vizuri kwani, watu wanaiga hata vyakula wasivyojua asili na hata umuhimu wake.

Katika mandhari ya mjadala kati ya Eks na MKUU, Eks anapewa amri saba. Hizi ni kama zile amri kumi za Mungu katika Biblia ambazo ni sharti zitimizwe ingawa vigumu. Katika mandhari haya, matukio ya kiajabu yanafanyika. EKS

anaamrishwa kubadilisha jina lake na umri wake upunguzwe kutoka **70** hadi **23**. (uk. 36).

Baada ya MKUU kumpa EKS amri hizi, anafyatuka na kufifia angani na anaporudi anawatolea binadamu wote wa Kiafra ushauri. Tunapata hotuba ya kiajabu ambapo MKUU anajua matatizo ya ulimwengu wote ambapo tatizo la afya ni changamoto kila pahali na wanaoteseka zaidi ni Wakiafra kwani kuna uchache wa hospitali, madaktari na dawa. Mandhari haya yanadhihirisha nguvu za ajabu ambazo ni za kiungu na kuna marejeleo mengi ya biblia takatifu kama mahubiri. Mkuu anasema:

> Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu
> watajinyenyekeza watubu dhambi zao na kuniomba, mimi
> nitasikia kutoka POPOTE na kuiponya Kiafra (uk. 37).

Sikujua ni rafikiye mkubwa wa Mwalimu Baya na anafunga safari kwenda kumtafuta. Anapitia katika mtaa wa *Reciful Meadows* na katika mandhari haya, anagongana na msichana maridadi kwa jina Takosani binti Inatesh. Kama jina lake linavyoashiria, Sikujua anamtamani awe mchumba wake wa ndoa bila kujua mienendo yake. Wanajadiliana na ajabu ni kuwa, msichana huyu wa kiajabu ana mambo ya kiajabu. Takosani anaeleza kuwa, anapenda kutembelea makaburini na kuombea kaburi la mama yake, huku akilipigia magoti na kuweka sarafu juu ya kaburi kama salamu. Anaeleza kuwa anazungumza na mizimu ya mama yake na vile vile uraibu wake ni kuogelea baharini (uk. 41-43).

Sikujua anashtuka anavyosikia haya lakini kwa sababu ya urembo wa msichana huyu wa kiajabu, wanapanga vyumba nambari 15 na 18 kila mtu chumba chake bila woga. Takosani anaomba chumba nambari 18 kibadilishwe wachukue chumba nambari 13. Kulingana na imani na itikadi za baadhi ya jamii, kuna nambari ambazo zinahusishwa na imani fulani. Katika imani na itikadi za jamii nyingi za Ulaya, nambari 13 inahusishwa na nuksi au mikosi. Katika jamii hizi, ni vigumu kupata chumba au ghorofa ya 13. Vilevile katika mchezo wa kandanda, ni vigumu kupata mchezaji nambari 13 au gari nambari 13 katika mbio za magari maarufu kama *Safari Rally*. Vilevile, nambari **7** ina umuhimu sana katika biblia takatifu, ilhali nambari 666 inahusishwa na shetani. Katika mila na desturi za jamii ya Wakikuyu, watoto hawakuwa wakihesabiwa na ilikuwa hatia kutaja watoto wote wa mtu kwani, waliamini kufanya hivi kungeleta maafa. Kwa hivyo, uhalisiajabu wa nambari 13 katika riwaya hii, ni mfano wa jinsi mila na tamaduni nyingi duniani zinavyochukulia nambari.

Katika mandhari haya ya kiajabu ya chumba nambari 13, matukio ya kiajabu yanapatikana. Baada ya Sikujua na Takosani kufanya mahaba, Takosani anaondoka kupitia ukutani lakini Sikujua hafahamu. Takosani anamwahidi Sikujua utajiri jambo ambalo linamshangaza Sikujua na kumuuliza kama yeye ni jini. Takosani anakataa na kumhakikishia yeye si jini na hadithi za majini haziamini.

Takosani anamwamuru Sikujua afumbe macho na anapofumba macho anapoteza fahamu. Anapozinduka, anajikuta kwenye mandhari ya kiajabu eneo linalozungukwa na mipapindi mingi na mchanga tifutifu huku Takosani akimtaka wafunge ndoa. Kwake Sikujua haelewi kama anaota ndoto au ni hali halisi na anamwambia Takosani anaona kama yeye ni jini lakini anamjibu yeye ni binadamu halisi. Takosani anamfahamisha wako *Anneheg Xpress*, mtaa wa *Resiful Meadows* na kuwa nyumbani kwao ni chini ya bahari na duniani yeye hufika kwa shughuli maalum. Kadiri saa zinavyoendelea ndivyo Takosani anavyozidi kuwa mrembo. Katika mandhari haya ya ndotoni, wanajipata tena chumbani kwa Sikujua na Takosani anaomba awekewe wimbo wa *MWAKA WA SHETANI* lakini Sikujua anasema hana santuri inayoitwa hivyo. Takosani anazidadisi santuri zile na mara anaibuka na santuri iliyoandikwa kwa rangi nyekundu tena nzito *Inatesh aw akawm*. Hii ni santuri yenye michoro ya kiajabu na wimbo unapaswa kuanza mwisho kwenda mwanzo ili mtu apate maneno kinyumenyume. Wimbo huo wa *mwaka wa shetani* ukiwa unaendelea Sikujua anaona gari pale kando na haelewi kama anaota ama ni hali halisi na anajisemea kuwa hali halisi na ndoto ni kitu kimoja (uk. 48-52).

Kutokana na kisa hiki, tunaelewa wazi jinsi watu wengi wanavyojipata katika sakata za kutisha na hata kunaswa kwenye nguvu za giza bila kujua. Wanafunzi wengi hasa katika vyuo vikuu wanajipata tayari wamenaswa katika matumizi ya dawa za kulevya, imani za nguvu za giza na pia katika anasa bila kujua. Nyimbo nyingi zinazoimbwa kwenye magari, klabu na hata mtaani hazieleweki lakini

wasiojua hununua kanda hizi na kuzifurahia huku wakijitia mashakani. Matukio ya aina hii pia yamo katika sehemu za kuabudia na kufanyia kazi na hata kama wengi wanadai hayapo, ni mambo halisi yanayopatikana kila siku. Hivyo, mtunzi amejaribu kumulika visa vya aina hii na kutahadharisha wasomaji na jamii yote kwa jumla.

Mtunzi wa riwaya ya *Watu wa Gehenna* amefanikiwa kuvunja mipaka ya kijamii, kitaifa na hata kimataifa. Hii ni kwa sababu wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja. Katika kisa kimoja, mhusika Akilimali Van Krockoff kutoka Tasmania anajadiliana na Siyawezi kuhusu Kiafra. Krockoff amehitimu shahada ya uzamifu katika Chuo Kikuu cha *The End of the World* huko Magharibi mwa Tasmania. Majadiliano yenyewe ni kuhusu wanasiasa wa nchi za Kiafra na jinsi wanavyowapa wananchi matumaini wakati wa uchaguzi na mwishowe raia huishia mtoni kwani chama kinajengwa juu ya mtu mmoja ambaye anakuwa yeye ndiye chama, katiba, sera, kila kitu ndani ya yote, na rais akifa siasa zinayumbayumba kwani madaraka yote yamo mabegani mwake (uk. 54-55). Akieleza kuhusu siasa huko Tasmania, Krockoff anasimulia matukio ya kiajabu yanayotokea. Anasema kuwa siasa na ushirikina huandamana, na wanasiasa wanaamini mambo ya ndumba. Akifafanua, anaeleza kuwa ndumba ni jina pana linalojumuisha siri ya mizungu, mazingaombwe, nguvu na maombi na imani potofu, ufundi wa kuwasiliana na mizimu, dawa za kushirikiana na jicho la

pili. Anaeleza kuwa huko Tasmania, wanasiasa wanatumia nguvu za kichawi kupata ushindi katika uchaguzi (uk. 54-55).

Akichangia mjadala, Siyawezi anaeleza kuwa kwa kipindi kirefu Kisiwa cha Pate kimekuwa na mafundi mahiri wa sayansi ya mazingaombwe. Katika miaka ya 2070, Malkia Bi. Kirembwe, aliheshimika na kukimbiliwa na wengi ambao upigaji ramli sio tatizo. Katika simulizi za Pate, Krockoff anaeleza kuwa picha ya fundi wa ndumba ni ya aina ile inayoelezwa na William Shakespeare katika tamthilia yake ya *Macbeth*, kuwa ni viumbe waliochakaa, wenye muonekano wa mnyama mwitu na hawaonyeshi kama wakaaji wa dunia hii ingawa wako juu yake (uk. 56). Wabunge na mawaziri katika suti zao nzuri hukalishwa chini na fundi wa aina ya Karumanzira na kutakiwa kuruka damu ya mnyama aliyechinjiwa njia panda saa mbaya ya usiku au anashuhudia mbuzi akizikwa hai huku macho, masikio na midomo ya mnyama huyo imeshonwa kwa jina la kifo cha demokrasia, ili kuzika nguvu za wapinzani wao. Kisha usiku unaofuata unamwona akitema cheche bungeni kama mtu wa watu wakati ukweli ni mtu wa Gehenna (uk. 57).

Kisiwani Pate, tunaelezwa kuwa wanasiasa hutumia popobawa kuwadhulumu wapinzani wao. Katika vyombo vya usafiri, wanaosafiri kwa jahazi usiku kutoka Pate kwenda Lamu hawafungi macho kwa muda wao wa usafiri kwa kuhofia kujeruhiwa na popobawa, kwani inaaminika kuwa wanatumiwa na mwanasiasa mmoja kushambulia watu huku akieneza ugonjwa wa ukimwi kwa lengo la

kodhoofisha ngome ya Chama cha Mwananchi. Siyawezi anasema kuwa, imani ya ushirikina na maswala ya majini, mazimwi na wanga yana historia ndefu kisiwani Pate. Matukio ya kiajabu yanafanyika hivi kwamba mtu anaondolewa nyumbani kwake usiku bila mwenyewe kujua na kwenda kufanyishwa kazi ya kuvunja mawe usiku kucha au kuchimba kisima na kurudishwa alfajiri akiwa amechoka (uk.58-59). Hata hivyo, kuna baadhi ya jamii au watu wanaoamini mambo ya aina hii na ukweli ni kwamba, mtu huona anachotaka kuona na kusikia anachotaka kusikia na imani za majini au nguvu za giza humuathiri mwenye imani hizo.

Tunapatana na ndoto ya kiajabu ambapo Sikujua analiona gari wanamosafiria likizama baharini. Anajikuta akiwa yupo kwenye mji mzuri uliokuwa na ghorofa za kupendeza. Anajisemea kuwa, hiyo haikuwa ndoto, fikra wala hali halisi, bali yote matatu kwa pamoja (uk. 60).

Kutokana na usemi huu wa Sikujua, tunaona jinsi uhalisi na ndoto vinavyochanganyika hivi kwamba hakuna mipaka ya uhalisi na jinamizi katika uhalisiajabu. Mara Sikujua analetewa chakula na wapambe wa Takosani. Mara mandhari haya yanageuka mahakama na wapambe hawa wanamshtaki kuwa alipokuwa duniani alizoea kukata maelfu ya miti na aliposhutumiwa kutoendelea aliwalaani wale aliodai ni wapinzani wake. Pia anashtakiwa kuwa alipokuwa mamlakani kama mbunge, alishiriki katika vita vya kikabila na kusababisha umwagikaji wa damu wakati na baada ya uchaguzi. Vilevile, anashtakiwa kwa

kutumia nguvu za giza kupata cheo cha ubunge na kutumia dawa ya kuongeza nguvu za kiume zinazotokana na wachawi ili kumwezesha kufanya mapenzi kwa muda mrefu na mtu asiye mke wake. Alimhimiza mwanamke kutumia dawa ya kutengeneza ubikira bandia ili amfurahishe katika uzinzi na mwisho anashtakiwa kwa mazoea ya kusoma *The Codex Gigas.* Wapambe hawa wanamfunga kitandani na kumtandika bila huruma (uk. 60-62).

Mtunzi anatumia uhalisiajabu huu kumulika dunia na mambo yanayofanyika kisirisiri katika ulimwengu tunamoishi. Watu wengi hasa viongozi hushiriki maovu ya aina yote kisirisiri, lakini ukweli ni kwamba kuna wakati haya yote yatafichuka na adhabu kali kutolewa kwao.

Kuna mandhari ambapo mchezo wa kiajabu unachezwa na wahusika wakuu watatu ambao ni Sikujua, *The Codex Gigas* na Daktari Majini Tisa na unasemekana ni mchezo wa ukweli. Pazia jekundu linaanguka na linaporudishwa mara moja linafuatwa na pazia jeusi. Katika mandhari haya ya kiajabu, Sikujua ni mbunge aliyewaua watu 666 na kwa kufanya hivi anavishwa *Knight in the National Order of the Legion of Honour* na kuapa kwa *The Codex Gigas* mara 666 huku amefungua ukurasa 290. Usiku wa manane Sikujua anakutana na Daktari Majini Tisa huko mahame ya Ndagoni na wanaelekea bandari kubwa ya Wete ambayo ingaliwawezesha kusafirisha miili ya albino wakitumia merikebu za kuelekea Tanga zilizokuwa zimepakia mashehena ya saruji, mbao, karafuu, mapakacha ya *minazi* na ndizi. Kuna stoo kubwa ya kuhifadhi miili ya albino

Katika mandhari ya safarini, tukio la kiajabu na la kushtua linafanyika wakati Mwalimu Baya anampeleka msichana Mishi huko Chumbageni. Wakiendelea na safari yao kwa vokswageni ya Sikujua, treni inapiga honi inayoashiria kuwa iko karibu na hivyo Mwalimu Baya anaamua kuongeza mwendo ili apite kabla ya treni kufika kwani hakutaka kuzidi kuchelewa. Ghafla, gari lake linazimika katikati ya reli na anapojaribu kuwasha bila mafanikio, kwani betri ilikuwa imekwisha kawi; anaona taa ile kubwa mbele ya kichwa cha treni. Anamuamuru Mishi afungue mlango atoke nje lakini anaendelea kukaa kama amepigwa na bumbuazi na haonyeshi dalili ya kufahamu hatari inayowakabili. Anapojaribu kufungua mlango wake atoke, nao unakataa na kuhisi akili inamruka. Anapojaribu kuvunja vioo kwa ngumi navyo vinakataa amri na kumfanya ajilaumu kwa nini akampa lifti binti huyo mwenye mkosi (uk. 102-107).

Mara Mishi anamgeukia kwa haraka na kukunjua mikono yake kwa kasi ya mwanga na kumkumbatia Mwalimu Baya kabla tu treni haijagonga gari (uk. 107). Mishi anatamka jina *Shemhamforash!* Kwa haraka kwenye sikio la Mwalimu Baya na mara treni inaligonga gari lao kwa kishindo kama sauti ya radi ikipasua matlai lakini Mwalimu Baya hasikii sauti yoyote na kimya kinatanda akiwa mikononi mwa Mishi. Anapofumbua macho, anaona mabehewa ya treni yakipita ndani yao kama waliokuwa mizuka. Anaweza kuona viti, watu na kila kitu ndani ya treni huku treni ikiendelea kwa kasi. Baya haamini jinsi treni imepita ndani yao, bila kuwadhuru na anaendelea kushuhudia behewa la mwisho bado wakiwa katikati ya reli huku treni inaendelea mbele. Mishi anamwachilia na anarudi

kitini kujaribu kuwasha gari ambalo linawaka mara moja. Anaegesha gari pembeni aweze kuvuta pumzi alizokosa kwa muda ule wote. Anashtuka kwani hajui kama bado yu hai, ndotoni, au ndio ashakufa na roho yake bado inatangatanga (uk. 107-108).

Wakiwa garini, tukio lingine linatokea wakati Mishi anafungua mlango na kutoka kuelekea nyumbani. Mwalimu Baya anasikia mlio wa 'Ko Ko Ko' kama vile mtu aliyevaa viatu vya mchuchumio. Ana hakika moyoni mwake kuwa Mishi hakuwa amevaa viatu vya mchuchumio kwani alikuwaamevaa viatu vya wazi. Anapotazama miguu yake aone ni viatu gani hivyo vyenye kutoa mlio ungedhani mbao ikigonga sakafu, moyo unampasuka kwani hakuyaamini macho yake. Miguu ya Mishi imegeuka kwato za ng'ombe. Baya hataki ushahidi wa ziada. Lo! Mishi alikuwa jini (uk. 109-110). Tukio hili la kiajabu linatahadharisha watu dhidi ya kushirikiana na watu ambao hawawajui vyema. Wakati mwingine madereva wanawapa wasichana warembo au akina mama wajawazito lifti na baadaye wanawageuka kuwa majambazi na hivyo kuhatarisha maisha yao. Katika nadharia ya uhalisiajabu, mazingira ni sehemu muhimu sana na majitu na mazimwi hurejelewa na Mishi ni mfano wa wahusika wa kiajabu katika riwaya hii.

Mwalimu Baya anaendelea na safari huku akikanyaga mafuta kama aliyepagawa na mara anajihisi kibaridi kikimpuliza shingoni mwake na kudhania ameacha mojawapo ya madirisha ya gari wazi. Anapoangalia madirisha yamefungwa lakini

nywele zinamsimama na kujua kuna tatizo. Sauti ndogo ya kike inamshutua ungedhani ameuona mzimu wa Babu yake K katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ukimuita. Anapoangalia kiti cha nyuma, anamwona binti mdogo Saida akiwa amekaa upande ule ule wa gari kama alivyokuwa ameketi wakitoka Maweni. Ana uhakika alimshusha Saida Masiwani kwa mama yake na kuondoka yeye na Mishi tu. Kufumba na kufumbua, anaangalia nyuma na Saida ametoweka jinsi ile ile alivyoingia ndani ya gari. Mwalimu Baya anaanza kujua kuwa ameanza kurukwa na akili (uk. 113).

Katika mandhari ya kiajabu, Mishi na Mwalimu Baya wanajikuta kwenye ghorofa ndefu pembeni mwa bahari ya Hindi, huku wamekumbatiana kimapenzi kwenye kitanda cha sufi chenye mashuka ya hariri. Baada ya kufanya mapenzi, Baya anaendelea kumpapasa na kugundua binti huyo ana magamba mgongoni na mara mwili wake unapoteza joto na kuwa baridi kama barafu jambo ambalo linamshtua sana.

Anajisemea kuwa maajabu kama haya hayapaswi kuonekana na mwanadamu na baadaye kusimulia. Mishi anatamka tena neno *"Shemhamforash!"* na mara chumba kizima kinajazwa mwanga wenye rangi ya mbalamwezi angavu unaotoka ndani ya mwili wa binti huyo.Mwalimu Baya anamtazama na anajikuta roho inamtoka. Ajabu ni kwamba, Mishi ana jicho moja kwenye paji la uso wake, huku mwili wake ukiwa nusu toka juu hadi chini, titi moja, mkono mmoja, mguu

mmoja, nusu kila kitu. Anamsukuma kutoka kifuani mwake na kupiga ukelele kuomba msaada (uk. 117).

Anapozinduka usingizini, Mwalimu Baya anauhisi mwili wake wote ukipigwa na upepo mkali. Anapoangalia vizuri, anagundua hayumo chumbani mwake, wala ndani ya nyumba, wala ndani ya hoteli. Anajikuta juu ya mbuyu huku nguo zake zinaning'inia kwenye matawi yake (uk.117-118). Baada ya muda mfupi wasamaria wema wanamsaidia kuteremka na kumpa shuka ajisitiri. Anamueleza mzee mmoja kisa chote kutoka mwanzo hadi mwisho na mzee anamwambia kinachomsibu ni shetani wa mahaba kutoka Gehenna aliyewahi kuwa mke wa Shemhamforash! na kuwa hakuwa wa kwanza kupatwa na masaibu kama hayo. Anapomuuliza mzee huyo kama kuna dawa au madhara yaliyompata baada ya kukutana na mke wa Shemhamforash, mzee anamueleza kuwa kama amefanya mapenzi naye kwenye ndoto, ameshateuliwa na hivyo hatamuacha alale na mwanamke mwingine yeyote hadi kifo. Anamuelezea kuwa njia ya pekee ni kwenda Mabokweni kwa Sheikh Hamza Hamdani ili ampe dawa na kumuagua, Baya anauliza kama Sheikh huyo ni jini lakini mzee anamhakikishia si jini wala ndoto lakini ni mambo halisia. Baya anafunga safari ya kwenda kwa Sheikh anayempa masharti yanayomchukua karibu miaka saba kutimiza na mwishowe ile laana inavunjwa baada ya Mwalimu Baya kumtafuta mtu mgeni huko Chamada na kumtupia laana hiyo. Mwalimu Baya anaamka kutoka kitandani na kupata kuwa matukio haya yote yametendeka akilini mwake (uk. 112-120).

Kutokana na kisa hiki cha kiajabu, ni wazi kuwa matukio mengi hutokea akilini mwa binadamu kama ndoto anapolala ama wakati yu macho lakini yu mawazoni. Wakati mwingine matukio haya yanaonekana kama mazingaombwe lakini kuna wale wanaodai kuwa ni matukio ambayo yashawahi kutokea kwa binadamu halisi na ulimwengu halisi. Ni matukio ya kutisha na kuogofya na kawaida yanaathiri maisha ya binadamu hata mchana anapokumbuka yaliyotokea kwenye ndoto. Mtunzi anataka kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hutokea katika ulimwengu halisi.

Katika mandhari halisi ya Chuo Kikuu cha Kuhisika, wanafunzi wanagoma wakiungwa mkono na wazazi pamoja na baadhi ya walimu kwa kutoridhishwa na utawala wa kidhuluma. Wanabeba mabango huku mojawapo likiwa limeandikwa: *THE CORRUPT POLITICIAN'S CREED (uk. 122).* Mwanafunzi anayelibeba bango hili anapigwa risasi na polisi na kuumizwa vibaya. Wanafunzi wanasisitiza maktaba ichomwe wakidai inahifadhi nakala ya *The Codex Gigas* na makala ya *Hydropolitics around the Nile.* Maandamano ya aina hii pia yanafanyika katika nchi nyingi za Kiafra ambapo ujumbe kutoka kwa *Anonymous* katika nchi ya Mafirauni unaenezwa kupitia kwa *facebook* na *twitter.*

Maandamano ya aina hii yamewekea msingi nadharia ya uhalisiajabu kuwa, wakati na mahali vina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Kwa hivyo tunaona jambo linapotokea mahali fulani linajirudia kwa sura nyingine mahali pengine. Migomo ya wanafunzi wa shule za upili, vyuo na raia kutoka nchi tofauti za

Kiafra hutokea mara kwa mara na mwishowe tunaona nchi nyingi zinaanguka moja baada ya nyingine. Pia tunaona athari ya utandawazi kwa vile jumbe zinasambazwa haraka nchini na hata katika kiwango cha kimataifa.

Katika mandhari ya *Gehenna Systems Centre* (GMC), mhusika Yunasi anapofanya kazi huko Newyork, tunaona uhalisi na ndoto zinachanganyika. Yunasi haelewi kama yu ndotoni au ni ukweli na anamwandikia rafiki yake akimueleza sauti inavyomwambia jinsi alivyofuja pesa za washiriki na kulala na wake zao alipokuwa kasisi. Pia anajipata akisoma kitabu kinachoitwa *Encyclopaedia of Haunted Places* badala ya biblia takatifu chenye wimbo wa *Gehenna.* Yunasi kama mhusika halisi ana imani kuwa, kuna nguvu za ajabu katika jina la Yesu na wote wanaloliita wanaokolewa. Anaona amezungukwa na maiti za watu wengi huku akiongozwa na mtu asiyemjua mwenye koti lenye maandishi MKOMBOZI akiwa na tochi. Anahofia bibi yake (Saida) amekufa lakini anapompigia simu anamkubali Yesu na kuokoka. Mara anaposema amina, anashtuka na kuamka huku uso wake umelowa jasho lakini aliyoshuhudia hayakutokea kwani ilikuwa jinamizi na anaonelea labda yatatokea siku zijazo (uk.149-154).

Kuna mjadala unaotokea mawazoni mwa mhusika Hikmat. Hikmat mtazamaji halisi wa kipindi cha *The Night of the Living Dead* anachangia mjadala kuhusu matatizo yanayokumba Kiafra. Runingani, mjadala una wahusika watatu Ikmat, Kmat na Mat na ghafla kitendo cha kiajabu kinatokea. Hikmat anatoa maoni yake

na wale watangazaji wanakubaliana naye na kumhimiza aendelee na hivyo mtazamaji akawa mtangazaji na watangazaji wakawa watazamaji (uk.171). Ikmat anaeleza jinsi wananchi wamejawa na huzuni wakiona jinsi wanavyodharauliwa na kunyimwa matunda ya uhuru. Anasema tuepuke marejeo ya kitabu cha Maombolezo (4:8-9) yanayosema:

> Nyuso zao ni nyeusi kuliko makaa, hawajulikani katika njia kuu; ngozi yao yagandamana na mifupa yao imekauka, imekuwa kama mti. Heri wale waliouawa kwa upanga kuliko waliouawa kwa njaa maana hao husinyaa, wakichomwa kwa kukosa matunda ya mashamba (uk.172)

Tunaona jinsi uhalisiajabu unavyojitokeza hata katika Biblia takatifu. Ni ajabu kuona binadamu mweusi kuliko makaa mwenye mifupa iliyokauka. Mara nyingi ndoto hubadilika na kuwa ukweli wa mambo. Ndoto hii ya Hikmat inampeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio yasiyowezekana katika hali halisi. Pia tunaona jinsi mtunzi anavyomgeuza mhusika mmoja, na kuchukua nafasi ya wahusika watatu au wanne. Badala ya kutumia wahusika wengi, mhusika mmoja anachukua nafsi ya wahusika tofauti jambo ambalo linawezekana tu katika mtindo huu wa uhalisiajabu.

Matukio ya kiajabu yanafanyika nyumbani mwa Lakeisha. Anamuona rafiki yake Bi. Saeeda Khan akimkata mwanawe Baingama miguu yote miwili na kunyofowa nywele za utosini na kisogoni. Lakeisha anawaona watu wasiofahamika wakimkata mwanawe mkono wa kulia na kuacha wa kushoto ukining'inia. Wanamfukua alikozikwa na wanaunyonga mwili wake hadi kufa halafu kukata

kichwa na ulimi huku mwanawe akilia kwa huzuni. Lakeisha anaona kitendo hiki cha ajabu cha mfu kunyongwa na mara sauti ya mama inasika ikisema: "AMEKUFA MARA MBILI" huku paka mkubwa akitokea na kukimbia. Mara Baingama anamuita na kumuuliza kwa nini analia na ajabu ni kuwa anapokataa kumjibu, mwanawe anamuuliza kama ametumwa na watu wanaotafuta zeruzeru kama yeye (uk.182-185).

Katika mahakama ya kiajabu, Baingama anaona jaji wa Gehenna akiwahukumu Bi. Saeeda Khan kwa kushiriki katika kuua zeruzeru na kunyofoa viwiliwili vyao kwa ajili ya biashara. Kwake Bi. Saeeda haoni mahakama hii ya Gehenna ikiwa na uwezo wa kuhukumu mtu kifo kwa ajili ya zeruzeru kwani ni baraka kupata zeruzeru, kumuua na kuuza sehemu za mwili wake kwa wapiga ramli, na anadai kuwa hata hospitali yake inatokana na mauzo ya viwiliwili vya zeruzeru (uk.187-188).

Katika mahakama hii, Bi. Saeeda na Bi. Rebecca Balira wanasukumwa pembeni mwa rusu ya *Chhaldabius* huku Mwanahamisi Mruke na Methodia waliowatesa wakiwa wafanyikazi wa nyumbani wanaendelea kupiga soga pahali pa starehe. Mara Baingama anasikia sauti ya mamake Lakeisha ikimuita na anashtuka anapogundua alikuwa amelala usingizi mzito ulioambatana na jinamizi kali. Mtunzi anamshirikisha msomaji anapouliza kama anafikiri ilikuwa ni ndoto (uk.189). Mtunzi kwa kutumia uhalisiajabu katika ndoto ya aina hii anamulika uovu unaotekelezwa na watu mashuhuri kufanya mazingaombwe. Wanasiasa,

wafanyibiashara na watu waovu wanatumia viwiliwili vya zeruzeru kupigia ramli ili watajirike huku wakipuuza haki za zeruzeru na kuwaona kama sio binadamu. Katika mahakama hii, mavazi mekundu kama damu yanayovaliwa na mahakimu pamoja na machozi ya damu ya washukiwa yanadhihirisha hatari.

Katika mandhari ya hospitali, tukio lingine la kiajabu linafanyika. Madaktari, wachungaji na wahudumu wa chumba cha kuhifadhia maiti wanashirikiana na wafanyibiashara haramu kukata viwiliwili vya maiti. Wanaelewa wazi kuwa binadamu wanaogopa binadamu wenzao wanapokufa, na hivyo hawana nafasi ya kuangalia sehemu zote za mwili kabla ya maiti kuwekwa kwenye jeneza. Baada ya kupanga ajali, kasisi Taabu anakimbia kuwaambia manusura kuwa binadamu anapowaumiza, Yesu atawaponya (uk.199). Waovu hawa wanatoa ulimi, masikio, macho na sehemu nyeti na kuweka katika friji na baadaye kuuza. Mara tunapata vichwa vya hadithi magazetini vikisema "BODY PART THIEVES HIT MORTUARY" na wahubiri kuendelea kuombea jambo hili. Ajabu ni kuwa zeruzeru wanauawa ili watu wajitajirishe huku wanasiasa wakitaka kujipatia kura na sasa wamemaliza zeruzeru wanavamia vyumba vya kuhifadhi maiti kutafuta nyeti za watu (uk 200).

Mauaji haya yanatokea wakati watu wanapata maagizo kutoka kwa waganga washirikina, tena matapeli wanaotumia nguvu za giza (uk.208). Mtunzi anaonyesha kuwa ushirikina ni ushirikina tu, uwe ni wa utabiri wa nyota, matumizi ya damu na viungo vya albino, kupiga ramli na kadhalika. Nafsi ya

Baingama inawaomba wananchi wapuuze ushirikina na kule kuamini katika sehemu za miili ya wafu ama albino. Anaendelea kusema kuwa kifo ni kazi ya Mungu na ndiye aliyetoa uhai kwa binadamu na atauchukua siku atakayopenda kwani kifo ni siri ya Mungu (uk.210).

Katika mandhari ya Mahakama, Takosani na Sikujua wanashtakiwa kwa makosa ya kumuua Yunasi na familia yake. Takosani anakiri kuwa yeye ni mtumishi wa shetani na amekuwa akiwasiliana naye tangu akiwa na umri wa miaka miwili na pia anatawaliwa na nadharia za ajabu na kuweka imani yake kwa msingi wa kitabu kimoja cha *The Codex Gigas.* Katika mandhari haya, tunaona wakili wake akimtetea kwa sheria zinazowalinda wenye matatizo ya kiakili lakini kwake Takosani anasisitiza kuwa yeye si mwendawazimu lakini ni mwenye imani ya dini ya kishetani (uk.212-218). Hapa, mtunzi anatoa mwanga jinsi mawakili hutetea washukiwa hata kama wametanda maovu bora tu walipwe na wajinufaishe.

Mahakama ya Gehenna inaendelea kuhukumu wahusika waliotenda mambo maovu. Kuna mchezo baina ya wahusika wawili wakubwa (Munkari na Nyamaume) na wahusika wengine wa Gehenna. Bi Saeeda Khan ni mhusika hewa asiyekuwepo ila jukumu kubwa ni kuwa mchezo unachezewa fikrani mwake. Anapuliza parari kubwa kuwaita watu wa Gehenna waje wahudhurie hotuba. Munkari anawahutubia halaiki hii kubwa akiwa amebeba hinzirani kubwa na kibogoshi chenye mafuvu ya watu. Wanaohutubiwa wanalia na kutoa sauti za

popobawa, lakini ni wakati wa kupewa mhadhara kwa dhambi walizotenda duniani (uk.221). Munkari anawaeleza kuwa wako pale kwa hiari yao wala hawakuletwa na yeyote na anawahoji kwa sababu ingawa wamekufa wao ni T*he living dead* (uk.221). Anawaeleza kuwa wameshiriki uongozi mbaya unaosababisha kutikisika kwa Kiafra huku akisisitiza ufisadi ung'olewe kwani *mafamba* ni hatari na ufisadi ni ugonjwa (uk.222). Mhusika huyu wa kiajabu anaeleza kuhusu athari za utandawazi ambapo mafisadi huhamisha utajiri wa Kiafra kwenda kutajirisha nchi nyingine (uk. 224).

Kwa kutumia mchezo huu wa *The Matrix of the corruption in Kiafra* ambao unafanyika fikrani mwa Bi. Saeeda na ambao ni tukio la kiajabu, mtunzi anatumia mhusika wa kiajabu anayeangazia maovu yanayotendeka katika nchi za Kiafra. Munkari anasema kuwa, anaohutubia ni wanaoshiriki ufisadi na anamwamuru Nyamaume avuvie moto (uk. 242). Nyamaume anavuvia moto maradufu na kilio kikali, mayowe na sokomoko kutoka kwa wanaohutubiwa zinaongezeka. Mchezo huu wote unafanyika fikrani mwa Bi Saeeda Khan ambaye ni mmojawapo wa watu wa Gehenna.

Kuna safari ya kuelekea Nahegen na kondakta amejaza gari kupita kiasi na pia gari linaendeshwa kasi ya kilomita 666 kwa saa. Gari linagonga shimo kubwa na dereva anashindwa kulidhibiti kwani linaenda kasi, mafuta yanavuja na moto kuwaka na ghafla mlipuko mkubwa kusikika huku moto ukisambaa kwa kasi na kuangamiza abiria wote wakawa majivu. Ajabu ni kuwa abiria mmoja kwa jina

Angamizamtuwewe II hakufariki. Tukio hili linafanyika huko NdaRwa na mara watu wa Gehenna wanafika katika mandhari ya ajali huku wakisherehekea na kuihesabu mifupa na kutoa hukumu (uk. 243-250).

Matukio mengi yanafanyika katika mandhari ya ndotoni hata ingawa katika hali halisi yaliwahi kutendeka katika nchi fulani. Mfano ni ndoto hii ya kondakta ambayo hata kama mtunzi hajasema nchi hiyo ni gani, inaonekana ni nchi ya Rwanda ambapo maelfu ya watu waliuawa katika vita vya kikabila na ilivyobaki ni watu kwenda kuhesabu mafuvu na mifupa iliyohifadhiwa.

Naye Faki Nahodha anazindushwa na mlio wa arafa ya ujumbe mfupi unaotoka parokia anayohudumu kasisi Taabu akitakikana huko kwa mipango ya mazishi kwani kasisi Taabu amepatikana kwenye madhabahu ya kanisa akiwa amejitia kitanzi. Anapofika huko parokia, haamini anachokiona na hivyo anapigwa na mshangao wa ajabu. Anampata kasisi akinywa chai, huku anasoma gazeti la *The Tombstone Epitaph* ambapo kasisi mmoja anashtakiwa kwa kumnajisi msichana wa umri wa miaka 13 kwenye madhabahu ya kanisa. Hii ni sadfa kwani kasisi Taabu alikuwa amefumaniwa na kibiritingoma mwingine wakiwa katika mahaba mazito kwenye madhabahu huku wanakunywa divai chapa *Blasted Church.* Ghafla, kasisi Taabu anamuuliza Faki Nahodha kama amuongeze chai. Faki anashtuka kwani kadhia hiyo yote inafanyika akilini mwake kwa kipindi cha sekunde sita pekee, pale pale anapokaa na kasisi Taabu (uk.253-257).

Mtunzi anatumia mandhari ya uhalisiajabu kwenye fikra za mhusika wake ili aonyeshe jinsi uovu umekithiri hata makanisani. Wachungaji wenye jukumu la kuchunga kondoo wako kwenye mstari wa mbele kunajisi wasichana wadogo huku wakijihusisha na vibiritingoma. Pia wanafuja pesa za kanisa na kunywa divai na wapenzi wao.

Nafsi ya Hikmat inachipuka tena na inaongea na Hikmat. Ni ajabu kuona mhusika anajadiliana na nafsi yake na kutoa uamuzi. Katika mandhari haya, uamuzi unapatikana kuwa, ukosefu wa vifaa muhimu hospitalini na shuleni, barabara mbovu, kiu na njaa inayowakabili Wakiafra inatokana na jinsi taasisi zinavyoongozwa kwa njia mbaya. Kuna hurafa mbalimbali ambazo zimetolewa kuhusu chanzo cha ufisadi. Hurafa moja ni kuwa, wakati wa enzi ya kiongozi fulani wa Kiafra, falsafa iliyoeleza ufisadi ilikuwa "kanyoni *gakwa wihithahithe na wonwo nduri wakwa"* yaani ndege wangu mdogo, endelea kujificha na utakapopatikana, hutakuwa wangu (uk. 263). Hivyo huu ndio ulikuwa msingi wa ufisadi lakini wakati kiongozi wa pili anapochukua hatamu za uongozi, falsafa ile inabadilika na kuwa "*Kanyoni gakwa oya kiria giothe uroya onawonwo turi o hamwe"* yaani ndege wangu mdogo chukua chochote utakacho na hata utakapopatikana sote tungali pamoja. Hivyo wanaume na wanawake wanaendelea kuharibu raslimali za nchi na kutumia hazina ya uzeeni kujinufaisha bila kuwajali wakongwe waliostaafu. Nafsi ya Hikmat inaendelea kumueleza kuwa hii ndiyo sababu historia ya taifa itakayosimuliwa na kuandikwa sura kama vile G.berg,

Mol Ashes, A. leasing, F.P.E.P, Makaburi na nyinginezo kutengeneza historia (uk. 264-266).

Mara mkewe, Takosani binti Abadalla mkewe anamwamsha Eks huku amelowa jasho na kuonekana kama alikuwa kwenye jinamizi. Anapofumbua macho, anajiona na kuiona dunia halisi. Ni tukio la kiuhalisiajabu jinsi mhusika huyu anavyobadilika na kuchukua maumbile ya wahusika wengi tofauti tofauti. Anakumbuka vema kuwa huko (ndotoni), alikuwa anazinduka, mara analala, mara anaamka, mara anafariki, mara anafufuka, mara yumo Gehenna, mara anateketea, mara yu baharini. Anachotaka kujua ni; nini kilitokea, mbona kilitokea, lini kilitokea, vipi kilitokea, wapi kilitokea na nani alifanya kitokee. Anapatwa na woga huku akifikiri matukio yote yaliyotokea ndotoni na anajaribu kuyasukuma nyuma. Anachokumbuka ni kuwa kabla ya kuupata usingizi ule mzito na kuzama katika jinamizi alikuwa ameusoma ukurasa wa mwisho wa riwaya ile yenye picha ya jalada na mifano ya watu wengi wakiwa katika bahari kubwa ya moto mkali wakiwa wanalia huku wamesimama kwa maumivu makali na kutoa machozi ya damu- riwaya ya *Watu wa Gehenna.* Asipojua hakika ni ikiwa yeye yu hai au mfu. Tunaona jinsi mitindo ya mbinu rejeshi na ukumbukaji inavyotumika katika mtiririko wa riwaya nzima.

### 4.2 WAHUSIKA WAKUU

Katika riwaya hii ya *Watu wa Gehenna,* mtunzi ametumia wahusika halisi na wahusika wa kiajabu katika kuendeleza dhami ra na maudhui ya kazi husika.

Kutokana na kushiriki katika matendo na migogoro muhimu katika kazi hii, tumetambua wahusika wakuu wawili ambao mtunzi amewapa uwezo wa kubadilisha nafsi na maumbile yao na kuchukua maumbile ya wahusika wengine tofautitofauti. Wahusika hawa ni Eks Ngwenyama na Takosani Binti Abdalla. Aidha, haya yote yanafanyika mawazoni mwa wahusika hawa wawili wakuu. Mtunzi amewaumba wahusika hawa kwa ustadi mkubwa hivi kwamba, ni vigumu kutambua wakati wanabadilika kutoka nafsi moja hadi nyingine ama kutoka mhusika mmoja na kuchukua maumbile ya mhusika mwingine ( uk 266-267).

### 4.2.1 Mhusika Eks

Eks ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* na jina lake kamili ni Eks Ngwenyama. Ni mhusika wa kiajabu sana kwani nafsi yake inabadilikabadilika. Kawaida nafsi yake haikuwa inalala lakini ajabu ni kuwa siku moja inaamua kulala. Sauti ya mbali sana inamwambia nafsi yake imelala, lakini yeye hajui ataiamsha namna gani na ndiyo inayompa mwelekeo.

Ni mhusika ambaye pia anabadilika na kuwa mhusika tofauti. Eks anabadilika na kuchukua nafsi ya wahusika halisi. Mwanzoni mwa riwaya (uk 10), tunampata Eks akizungumza na nafsi yake kama mhusika tofauti. Kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi, anaendelea kubadilikabadilika. Mara, anageuka na kuwa Sikujua, mara Mwalimu Baya, mara Yunasi, kasisi John, Baingama na mara Hikmat.

Ni katika fikra au akilini mwa Eks tunapopata mandhari ya kufanyika hadithi hii akiwa ndotoni. Eks anazungumza na nafsi yake ambayo inamhoji na kumuuliza binadamu ni nani. Anaposhindwa kujibu nafsi yake inamcheka. Kicheko hiki cha ajabu cha nafsi yake ni ishara ya kujicheka kwa binadamu kutokana na kushindwa kudhibiti maisha yake.

Eks ameifanyia kazi kampuni ya THE WORLD CEMENTES INC. kwa muda wa miaka 40 na wakati anapopatwa na matatizo ya kiafya anafurushwa (uk 10-17). Kwa hivyo, hapa Eks anawakilisha binadamu halisi na jinsi wanavyodhulumiwa na waajiri wasio na utu. Pia, hajafanikiwa kupata mtoto kwani shahawa zake zinapatikana na kasoro kulingana na madaktari. Eks na mkewe wanaishi maisha ya starehe na kula chakula kizuri kama vile nyama choma na mvinyo kinachomfanya awe na kitambi kinachomzuia kuvaa nguo anazotamani, kutembea, kufanya kazi za nyumbani, kuendesha gari, kuinama kuchukua ufunguo na pia kutekeleza kitendo muhimu cha ndoa (uk.18-19).

Eks anakalia kiti cha jeuri na kuendelea kumlaumu Mzee Afisul kwa kumpa ugonjwa na vilevile kumchukua mkewe. Kwake Eks haoni kama ni ndoto lakini anasikia sauti ya mzee Afisul ambayo haikumtisha. Ni mhusika shupavu na anamuuliza kama yeye ni shetani, Mzee Afisul anakana na kuendelea kumpa fomula ya akili ya binadamu, na kuwa Gehenna imo akilini mwa binadamu.

Eks kama mhusika wa kiajabu ana nafsi mbili. Nafsi yake ina uwezo wa kumuamuru afe na vilevile afufuke. Tunaambiwa ya kuwa baina ya kufa na kufufuka kwa Eks kulichukua miaka saba. Katika miaka hiyo saba MKUU na EKS wanaulizana na kujibizana maswali. Katika nadharia ya uhalisiajabu, tunapata wahusika wakiajabu wakifanya matukio ya kiajabu.

Eks Ngwenyama ni mhusika ambaye ana uwezo wa kubadilikabadilika na kuchukua maumbile ya wahusika wengi tofauti tofauti. Mara anazinduka mara analala, mara anaamka, mara anafariki, mara anafufuka, mara yumo Gehenna, mara anateketea, na mara yu baharini. Ni mhusika aliyekata tamaa na kutaka kujua nini kilitokea, mbona kilitokea, lini kilitokea, vipi kilitokea, wapi kilitokea na nani alifanya kitokee. Anapatwa na woga kwa yale yote amepitia na kile ambacho hajui ni ikiwa yeye yu hai au mfu (uk. 266-268).

Mtunzi ametumia mhusika EKS na kufinyanga fikra zake akachukua maumbile ya wahusika wengi huku akidhihirisha uovu katika jamii. Ingawa kuna wahusika wengi, katika riwaya hii ya watu wa Gehenna, wahusika ni wawili tu ambao ni Eks kama alivyo mhusika K katika *Babu Alipofufuka* na Takosani binti Abdalla. Hawa wawili wametumiwa na mtunzi kuwakilisha wahusika wengine katika nafsi zao.

### 4.2.2 **Takosani binti Abdalla**

Takosani ni mhusika wa kiajabu ambaye mtunzi amemuumba kama mhusika anayebadilikabadilika na kuchukua nafsi za wahusika wengine. Kama mhusika halisia, anapenda kuona mumewe Eks anakula chakula kizuri. Pia hajafanikiwa kupata mtoto. Anatembelewa na ziraili magharibi ya siku ya kwanza ya mfungo sita na anaenda zake jongomeo na kumuacha Eks.

Tunamuona Takosani akibadilika na kuchukua nafsi na maumbile ya wahusika tofauti. Anabadilika na kuwa Takosani binti Inatesh (yaani binti shetani), mhusika wa kiajabu. Ni mwenye nia mbaya na anataka kumteka mhusika kwa jina Sikujua na kufanya mapenzi naye na hivyo kumnasa awe mfuasi wake. Ni mdanganyifu kwani anasema kuwa wanaume ni waongo ilhali anamnasa Sikujua. Ni mwenye uchu wa mapenzi na anasema angependa mwanamume mwenye mapenzi ya kweli. Kwa ustadi mkubwa anamuonya Sikujua kuwa akimjua kabisa hatamuweza kwani hajui jinsi anavyoishi, anachokula na kunywa na starehe zake. Aliwahi kufunga ndoa na Mwarabu lakini ndoa ile ikavunjika baada ya siku saba na hivyo anaamini wanaume ni wakorofi na anaonelea vyema kubaki peke yake (uk. 41-42).

Takosani binti Inatesh ni msiri na mlaghai kwani analia kwa uchungu akimwomba Sikujua asimuoe kwa maana hangeweza kuyatii masharti yake lakini haya ni machozi ya mamba. Anafanya matendo ya kushtua na kuogofya lakini kwake Sikujua anashindwa kudhibiti hisia zake juu yake kwa sababu ya urembo

wake huku akisahau sio vyote ving'aavyo ni dhahabu. Ana mazoea ya kuombea kaburi la mama yake lililoko Kizingitini kisiwani Pate, huku akilipigia magoti na kuliwekea sarafu na lazima kila usiku aamke na kwenda makaburini. Anaposafiri, lazima aombe ruhusa mizimu yake iridhike na sarafu yake ambayo kwao ni salamu. Uraibu wake ni kuogelea baharini na macho yake yanabadilikabadilika na kwa hivyo anavaa miwani (uk. 42-43).

Katika mandhari ya hoteli ya *Anneheg Xpress* katika mtaa wa *Reciful Meadows,* Sikujua analipia vyumba viwili, chumba nambari 15 na chumba nambari 18 lakini Takosani anataka chumba nambari 13 na hivyo kumtaka Sikujua abadilishiwe chumba kile. Chumba kinapatikana ambacho kimeandikwa "*Room Thirteen*" kwa rangi nyekundu tena nzito sana kama rangi ya damu. Ni mwenye kupenda mahaba na anateta anahisi joto kali na kuomba apunguze nguo huku Sikujua akifarikija moyoni akimuona akiendelea kutoa nguo zote kwani kwake huu ulikuwa ushindi mkubwa. Kwake chumba nambari 13 ni cha maana sana cha kumwezesha kutekeleza shughuli zake lakini Sikujua mhusika wa kiuhalisia hang'amui chochote (uk. 44-45).

Anapenda kujipulizia manukato makali aina ya chapa *poison* yanayomfanya Sikujua apate tabu kupumua ilhali haonyeshi kukerwa na harufu hiyo. Ajabu nyingine ni kuwa Takosani anaondoka kwa kupitia ukutani na anaporudi chumbani harufu ya manukato inamtanguliza. Anamwambia Sikujua kuwa angetaka kumpa utajiri jambo linalomfanya Sikujua amuulize kama yeye ni jini.

Anaseme yeye si jini na hadithi za majini haziamini lakini hangethubutu kumpa utajiri ingawa ana uwezo kwani akiwa tajiri atamsahau Mungu.

Pia ana uwezo wa kumfanya Sikujua apoteze fahamu na pia kumpeleka makazi yake chini ya bahari jambo ambalo linamfanya Sikujua ashindwe kama anaota ndoto au ni hali halisi kwani haoni jinsi mandhari yanavyobadilika. Anamueleza Sikujua kuwa makazi yake ni chini ya bahari na kuwa duniani anafika kutekeleza shughuli maalum. Anapenda nyimbo na anataka Santuri ya MWAKA WA SHETANI. Ajabu ni kuwa Sikujua haelewi kuwa katika dunia ya akina Takosani maneno huandikwa kinyumenyume na hivyo basi ni vigumu binadamu halisi ambaye sio wa dunia yao kung'amua maana yake. Anapodadisi santuri zile anapata santuri iliyoandikwa kwa rangi nyekundu tena nzito *inatesh aw akawn* na mchoro mkubwa wa ngorombwe upande mmoja na upande wa pili umechorwa picha ya parari. Anaeleza kuwa mwaka fulani unaweza ukawa wa shetani hivi kwamba kila unachotaka kufanya hakitimii na kila mpango unavurugika. Mambo haya yanamfanya Sikujua asijue kama anaota ama ni hali halisi lakini ukweli ni kuwa hali halisi na ndoto ni kitu kimoja (uk. 48-52).

Mtunzi anatumia mhusika huyu wa kiajabu kudhihirisha kuwa katika maisha ya binadamu, matukio haya ya kiajabu hutokea hata kama ni ndotoni na kuwa mara nyingi mambo haya yanaonekana kama ya kiajabu lakini yanakuwa halisi kwani baadhi ya watu wanaabudu shetani na nguvu zingine za giza na wakati tunapotagusana nao katika maisha halisi, matukio ya aina hii yana uwezekano wa

kutokea. Pia anataka msomaji aelewe kuwa, ni vigumu kuwatambua wahusika wa kiajabu miongoni mwa binadamu halisi.

Katika fasihi simulizi za jamii nyingi za Afrika, watoto walikuwa wamefunzwa kuhifadhi siri kwa wageni na pia kutowafuata kwa vile hawakuelewa nia zao. Katika hadithi moja kutoka jamii ya Wakikuyu, wasichana walienda kucheza densi kama ilivyokuwa kawaida baada ya mavuno. Wasichana wale walipatana na kijana mmoja mtanashati na wote wakapendezwa naye. Sherehe ilipokwisha, wasichana kumi walimfuata kwani kila mmoja alitamani kuolewa naye. Njiani, yule kijana alikuwa akiwashika nzi na kuwaweka kisogoni mlimokuwa na kinywa kilichokuwa kimefunikwa na nywele. Msichana aliyekuwa nyuma yake aliona kitendo kile cha ajabu na kugundua kijana huyo alikuwa jini na hivyo akawaambia wenzake kuwa hataendelea na safari kwani alikuwa ametumwa na mzazi wake kwenda kuteka maji. Kila mmoja alipata nafasi ya kuona kitendo cha kumega nzi na wasichana tisa wakajipatia sababu za kutoendelea na safari akabaki mmoja ambaye hakutaka kumuacha. Walipofika nyumbani kwa yule kijana, ajuza mmoja alishtuka kumuona na akamueleza kuwa yule ni jini na alikuwa amemnasa kule ili awe akimpikia wasichana warembo. Yule ajuza alimnusuru na kumuonya kuwa, sio chote king'aacho ni dhahabu.

Kutokana na hadithi hii, tumebainisha kuwa uhalisiajabu ulitumika sana katika fasihi simulizi za jamii nyingi na hutumika kuwaelimisha, kutahadharisha na kuwaonya watu kuhusu dunia wanamoishi. Kisa hiki kinafanana na kisa katika

riwaya hii ambapo Sikujua anaona bahati ya kupata msichana mrembo, na hata baada ya kuona matukio ya kiajabu anayoyafanya, yeye amenaswa na urembo na mapenzi kwa mtu asiyemjua hakika.Vilevile, mtunzi, anaonya jamii kutojihusisha na watu ambao hawaeleweki vyema mienendo na nia zao.

Takosani ni muuaji kwani anasababisha kifo cha Yunasi na familia yake. Takosani na Sikujua wanaonekana watumiaji wa dawa za kulevya, wamejichora picha za kutisha katika miili yao, kujitoboa toga masikioni, puani, kwenye ulimi, kidevuni, midomoni, kwenye nyusi na kujivika vipuli na kukata nywele zao kwa mtindo wa kiajabu. Anavaa mavazi meusi yenye michoro ya mafuvu ya watu na joka kubwa na pia yenye maandishi ya kiajabu yaliyoandikwa kwa rangi nyekundu *Oxyuranus mirolepidotus.* Mikononi amejichora *Dragon yin yang* wa Uchina na fomula ya nishati ya $E=MC^2$. Fulana yake imeandikwa swali na jibu; *"Do we not possess superior intelligence? We Simply do" (uk. 215).*

Ana nguvu za kiajabu kwani anaiba bunduki aina ya metal storm na makasha mawili ya risasi kutoka kwa afisa mmoja wa kitengo cha udhibiti wa silaha. (uk. 214-215). Anapopelekwa mahakamani anakiri kuwa yeye ni mtumishi wa shetani na kuwa amekuwa akiwasiliana naye tangu akiwa na umri wa miaka miwili, pia ni mpinzani wa masihi Yesu Kristu na ni binti wa shetani hivyo Takosani binti Inatesh. Ameweka imani yake kwenye *The Codex Gigas* biblia ya shetani. Wakili wake anapomtetea kuwa ana matatizo ya kiakili kwani watu wa aina hii wanalindwa kisheria, anaamini kuwa yeye sio mwendawazimu na anaongezea

kuwa ana mpango unaoratibiwa na baba yake shetani wa kuwaandaa vijana wote duniani waasi (uk.216-218).

## 4.3 **WAHUSIKA WADOGO**

Wahusika wadogo katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* wamechukua nafasi kubwa katika kujenga dhamira na vilevile katika ujenzi wa wahusika wakuu ambao ni Takosani binti Abdalla na Eks Ngwenyama. Aidha wahusika hawa wadogo ni wengi mno lakini kwetu tunaangalia wahusika wa kiajabu watakaotusaidia kuwekea misingi nadharia hii ya uhalisiajabu.

### 4.3.1. **Mishi**

Mishi ni mhusika wa kiajabu anayeonekana na mara kutoweka kiajabuajabu. Kutoka fasihi ya Ugiriki wa kale, kuna mhusika wa kiajabu kwa jina Muse mwenye nguvu za kiajabu na tunaweza kumlinganisha na Mishi katika *Watu wa Gehenna.* Ni mhusika muhimu sana katika kuendeleza riwaya na kudhihirisha uhalisiajabu katika hadithi. Tunapata Mize mhusika muhimu katika riwaya ya *Dunia Yao*, mwenye sifa za kiajabu kama Mishi. Mishi ni mhusika wa kiajabu anayeingia riwayani akiwa kama dhana kwenye akili ya mhusika Mwalimu Baya. Ana uwezo wa kujipa mwili wa kumvutia Mwalimu Baya, kama mwanamke wa kutamanisha. Mwalimu Baya anatamani sana kufanya mapenzi naye.

Mishi kama mhusika wa kiajabu ana uwezo pia wa kukwamisha gari la Mwalimu Baya katikati mwa reli treni inapokuwa inakuja kwa mwendo wa kasi. Mara kwa

mara, analitamka jina *Shemhamforash!* kila wakati tukio la kiajabu liko karibu kutokea. Haonyeshi dalili ya kufahamu hatari inayowakabili ya kugongwa na treni na wala hana hofu. Anamkumbatia Mwalimu Baya mikononi mwake na hivyo ana uwezo wa kiajabu wa kumuokoa binadamu halisi na kumfumba macho asing'amue kinachotokea. Mabehewa ya treni yanapita ndani yao kama waliokuwa mizuka huku wakiona viti, watu na kila kitu ndani ya treni huku treni inakwenda kwa kasi. Lakini kwake Mishi hili ni jambo ambalo si ajabu. Anaashiria nguvu za giza zinapompiga Mwalimu Baya kwenye kisogo na kumfanya aanguke chini kama gunia la mchanga.

Ni mhusika anayejibadilishabadilisha kiajabu kwani wakati mmoja mwalimu Baya anamuona na viatu vya wazi na mara miguu yake inabadilika na kuwa kwato za ng'ombe huku Baya akimuona jini lakini asiweze kujinasua kwake. Pia ana uwezo wa kuingia popote wakati wowote na kupitia popote hata ukutani bila binadamu halisi kufahamu. Ana uwezo pia wa kutawala nafsi ya binadamu halisi (Baya) kwa kumfanya alale usingizi mzito na kuota ndoto huku akiendelea kufanya mapenzi naye. Anajibadilisha mwili na mgongo wake kuwa na magamba na mara mwili unakuwa baridi kama barafu.

Mwili wa mhusika huyu wa kiajabu una uwezo wa kutoa mwanga wenye rangi ya mbalamwezi angavu. Mara mwili wake unageuka na kuwa kila kitu nusu toka juu hadi chini yaani jicho moja kwenye paji la uso wake, titi moja, mkono mmoja, mguu mmoja, nusu ya kila kitu.

Ajabu ni kuwa Mishi alikuwa mke wa Shehamforash na hivyo ni shetani wa mahaba na pindi tu mwanamume analala naye katika ndoto, anateuliwa na kupata laana kuwa hatalala na mke mwingine hadi kifo. Hivyo, amemteua Mwalimu Baya na kumning'iniza juu ya mti wa mbuyu akiwa uchi wa mnyama.

### 4.3.2 **Shamsa Muhashamy (Baadayadhiki)**

Mhusika Shamsa ni mhusika wa kiajabu na anaishi makaburini. Ni mpweke kwani anaishi peke yake kwa muda wa miaka miwili na chakula chake kikiwa maji ya marashi. Ni rafikiye Takosani anayependelea kumuita Baadayadhiki. Shamsa ni mpiga ramli na anasema alianza kupiga ramli kule Mbwajumwali na kuhamia Mombasa baadaye. Ni msimulizi hodari na kupitia kwake, tunapata kisa cha mwanasiasa mmoja kwa jina Vuai Nahodha alivyopewa wadhifa wa Waziri wa Afya na kushindwa kutekeleza wajibu wake. Anaeleza kuwa, mwanasiasa huyu aliweza kuwasiliana na madaktari wa vituo vya afya vya Tandauwa, Ndagoni, Wingwi, Makangale na Bogoa kupata kuchukua sampuli za damu za wagonjwa na baadaye kupanga njama ya kufyonza damu mbichi chupa 40 na kutupa miili ya wagonjwa. (uk.70). Anaelewa mambo halisi jinsi haki za wanyonge zinavyokiukwa, ufisadi na kuondolewa jamii fulani katika eneo fulani na kupiganisha makabila ni mambo yanayorudisha maendeleo nyuma katika Kiafra. Mtunzi anamtumia kufichua siri za wanaotenda maovu.

4.3.3. **MKUU**

MKUU ni mhusika wa kiajabu na ambaye anapatikana akilini mwa mhusika Eks. Ni mhusika mwenye uwezo wa kumhoji na kumuelimisha Eks. Akiwa kama nafsi ya Eks, anamuamuru Eks afe halafu afufuke. MKUU anamlaumu Eks kwa kupokea maelezo maovu kuhusu mchezo wa Sataranji kutoka kwa Mzee Asiful na ndio maana anamwamuru afe. Baina ya kufa na kufufuka kwa Eks kunakochukua miaka saba, na ni katika miaka hii ambapo MKUU na Eks wanaulizana na kujibizana maswali.

Ana uwezo wa kujua yanayotendeka na vilevile anayoyaona Eks akiwa amelala. Mkuu anaelewa wazi kuhusu dunia ilivyoumbwa na kuwa Mungu mwanzo aliumba ardhi kavu, akafinyanga konde, akawaumba wanyama na samaki… kabla ya kumuumba Eks, kwa maana ya binadamu. Ni mwanasayansi anayeelewa umuhimu wa majani na matunda katika kuimarisha afya ya binadamu. Ni mwalimu na ana utaratibu wa kuuliza na kujibu maswali kwani anamuelimisha Eks kuhusu lishe bora. Anamwamuru Eks asiukaribie mlango wa Gehenna. Ana uwezo wa kufyatuka na kufifia angani.

MKUU anaelewa vyema matatizo ya watu duniani hasa matatizo ya kiafya. Anaelewa kuwa mataifa ya Kiafra yana uchache wa hospitali, madaktari na dawa na hii imechangiwa na kutotilia maanani dawa za asili huku wakizikumbatia zile za nchi za magharibi ambazo ni wachache tu wanaoweza kuzigharamia. Kwake, dawa hizi ni zile ambazo muda wake wa kutumia umeisha au zile zinazofanyiwa

majaribio kwa mara ya kwanza na ni zenye athari ambayo haijafahamika. Hivyo wanatumika kama vipanya vya maabara.

Ni mwenye hekima na anapoulizwa na Eks kama ana ushahidi kuhusu madai yake, anatoa majibu kuyatetea maoni yake kuwa katika enzi za mababu wa akina Eks, kila ugonjwa ulitibiwa na aina fulani ya miti shamba na kulikuwepo na watu wa kufanyia utafiti dawa hizo. Anapendekeza kuwa watafiti hao wangeendelea, kungepatikana dawa ya ukimwi.

MKUU ana uwezo na nguvu za kiungu. Anamrejelea Mungu pamoja na maandiko matakatifu kwa ustadi. Anasema kuwa Mungu alipomuumba mwanadamu, alimwekea duniani kila aina ya miti kwa matumizi mbalimbali na moja ya matumizi hayo ilikuwa ni dawa. Kwa hivyo, tatizo la kuendelea kuumwa wakati kuna dawa silo tatizo la Mungu ila ni la binadamu. Anasema:

> Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu
> watajinyenyekeza watubu dhambi zao na kuniomba, mimi
> nitasikia kutoka POPOTE na kuiponya Kiafra. Nadhari
> njia ya peponi (uk 37).

Mtunzi anamtumia MKUU kudhihirisha nguvu za kiungu. MKUU anajua kuwa tatizo la Wakiafra ni kufikiri kuwa utaalamu wa bara jingine ni bora kuliko ule wa kwao. MKUU anatahadharisha maendeleo kama adui mkubwa wa binadamu huku akijiita '*INTELLIGENT!*' Binadamu anapotengeneza ndege, basi anahitaji utaalamu wa kutengeneza mahali pa kuegesha hewani ili irekebishwe

inapoharibika. Kwake Mungu amempa binadamu uhuru wa kufanya atakavyo na kwa hivyo akitengeneza umeme halafu umchome, asimlaumu Mungu kwa maana umeme sio moja ya vitu alivyoweka ulimwenguni pale mwanzo, na YEYE hajui umeme ni kitu gani. MKUU anawalaumu madaktari ambao wamepewa hekima na Mungu na badala yake wanawatoza wagonjwa pesa nyingi ili wajinufaishe.

### 4.3.4 **Munkari**

Munkari ni mhusika wa kiajabu na ambaye ni hakimu wa Gehenna. Ni mlinzi mkali na tunamwona akimzuia Yunasi kumwokoa mkewe Saida kwani yeye si mtu wa Gehenna (uk.219). Akisaidiana na Nyamaume, wanawazuia Bi Saeeda Khan na Bi. Rebecca Balira wasitoroke Gehenna ili wapate adhabu ya maovu waliotenda – huku wakitumia neno Nobe*!* Anajua maovu yote ambayo kila mshukiwa ameyatenda na hivyo yuko tayari kuwasomea mashtaka na kuwapa adhabu kali (uk. 226-227).

Anapendelea michezo ya kuigiza wakati anapotoa hukumu huku akishirikisha wahusika wa Gehenna kama vile Bi Saeeda ambaye mchezo umo fikrani mwake. Munkari ana jukumu la kuwakaribisha watu Gehenna (uk. 248-252). Pia ana uwezo wa kuchipuka ardhini kiajabu huku amevaa sare nyekundu kama damu na kuanza kucheza na kasisi Taabu aliyemdhalilisha kijinsia binti mmoja kwa jina Kinaya katika madhabahu ya kanisa wakati alikuwa padre. Anaielekeza bunduki kichwani na kujifyatulia lakini hakuna risasi inayotoka na anapomwambia kasisi Taabu ajifyatulie, risasi inatoka kwa hakika na kuufumua nje ubongo wake huku

watu wa Gehenna wakiukimbilia. Anaeleza sababu ya kasisi kupata adhabu hiyo ni kwa kutokuwa mwaminifu katika kiapo chake cha useja (uk. 255).

Munkari anaonya kuwa watenda dhambi wote watahukumiwa na kupewa adhabu kali siku moja baada ya maisha ya duniani.

4.3.5 **Hikmat**

Hikmat anatokea kama mhusika halisi ambaye anazindua rasmi kampeni za ubunge pale Ndotoni. Ni mwenye maarifa na anapongezwa na wananchi kwa kuzindua manifesto yake yenye ushawishi mkubwa na ahadi zenye kupigania uhuru wa nchi za Kiafra hata ingawa uhusiano wao na nchi za kigeni utadhoofika (uk. 159). Ni mhusika mwenye nafsi mbili. Moja ya Hikmat yeye anayetimiza ndoto zake kikweli na Hikmat mwingine mwanasiasa anayetimiza ndoto zake kibahati.

Ni mfuasi wa kipindi cha *The Night of the Living Dead* kwenye runinga kwani kinaleta mjadala kuhusu changamoto katika nchi za kiafra. Ana uwezo wa kuchangia mjadala huu moja kwa moja na ajabu ni kuwa anageuka kuwa mtangazaji nao watangazaji watatu ambao ni Ikmat, Kmat na mat wanakuwa watazamaji. Nafsi yake ndiyo yenye wahusika Ikmat, Kmat na Mat na mjadala unafanyika akilini mwake lakini unaonekana kama mjadala halisi. Nafsi yake na yeye wana mazoea ya kufanya dayalojia pamoja hasa kuhusu uongozi mbaya unaosababisha kusambaratika kwa nchi za Kiafra (uk. 263-266).

Ni mtetezi wa wanyonge na anakashifu jinsi wabunge kama wawakilishi wa watu wanavyosimama bungeni kudai nyongeza ya posho zao badala ya kuomba sehemu ya mishahara yao ikatwe kwa ajili ya kugharimia operesheni kwenye kaunti zao ili kuonyesha upendo wao kwa wananchi (uk. 176).

4.3.6 **Watu wa Gehenna**

Watu wa Gehenna ni wale walioshiriki matendo maovu wakiwa duniani. Wana walinzi wao na mahakimu wao. Wakazi wa Gehenna wana tabia za ajabu sana na kila mmoja wao anajiona afadhali kuliko mwenzake lakini uovu ni uovu na watendao maovu wote ni watu wa Gehenna. Ni wakazi wanaoonekana wakiwa kwenye bahari ya luja au biwi la simanzi na wako kwenye lindi la fikra nyingi.

Ni wabinafsi na kila mkazi wa Gehenna anafuata ajenda yake na kwa hivyo hawana ushirikiano. Hawa ni watu wanaojuta kwa sababu walishiriki katika ukataji misitu, kuwanajisi wasichana, kuiba dawa za hospitali, kupokea rushwa, kupiga ramli, kuua, na kuuza viwiliwili vya albino, kueneza ukabila, kuwapunja wafanyakazi wao, kushiriki ufisadi baadhi ya maovu mengine.Hapa Gehenna, wanawekewa muziki unaoitwa *walijuta* ambao unachezwa kuwakumbusha maovu waliyoyatenda (uk. 8).

Wakaazi wa Gehenna ni wengi na ingawa wanaweza kufanya kazi kwa ushirikiano, azimio lao hasa ni kujitosheleza kibinafsi. Ni watu ambao hawajali kinachofikiriwa na wenzao wanapojitosheleza. Vilevile ni watu wajanja, wenye

akili na kuzidi yote, watu hatari. Siri yao kubwa ni kujitia katika ndoto ya utendaji huria yaani hakuna chochote ila hiari ya mwenye nguvu na hiari ya mnyonge na kila mkazi ana ajenda yake ambayo hamfichulii mwenzake (uk. 9).

Bi Saeeda Khan na Bi Rebecca Balira ni baadhi ya wakazi wa Gehenna wanaohukumiwa kwa kuwatesa wafanyikazi wa nyumba na kuwaua zeruzeru na kuuza viwiliwili vyao (uk. 187). Wote walioangamia kwenye ajali ya barabara huko Nahegen pia ni wakazi wa huku.

Wakazi waliotangulia Gehenna ni watu wanaofurahia wakati kuna tukio la kiajabu litakalowawezesha kuongezeka kama vile mauaji ya kikabila na ajali za barabarani. Baada ya muda fulani, wanakuwa na sherehe za kuihesabu mifupa na kutoa hukumu wakiongozwa na Munkari (uk. 250-252). Watu wa Gehenna ni wahusika wa kiajabu kwani wakati kasisi Taabu anapojifyatulia risasi na kuufumua nje ubongo wake, watu wa Gehenna wanaukimbilia ubongo huo na kumkaribisha awe mtu wa Gehenna. (uk. 255)

Wengine wao ni wauaji na wengine walevi. Wakili Angamizamtuwewe II aliyepanga njama za mauaji ya kimbari nchini NdaRwa mnamo 2064 na mlevi aliyeshiriki kufanya mapenzi ya jinsia moja nchini na mwanamume mwenzake pia ni watu wa Gehenna wenye kilio kikali chenye machozi ya damu huku wakitoa mayowe na kusononeka (uk. 220-242).

## 4.4 HITIMISHO

Katika sura hii tumechunguza na kubainisha mandhari na matukio chungu nzima ya uhalisia na uhalisiajabu kama yanavyojitokeza katika riwaya hii ya *Watu wa Gehenna.* Mandhari haya hasa yanapatikana akilini mwa wahusika kwenye ndoto na wakati mwingine yanaonekana halisi kabisa kwa msomaji, ilhali wakati mwingine yanabadilika na kuwa yenye kushtua na kuogofya.

Pia tumechunguza na kubainisha wahusika wa kiuhalisia na wale wa kiajabu katika riwaya hii. Wahusika halisia wanabadilika na kuwa wa kiajabu na kupata maumbile ya kutisha pamoja na kufanya vitendo vya kuogofya kwa mfano mhusika Mishi. Aidha, kwa kutumia mandhari, matukio na wahusika wanaochanganya uhalisia na uhalisiajabu, mwandishi Tom Olali ameweza kudhihirisha, kumulika na kueleza kwa ustadi zaidi baadhi ya mambo ambayo hayangeweza kuelezwa kwa mtindo wa kawaida. Wamitila (2003:274) anaeleza uhalisiajabu kama sifa ya kuyaeleza matukio ya kifantasia, ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja inayoyafanya yaonekane ya kawaida tu, na hivyo kufanya mpaka uliopo kati ya yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana kuwa mdogo sana. Kwa hivyo, mwandishi Tom Olali ameweza kusimulia chimbuko la ufisadi na maswala mengine ibuka kama vile athari za utandawazi na biashara haramu ya kuuza viwiliwili vya zeruzeru na baadhi ya maswala mengine kwa kutumia mbinu hii ya uhalisiajabu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ambayo ni ya mwisho katika utafiti wetu, tumetoa muhtasari wa matokeo kutokana na uchunguzi wetu. Tunakusudia kubainisha iwapo madhumuni ya utafiti wetu yameafikiwa. Pia tumepima nadharia tete za utafiti wetu pamoja na kutoa mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu.

## 5.1 KUHUSU MADHUMUNI YETU

Katika utafiti wetu, tumeshughulikia riwaya mbili za waandishi wawili, Said A. Mohamed (*Babu Alipofufuka)* na Tom Olali (*Watu wa Gehenna*). Tumetumia nadharia ya uhalisiajabu kuchunguza na kubainisha dhana za uhalisia na uhalisiajabu katika vipengele vya wahusika na mandhari katika riwaya hizi. Tumepata ya kuwa, waandishi hawa wawili wametumia wahusika wakiajabu na mandhari yenye matukio mengi ya kiajabu. Tumebainisha kuwa dhana ya uhalisiajabu imejijitokeza katika viwango vya wahusika na mandhari.

Pia tumetumia tajriba yetu kama wanafasihi kutoa maoni yetu ambayo yametusaidia kupanua mawazo yetu katika kuikamilisha tasnifu yetu. Tumeweza kugusia jinsi uhalisiajabu unavyojitokeza katika fasihi simulizi za jamii zetu na hivyo kudhihirisha kuwa uhalisiajabu sio mtindo mpya lakini umekuwepo katika tamaduni za kila jamii.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia hatua ambazo uhalisiajabu umepiga kwa kuangalia vipindi vya uhalisia hakiki na uhalisia wa kijamaa na kubainisha kuwa kipindi cha uhalisiajabu kiliibuka ili kuweza kuzungumzia masuala ambayo hayangeweza kuzungumziwa kwa njia ya kawaida au kwa mtindo wa kiuhalisia. Kwa kutumia uhalisiajabu, riwaya hizi zimefanikiwa kujadili masuala ibuka na kumulika uozo katika jamii; jambo ambalo mtindo wa kiuhalisia haungeweza. Katika *Babu Alipofufuka*, Babu Mzuka ameyaingilia maisha ya mjukuu wake K na kuyaathiri maisha yake na anavyoendelea kusaka furaha na maana ya maisha ndivyo anapata kinyume chake.

Kutokana na maelezo haya tunapata ya kuwa binadamu anaonekana kutokuwa na uwezo wa kuyadhibiti maisha na maisha yamebaki kitendawili kisichoweza kuteguka. Hivyo tumebainisha ya kuwa binadamu yumo mbioni kupata furaha bila mafanikio. Pia, tumepata ya kuwa, waliokufa bado wangalipo katika hali tofauti na wanaendelea kuathiri maisha ya walio hai.

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*, mwandishi amesimulia chimbuko la ufisadi na kupiga msasa masuala ibuka mathalan biashara haramu ya viwiliwili vya zeruzeru, kuteswa kwa wafanyikazi wa nyumbani katika mataifa ya ng'ambo na vilevile athari za utandawazi katika mitandao ya kijamii maarufu kama '*facebook.*' Kwa mfano, tunampata Lakeisha mamake Baingama ambaye ni zeruzeru amepata mwanamume tajiri wa kumuoa kupitia kwa mtandao na kuwaacha watoto wake wakiteseka na hivyo kuingilia maisha ya ulanguzi wa

dawa za kulevya pamoja na uasherati ili kukidhi mahitaji yao. Mwandishi anakashifu uigaji wa tamaduni za jamii za ulaya na kuacha mila na tamaduni asilia za Kiafrika. Hii ni mifano tu ya masuala ambayo yamezungumziwa kwa ustadi mkubwa kwa kutumia mtindo huu wa kiuhalisiajabu katika riwaya tulizoshughulikia yakaweza kuteka hisia za msomaji.

Katika sura ya tatu na ya nne, tumechunguza riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* mtawalia. Tumebainisha uhalisia na uhalisiajabu katika vipengele vya mandhari na wahusika na kupata ya kuwa, uhalisi na ndoto vinachanganyika na hivyo ni vigumu kuweka mipaka kati ya uhalisia na uhalisiajabu. Hivyo tumewekea msingi nadharia yetu kuwa labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.

Katika utafiti wetu, tumepata mandhari yenye matukio na wahusika wa kiajabuajabu kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya zetu teule. Wahusika wanabadilikabadilika na kuchukua nafsi tofauti na kutenda mambo ya kushtua na kuogofya. Kutokana na madhumuni yetu, tumebainisha kwamba riwaya hizi mbili zinaingiliana na kuchangiana kwa kiasi kikubwa. Aidha vipengele vya uhalisiajabu ni vingi mno katika riwaya hizi lakini tumebainisha tu uhalisiajabu katika vipengele vya wahusika na mandhari na tumepata uhalisiajabu unajibainisha kwa kiwango kikubwa katika riwaya hizi.

## 5.2 UPIMAJI WA NADHARIA TETE

Dhana ya uhalisiajabu imechukua nafasi kubwa katika uendelezaji wa riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.* Tumedhihirisha kuwa uhalisia na uhalisiajabu zinaingiliana sana.

Visa vya kimazingaombwe ni vingi mno katika riwaya hizi mbili. Kuna wahusika wengi wa kiajabuajabu ambao hulka yao inaweza kusemekana inatokana na kutokuwa binadamu kamili. Vilevile, kuna wahusika wengine wa kawaida kwenye riwaya hizi walio na uwezo usiokuwa wa kawaida kama tulivyobainisha katika sura ya tatu na ya nne.

Suala la ndoto katika riwaya hizi mbili limechukua nafasi kubwa kama mojawapo wa mihimili ya uhalisiajabu. Jambo hili la kuchanganyika kwa ndoto na uhalisia limeweka ugumu wa kubainisha mipaka ya uhalisi na uhalisiajabu na ndipo tukaweka msingi mhimili wa uhalisiajabu kuwa labda wakati mtu anapoota ndipo yumo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.

Matukio mengi katika riwaya hizi yametokea mawazoni mwa wahusika wanapolala ama wako macho na kuota ndoto za kiajabu. Ndoto hizi zinaonekana kama matukio halisi kabisa kwa wahusika hawa na zinaathiri maisha yao hivi kwamba, wanafikia maoni kuwa kama hazijatokea, zitaweza kutokea katika hali halisi wakati mmoja.

Tumebainisha kuwa riwaya hizi kuandikiwa katika pahala na nyakati tofauti sio kizuizi kwa dayalojia kati ya riwaya hizi zinazoitika mwangwi wa riwaya nyingine zenye kutumia mtindo kama huu. Hili ni dhihirisho kuwa mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa imevunjwa kwa maana wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja.

Kwa kujitenga na mtindo wa kiuhalisia, riwaya hizi zimo katika tapo la sanaa za kimajaribio zinazojaribu kufaulu pale ambapo uhalisia umelemewa katika kuelezea matukio ya kiajabu kwani, wanauhalisia wanadai kuwa lazima yanayozungumziwa yawiane na ukweli na yawe akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Huenda sababu mojawapo ya waandishi Mohamed A. Said na Olali Tom kutumia uhalisiamazingaombwe katika kazi zao ni kutokana na misukosuko na mawimbi ya mabadiliko na ukosefu wa uthabiti wa kijamii, kisiasa, kiuchumi pamoja na masuala ibuka mathalan biashara haramu ya kuuza viwiliwili vya zeruzeru, kuteswa kwa wafanyakazi wa nyumbani katika mataifa ya ng'ambo na athari za utandawazi katika mitandao ya kijamii.

Kutokana na vipengele ambavyo tumevishughulikia, twaweza kusema kwamba, njia mwafaka ya kufasiri utafiti huu ni kuwa riwaya hizi zimeandikwa katika kuzingatia kaida na kunga za uhalisiajabu ambao umejenga jumuiya pana na inayoendelea kupanuka kote duniani kila uchao. Matumizi ya mtindo huu wa uhalisiajabu umeweza kuangaza uovu na adhabu yake katika jamii kwa ustadi

unaovuta makini ya wasomaji na kuathiri hisia zao. Kuna uwezekano mkubwa wa kuyakumbuka matukio yanayotoa mafunzo kwa wanajamii kama yanavyojitokeza katika riwaya hizi.

Riwaya hizi mbili zina uhusiano mkubwa na kwa kujua au kwa kutojua, waandishi hawa wawili wamo katika dayalojia au mazungumzo yanayoonekana kuigana na kuathiriana kimtindo na kimaudhui. Kimsingi, tunaweza kusema kuwa fasihi moja inasema au inajibizana na nyingine au kutoa mwangwi wa mambo yanayofanana au kulingana na yale ya fasihi nyingine.

Kazi hizi mbili zimetumia sifa bainifu za uhalisiajabu kama nyenzo za kuakisi na kuangaza hali halisi ya udhaifu, kuyumbayumba na ukosefu wa uthabiti na udumifu katika Afrika na ulimwengu wote. Kwa jumla, utafiti huu unatilia mkazo kwamba, uhalisiajabu ndio nguzo kuu ya uendelezaji wa riwaya hizi katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui. Dhamira kuu ya kuangaza uozo katika jamii na adhabu yake imefanikishwa kupitia uhalisiajabu katika vipengele vya wahusika na mandhari ambapo maudhui mbalimbali yamebainika.

Kwa hivyo, tumepata nadharia tete zetu kuwa kweli kwani, vipengele vya uhalisia na uhalisiajabu vimejitokeza kwa kiasi kikubwa na pia dhana ya uhalisiajabu imejitokeza kama mhimili mkuu wa dhamira katika riwaya mbili tulizoshughulikia.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Matumaini yetu ni kuwa, utafiti huu utakuwa msingi bora wa uchanganuzi wa uhalisiajabu wa riwaya za kimajaribio au riwaya mpya. Kwa kuwa utafiti wetu umeshughulikia uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna,* bado tafiti zaidi zinahitajika kwa kuzingatia mielekeo mingine ya kuzihakiki riwaya hizi. Kwa sababu hiyo, tumependekeza utafiti zaidi kuhusu mambo yafuatayo:

1. Watafiti wengine waweze kutumia nadharia zingine kutafiti vipengele tofatutitofauti kwani utafiti wetu umejikita katika vipengele vya wahusika na mandhari katika mwanda mpana wa uhalisiajabu.
2. Uchunguzi wa dhana ya uchimuzi katika riwaya ya *Watu wa Gehenna.*

## MAREJELEO


Alexander, M. (1990). *Flights from Realism.* London. Edward Anold.

Allende, I. (1985). *The House of the Spirits.* London. Anchor Brendon Ltd.

Baldic, C. (2001). *Oxford Concise Dictionary of Literacy Terms*. Oxford. Oxford University Press.

Cooper, B. (1988). *Magical Realism in West African Fiction.* New York: Routledge.

__________ (1998). *Magical Realism in West African Literature*: Seeing *with a Third Eye*. New York: Routledge.

Crystal, D. (1997). *Dictionary of Linguistics and Phonetics.* 4th edition Oxford: Blackwell.

D' Haen, Theo L. (2005). *Magic Realism and Post modernism.* Decentering Priviledged Centers. Zamora Lois Parkison and Wendy Faris (Eds) Magic Realism: Theory, History Community. Durham & London: Duke University Press. PP. 191-208.

Danow, K.D. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grostesque.* Kentucky University of Kentucky Press.

Drouwart,L. (1993). *Journal of the South Pacific Association for Commonwealth, Literature and Language Studies*. London. No.36

Encarta Encyclopaedia (2002). New York. Microsoft Company Limited.

Green, J.A (2009). *Dreams of Freedom: Magic Realism and Visionary Materialism in Okri and Blake*. Romanticism 15/1:18-32.

Gromov, M. (2002). *Post Modernistic Elements in Recent Swahili Novels.* Nairobi. (Haijachapishwa).

Hough, G. (1969). *Style and Stylistics*. London. Routledge & Kegan Paul.

Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Dar es Salaam. Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

_____________ (1991). *Mzingile.* Dar es Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

Khaemba S.S (1999). *Ulinganishi wa Maudhui ya Mapinduzi katika Dunia Mti Mkavu na Kiza katika Nuru.* Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Khamis, S. A.M (2005). *Signs of New Features in the Swahili Novel*. Research in African Literature 36/1: 92-108.

Magaju, J. (2004). *Uhalisiajabu kati ya Riwaya ya Babu Alipofufuka* (2001) ya S.A Mohamed na *Bina-Adamu!(*2002) ya K.W Wamitila. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Malcolm, N. (1959*). Dreaming U.S.A*. London. Routledge and Kegan Paul Ltd.

Marquez, G.C. (1980). *One Hundred Years of Solitude*. London. Pan Books Ltd.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Graphics & Publishers.

Mdee, J. S., Shafi, A., Kiango, J.G. & Njogu, K. (2009). *Kamusi Kamili ya Kiswahili.* Nairobi. Longhorn Publishers

Mkangi, K. (1984). *Mafuta. Nairobi.* East African Educational Publications.

Mugwika, F. (2012). *Dhana ya Uchimuzi katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kimajaribio ya Mafamba.* Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K & Wafula,R.M (2007*). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Nyabunga, A. (2005). *Uhakiki wa Bina- Adamu! (2002) na Musaleo*! (2004) za K.W Wamitila. (Haijachapishwa)

Okri, B. (1992). *The Famished Road.* New York: N.A Talese.

Olali, T. (2008). *Mafamba.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

__________(2010). *Structure and Anti-structure of a Swahili New Novel: A Stylistic Analysis of Babu Alipofufuka.* The Nairobi Journal of Literature, UoN 82-98.

____________(2012). *Watu wa Gehenna.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Robert, S. (1951). *Kusadikika*, London, Nelson.

____________(1967). *Kufikirika*. London: Nelson.

Roh, F. (1925) Nach-Expressionismus-Magischer Realismus. Leipzig. Krinkhardt & Biermann.

Said, A. M. (2001). *Babu Alipofufuka.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

___________ (2006). *Dunia Yao.* Nairobi. Oxford University Press.

Thiong'o, N. (2004). *Murogi wa Kagogo.* Nairobi. East African Educational Publishers Ltd.

___________ (2005). *Wizard of the Crow.* New York: Pantheon.

TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi. Oxford University Press.

_________(2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Toleo la Tatu: Dar es salaam. Institute of Kiswahili Research.

Wafula, R.M & Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wales, K. (1989). *A Dictionary of Stylistics.* London: Longman Group.

Walibora, K. (2010). *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Swahili Forum 17(2010): 143-157.

Wamitila, K.W (1991) *Nagona and Mzingile:* Kezilahabi's Metaphysics. Kiswahili 60: 62-67.

________ K.W. (1999). *Unlocking Katana Mkangi's Walenisi. A Case of parabolic narrative?* Kiswahili 61:83-93.

___________ (2001). *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers.

___________(2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

____________(2002) *Uhakiki wa Fasihi; Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi Phoenix Publishers Ltd.

___________ (2003). *Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's Nagona* and *Mzingile* and Juan Rulfo's *Pedro Paramo*. Kiswahili 66:49-58.

___________ (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publications Ltd.

___________ (2004). *Musaleo!* Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

_____________(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Warnes, C. (2006). *Magic Realism and German Idealism. Modern Language Review.* 101/2:488-498.

Williams, R. (1995). *The Postmodern Novel in Latin America: Politics, Culture, and the Crisis of Truth*. New York: St. Martin's.

Williams, R. (1999). *Marxism and Literature*. New York. New York University Press.

Zamora P.L. & Faris B.W. (1995). *Margical Realism: Theory, History and Community.* London. Duke University Press.